**NAFASI YA FASIHI KATIKA UFUNDISHAJI WA LUGHA YA PILI KWENYE MUKTADHA WA MTAALA UNAOEGEMEA UWEZO:** ***MFANO WA SHULE TEULE ZA SEKONDARI WILAYANI RUSIZI, RWANDA***

**Donard BIKORIMANA**

Tasinifu iliyowasilishwa ikiwa ni Sehemu ya Kukamilisha Shahada ya Umahiri wa Elimu katika Kiswahili na Elimu katika Chuo Kikuu cha Rwanda, Ndaki ya Elimu

CHUO KIKUU CHA RWANDA

Aprili, 2022

## ITHIBATI YA MSIMAMIZI

Aliyetia saini hapa chini anathibitisha kuwa ameisoma tasinifu hii yenye anwani ya **Nafasi ya Fasihi katika Ufundishaji wa Lugha ya Pili kwenye Muktadha wa Mtaala Unaoegemea Uwezo :** ***Mfano wa Shule Teule Wilayani Rusizi, Rwanda***, na kwamba imefanywa chini ya usimamizi wake na anapendekeza ikubaliwe na Chuo Kikuu cha Rwanda, Ndaki ya Elimu kwa ajili ya tunzo ya Shahada ya Umahiri katika Kiswahili na Elimu.

…………………………………………


Dkt. W. K. Mlaga

(Msimamizi)

Tarehe ………………………………

## IKIRARI NA HAKIMILIKI

Mimi **Donard BIKORIMANA**, ninathibitisha kwamba tasinifu hii ni kazi yangu halisi, na haijawahi kuwasilishwa na wala haitawasilishwa katika Chuo Kikuu kingine chochote kwa ajili ya kutunukiwa shahada yoyote.



Saini

Hairuhusiwi kuiga, kuchapisha, kutoa nakala, kutafsiri wala kusambaza sehemu yoyote ya tasinifu hii kwa namna yoyote ile bila kibali cha maandishi kutoka kwa mwandishi au Chuo Kikuu cha Rwanda.

## SHUKURANI

Ninatoa shukurani zangu za dhati kwa Mola Muumba na Mlinzi wa watu wake, kwa kunijalia afya njema na kunipa uwezo wa kufanya utafiti, kuandika, na kuikamilisha tasinifu hii.

Ninatoa shukurani za kipekee kwa msimamizi wangu, Dkt.Wallace. K. Mlaga. Licha ya majukumu yake mengi ya kitaaluma, kiofisi na kifamilia yaliyomkabili, alijitolea kuniongoza na kunishauri hatua kwa hatua hadi mwisho wa utafiti huu. Msimamizi huyu alikuwa mshauri, mwelekezaji na mwalimu aliyenikosoa na kunielekeza kwa busara na hekima kubwa wakati wowote ilipohitajika. Sina cha kumlipa lakini ninamwombea wa Mwenyezi Mungu amzidishie moyo wa upendo na ampe nguvu zaidi. Ulinzi wa Mola umwezeshe kuendelea kuwa hazina kubwa yenye kutegemewa kusudi wanufaike wengi wa enzi hizi na zijazo. Aidha, ninaushukuru uongozi mzima wa Chuo Kikuu cha Rwanda, hasa walimu waliopo katika Ndaki ya Elimu kwa kunifundisha, na kunishauri mpaka kukamilika kwa tasinifu hii.

Ninawashukuru sanawazazi wangu. Shukurani za dhati ni kwa mama yangu mpenzi, Bi. Philoménè Nyirandabizi kwa kunizaa na kunilea kwa kadri alivyojaliwa na Mwenyezi Mungu. Asante sana kwa kunilea, kunisomesha, kunishauri na kuendelea kuwa rafiki mwema na wa kweli katika maisha yangu. Ninakupenda sana, mwenyezi Mungu aendelee kukutunza na kukubariki. Ninaishukuru familia ya Bw. Théobald Bavugamenshi na Seraphine Mutumwinka na familia ya Bw. Joas Tugizimana na Collete Nyirahakuzimana. Shukurani maalumuni kwa walimu wangu wote kutoka shule za chekechea hadi chuoni. Pia, nitumie maneno machache kuwashukuru wote ambao kwa namna moja au nyingine wameshirikiana nami katika kukamilisha kazi hii. Sina fursa ya kuwataja wote, ila ninawashukuru sana kwa michango yenu.

## TABARUKU

Ninaitabaruku tasinifu hii kwamama yangu Philomène Nyirandabizi pamoja na familia ya Théobald Bavugamenshi na Seraphine Mutumwinka. Hawa ndio walimu wangu wa awali ambao walinipatia elimu ya msingi iliyonisaidia kuwa jinsi nilivyo leo. Kazi hiini matunda ya jitihada zao kubwa na za muda mrefu walizowekeza kwangu. Pia, ninaitabaruku tasinifu hii kwa familia ya Jean Claude Ndagijimana na Herène Mushimiyimana pamoja na familia ya Jean Pierre Ndayambaje na Ellen Akingeneye. Mwisho, ninaitabaruku kwa Wanyarwanda, Waafrika na watu wote wenye moyo na ari ya kuendeleza lugha ya Kiswahili kama utambulisho wa Mwafrika.

## IKISIRI

Tasinifu hii inayoitwa “*Nafasi ya Fasihi katika Ufundishaji wa Lugha ya Pili kenye Muktadha wa Mtaala Unaoegemea katika Uwezo: Mfano wa Shule Teule Wilayani Rusizi, RWANDA*" ina malengo mahususi mawili. Lengo la kwanza ni kutathimini ufaafu wa fasihi katika ufundishaji wa lugha ya pili na utekelezaji wa mtaala unaoegemea katika uwezo kwa wanafunzi wa Kiswahili wa kidato cha tano. Lengo la pili ni kubainisha namna fasihi inavyoweza kutumika katika ufundishaji wa lugha ya pili na utekelezaji wa mtaala unaoegemea katika uwezo kwa wanafunzi wa Kiswahili wa kidato cha tano. Taarifa zilipatikana kwa njia ya mahojiano, ushuhudiaji, na mapitio ya maandiko. Sampuli iligawanyika katika makundi mawili ambayo ni watu na kazi za fasihi. Sampuli ya watu ni walimu na wanafunzi wa Kiswahili katika kidato cha tano katika shule za sekondari, ilhali sampuli ya kazi za fasihi ilihusishakazi tofauti za fasihi andishi na fasihi simulizi. Sampuli ilipatikana kwa mbinu ya sampuli lengwa. Uchambuzi wa data umeegemezwa katika nadharia mbili ambazo ni Utambuzi na Maingiliano ya Tamaduni-Jamii. Matokeo ya utafiti uliofanyika yanaonesha kwamba fasihi hujumuisha mifano bora ya kufundishia lugha ya pili. Hii ni kutokana na hoja kwamba katika kazi za fasihi, inapatikana mifano ya kufundisha sarufi, msamiati na stadi zote za lugha. Pia, Matokeo ya utafiti uliofanyika yamebaini kwamba fasihi hutoa mifano ya uwezo wa jumla na masuwala mtambuka ikiwemo thamani na mwenendo mwema. Pamoja na hayo, utafiti umebaini kwamba fasihi hufaa kwa kufundishia lugha ya pili kwa upande mmoja na kutekeleza mtaala unaoegemea katika uwezo kwa upande mwingine. Mwisho, utafiti umeonesha namna ambavyo fasihi inavyoweza kutumiwa kama nyenzo ya kufundishia lugha ya pili na kutekeleza mtaala unaoegemea katika uwezo.

## YALIYOMO

**ITHIBATI YA MSIMAMIZI** .......... **i**

**IKIRARI NA HAKIMILIKI** .......... **ii**

**SHUKURANI** .......... **iii**

**TABARUKU** .......... **iv**

**IKISIRI** .......... **x**

**YALIYOMO** .......... **x**

**ORODHA YA VIFUPISHO NA UFAFANUZI** .......... **ix**

**SURA YA KWANZA** .......... **1**

**UTANGULIZI WA JUMLA** .......... **1**

1.1 Utangulizi .......... 1

1.2 Usuli wa Tatizo la Utafiti .......... 1

1.3 Tamko la Tatizo la Utafiti .......... 4

1.4 Malengo ya Utafiti .......... 5

1.4.1 Lengo la Jumla .......... 5

1.4.2 Malengo Mahususi .......... 5

1.5 Maswali ya Utafiti .......... 5

1.6 Manufaa ya Utafiti .......... 6

1.7 Mawanda ya Utafiti....7
1.8 Muhtasari wa Sura ya Kwanza ....7
**SURA YA PILI....8**
**MAPITIO YA MAANDIKO NA KIUNZI CHA NADHARIA ....8**
2.1 Utangulizi....8
2.2 Mapitio kuhusu Fasihi....8
2.3 Lugha ....9
2.4 Ufundishaji wa Lugha ya Pili ....9
2.5 Utumizi wa Fasihi katika Ufundishaji wa Lugha ya Pili ....11
2.6 Mtaala Unaoegemea katika Uwezo ....14
2.7 Nafasi ya Fasihi katika Ukuzaji wa Uwezo wa Mwanafunzi ....17
2.8 Mapengo Yanayojitokeza Kutokana na Mapitio ya Maandiko ....18
2.9 Kiunzi cha Nadharia za Utafiti ....19
2.9.1 Nadharia ya Utambuzi ....19
2.9.2 Nadharia ya Maingiliano ya Tamaduni-jamii....21
2.9.3 Jinsi Nadharia ya Utambuzi na Maingiliano ya Tamaduni-jamii Zilivyotumika ....22
2.10 Muhtasari wa Sura ya Pili....23
**SURA YA TATU: METHODOLOJIA YA UTAFITI ....24**
3.1 Utangulizi....24
3.2 Usanifu wa Utafiti....24

3.3 Eneo la Utafiti ........................................................................................................ 24

3.4 Wango na Sampuli ya Utafiti.............................................................................. 25

3.4.1 Wango la Utafiti................................................................................................ 25

3.4.2 Sampuli na Usampulishaji wa Utafiti ................................................................ 25

3.5 Ukusanyaji wa Data ............................................................................................ 26

3.5.1 Njia ya Ushuhudiaji ........................................................................................... 27

3.5.2 Njia ya Uchanganuzi wa Matini ........................................................................ 28

3.5.3 Njia ya Usaili ..................................................................................................... 28

3.6 Uchanganuzi wa Data ......................................................................................... 28

3.7 Itikeli za Utafiti ................................................................................................... 29

3.8. Uhalali na Uthabiti wa Utafiti............................................................................ 30

3.9 Muhtasari wa Sura ya Tatu ................................................................................. 30

**SURA YA NNE: UWASILISHAJI, UCHAMBUZI WA DATA NA MJADALA WA MATOKEO.** ........................................................................................................ 31

4.1 Utangulizi............................................................................................................ 31

4.2 Ufaafu wa Fasihi katika Ufundishaji wa Lugha ya Pili kwenye Muktadha wa Utekelezaji wa Mtaala Unaoegemea katika Uwezo. ......................................................................... 31

4.2.1 Utayari wa Walimu katika Utumizi wa Fasihi Kufundishia Lugha na Kutekeleza Mtaala 32

4.2.2 Fasihi katika Ufundishaji wa Lugha ya Pili ...................................................... 33

4.2.2.1 Fasihi kama Nyenzo ya Kufundishia Sarufi .................................................. 33

4.2.2.2 Fasihi katika Ufundishaji wa Msamiati ......................................................... 35

4.2.2.3 Fasihi katika Ufundishaji wa Stadi ya Kusoma ........................................................ 37

4.2.2.4 Fasihi kama Nyenzo ya Kufundishia Stadi ya Kuandika............................................ 38

4.2.2.5 Fasihi na Ufundishaji wa Stadi za Kuzungumza na Kusikiliza .................................. 40

4.2.3 Ufaafu wa Fasihi katika Utekelezaji wa Mtaala Unaoegemea katika Uwezo ................ 42

4.2.3.1 Fasihi katika Ukuzaji wa Tafakuri Tunduizi ............................................................. 43

4.2.3.2 Fasihi na Ukuzaji wa Utafiti na Utatuzi wa Matatizo ................................................. 44

4.2.3.3 Fasihi kama Nyenzo ya Ukuzaji wa Ubunifu na Ugunduzi ........................................ 45

4.2.3.4 Fasihi katika Ukuzaji wa Stadi za Mawasiliano ........................................................ 46

4.2.3.5 Ukuzaji wa Ushirikiano, Utawala Binafsi na Stadi za Maisha Kupitia Fasihi ............ 47

4.2.3.6 Fasihi kama Nyenzo ya Ukuzaji wa Ujifunzaji usio na Mpaka .................................. 49

4.2.4 Fasihi kama Njia ya Ufafanuzi wa Maswala Mtambuka ................................................ 51

4.2.4.1 Fasihi na Ujasiriamali ............................................................................................... 52

4.2.4.2 Fasihi na Usawa wa Jinsia ......................................................................................... 52

4.2.4.3 Fasihi na Elimu kuhusu Ufahamu wa Jinsia na UKIMWI .......................................... 53

4.2.4.4 Fasihi na Elimu kuhusu Utunzi wa Mazingira na Usafishaji...................................... 54

4.2.4.5 Fasihi na Thamani na Mitazamo ................................................................................ 54

4.3 Namna ya Kuitumia Fasihi Kufundishia Lugha katika Muktadha wa Mtaala Unaoegemea katik Uwezo ........................................................................................................................ 55

4.3.1 Utumizi wa Fasihi katika Ufundishaji wa Sarufi .......................................................... 55

4.3.2 Fasihi kama Nyenzo ya Kufundishia Msamiati ............................................................ 56

4.3.3 Jinsi ya Kuitumia Fasihi katika Ufundishaji wa Stadi za Lugha .................................... 58

4.3.3.1 Utumizi wa Fasihi katika Ufundishaji wa Stadi ya Kuandika ....................................60

4.3.3.2 Namna ya Ufundishaji wa Stadi ya Kusoma Kupitia Fasihi.......................................61

4.3.3.3 Jinsi ya Kuitumia Fasihi kama Nyenzo ya Ufundishaji wa Stadi za Kusikiliza na Kuzungumza ....................................................................................................................62

4.3.4 Namna ya Ukuzaji wa Uwezo wa Jumla Kupitia Fasihi................................................65

4.3.4.1 Jinsi ya Kuitumia Fasihi Kukuza Tafakuri Tunduizi. .................................................65

4.3.4.2 Namna ya Ukuzaji wa Utafiti na Utatuzi wa Matatizo Kupitia Fasihi ........................67

4.3.4.3 Jinsi ya Utumizi wa Fasihi kama Nyenzo ya Ukuzaji wa Ubunifu na Ugunduzi.........68

4.3.4.4 Kukuza Stadi za Mawasiliano Kupitia Fasihi .............................................................70

4.3.4.5 Ukuzaji wa Ushirikiano, Utawala Binafsi na Stadi za Maisha Kupitia Fasihi ............72

4.3.4.6 Fasihi katika Ukuzaji wa Ujifunzaji usio na Mpaka...................................................73

4.3.5 Namna ya Kuitumia Fasihi Kufundisha Maswala Mtambuka.......................................74

4.3.6 Uteuzi na Uchaguzi wa Kazi za Fasihi katika Ufundishaji wa Lugha naUkuzaji wa Uwezo wa Mwanafunzi 76

4.4 Muhtasari wa Sura ya Nne ..........................................................................................77

**SURA YA TANO ..........................................................................................................78**

**HITIMISHO.................................................................................................................78**

5.1 Utangulizi....................................................................................................................78

5.2 Muhtasari waTasinifu ..................................................................................................78

5.3 Utoshelevu wa Nadharia za Uchambuzi wa Data............................................................80

5.4 Mchango Mpya wa Utafiti Huu .......................................................................................81

5.5 Maoni kuhusu Utafiti Huu .......... 82

5.6 Mambo Yanayotakiwa Kuzingatiwa ili Kuondokana na Changamoto .......... 83

5.7 Mapendekezo .......... 84

5.7.1 Mapendekezo kwa Walimu na Wanafunzi .......... 84

5.7.2 Mapendekezo kwa Watunzi wa Fasihi kwa Jumla .......... 84

5.7.3 Mapendekezo kwa Serikali na Wakuzaji Mitaala .......... 85

5.7.4 Mapendekezo kwa Tafiti Zijazo .......... 85

**MAREJELEO .......... 98**

**VIAMBATANISHO .......... A**

## ORODHA YA VIFUPISHO NA UFAFANUZI

Ihj................................... Ishatajwa hapo juu

Khj……….…………… Keshatajwa hapo juu

Whj…………………… Wameshatajwa hapo juu

REB…………………... Rwanda Education Board

UNICEF……………..... United Nations International Children's Emergency Fund

Bw……………………. Bwana

Bi……………………...Bibi

Dkt ................................Daktari

OECD…………………Organisation for Economic Co-operation and Development

# SURA YA KWANZA

# UTANGULIZI WA JUMLA

## 1.1 Utangulizi

Utafiti uliofanyika ulihusu nafasi ya fasihi katika ufundishaji wa lugha ya pili na utekelezaji wa mtaala unaoegemea katika uwezo kwa kutumia mfano wa ufundishaji wilayani Rusizi.Utafiti ulilenga kueleza fasihi na mchango wake katika ufundishaji wa lugha kwa upande mmoja na utekelezaji wa mtaala unaoegemea katika uwezo kwa upande mwingine kulingana na darasa teule. Sura ya kwanza ni sura tangulizi inayofafanua masuala mbalimbali ya kuutambulisha utafiti. Hivyo, sura hii inahusu ufafanuzi wa istilahi muhimu, usuli wa tatizo la utafiti, tamko la tatizo la utafiti, malengo ya utafiti, maswali ya utafiti, manufaa ya utafiti, na mawanda ya utafiti.

## 1.2 Usuli wa Tatizo la Utafiti

Kwa muda mrefu, mikabala ya kimuundo na kidhima ya ufundishaji wa lugha ilipuuza fasihi kama nyenzo ya kufundishia lugha. Kutokana na mikabala ya kimuundo, utumizi wa fasihi katika kufundisha lugha hutazamwa kama mbinu ya kijadi. Hii ni kwa sababu mbinu ya kisasa ya ufundishaji wa lugha inasisitiza utumizi wa mawasiliano halisi na wala sio utumizi wa fasihi (Collie na Slater,1987 katika Hapsari, 2016)

Kwa mujibu wa mikabala ya kidhima, umuhimu wa lugha hutazamwa katika mawasiliano halisi ya lugha kama vile kuitumia lugha kwa malengo ya kibiashara, kuitumia hotelini au katika safari, kuitumia kununua vitu sokoni, na kununua chakula katika migahawa na kadhalika. Kwa hivyo, mikabala hii haiitazami fasihi kuwa mfano wa mawasiliano au mfano halisi wa matumizi ya lugha (Rahman, 2018). Kwa mtazamo wetu, maoni ya mikabala hii hayana mashiko wala ukweli kwa sababu hata misingi ya mbinu ya ufundishaji wa lugha kimawasiliano haipuuzi utumizi wa fasihi katika ufundishaji na ujifunzaji wa lugha.

Sio ajabu kuona kuwa wanaisimu na wataalamu wa lugha wamefikiria tena na kufufua nia ya fasihi kuwa mojawapo ya nyenzo muhimu sana za kufundishia na kujifunzia lugha. Fasihi ni nyenzo muhimu katika ufundishaji wa lugha ya pili (Lazar, 1993 katika Hapsari, 2016) Wataalam kama Bradford (2015) na Starja (2015) nao wanatanabahisha kwamba usomaji wa

fasihi unaweza kuwasaidia wanafunzi kujifunza au kuongeza msamiati, pia kuzoea mifumo fulani ya kisintaksia ambayo sio ya kawaida katika lugha ya kimazungumzo.

Aidha, Hapsari (2016) na Starja (2015) wanakubaliana kwamba utumizi wa fasihi katika ufundishaji na ujifunzaji wa lugha, unasaidia kujifunza fasihi na lugha kwa wakati mmoja. Kingine ni kwamba husaidia kuelewa mifumo ya kifasihi, kujifunza tamathali za usemi kutokana na kazi za fasihi na kujifunza misemo ya lugha lengwa isiyoweza kupatikana katika mazungumzo ya kawaida. Zaidi ya hivyo, husaidia wanafunzi kufikiria kuhusu lugha na kukuza umilisi wa kimawasiliano. Hivyo basi, fasihi si somo tu bali ni nyenzo ya kufundishia lugha. Kutokana na mawazo ya wataalamu hawa, pamoja na ujuzi unaopatikana kupitia fasihi, tunaona kwamba utumizi wa fasihi katika ufundishaji wa Kiswahili nchini Rwanda, bila shaka unaweza kuwa njia nzuri katika ufikiaji wa malengo ya ufundishaji na ujifunzaji wa lugha hii.

Utumizi wa fasihi katika ufundishaji wa lugha ya pili haulengi kufundisha lugha tu bali unalenga kumwelimisha mtu katika ukamilifu wake kwa upande mwingine (Lazar,1993 katika Hapsari, 2011). Wazo la Lazar (khj) linahusiana sana na kueleza umuhimu wa fasihi kama nyenzo ya kufundishia lugha kwa upande mmoja na utekelezaji wa mtaala unaoegemea katika uwezo kwa upande mwingine. Hata hivyo, tatizo linalowakumba walimu na wataalamu katika elimu ni pamoja na kuamua maana ya neno "uwezo" katika kila eneo la somo na kutambua njia za wanafunzi za kuonesha uwezo huo (Nodine, 2015). Chu na wenzake (2020) wanafafanua uwezo ni seti ya ujuzi, maarifa na tabia ambazo mtu anahitaji kuwa nazo ili kufanya majukumu mbalimbali, kazi au shughuli katika ulimwengu wa kazi.

OECD mnamo mwaka wa (2020) ilifanya utafiti kuhusu utekelezaji wa mtaala unaoegemea katika uwezo nchini Welisi ambayo ni mojawapo ya nchi inayotumia mtaala unaoegemea katika uwezo kama ilivyo kwa nchi ya Rwanda. Utaftiti wa OECD (khj) unaonesha kuwa walimu wanasifu mtaala unaoegemea katika uwezo. Wanautazama mtaala huu kama njia mpya ya kujifunza na kujenga wakati ujao kwa kuendana na maendeleo ya karne ya 21. Hii ni kutokana na ukweli kwamba msingi wa mtaala huu ni kuwapa wanafunzi heshima na fursa ya kuwasilisha uwezo na ujuzi wao, unaolenga kuwezesha wanafunzi kukuza, kuunganisha na kutumia uwezo unaohitajika, kama vile utatuzi wa matatizo, tafakuri tunduizi, ubunifu, teknolojia ya habari, ushirikiano na ujifunzaji usio na mpaka (Nzima, 2016).

Hivyo, inapochunguza ni kwa namna gani fasihi inaweza kutumika katika kutekeleza mtaala unaoegemea katika uwezo ni pamoja na kujikita kuangalia ni kwa namna gani fasihi ina nafasi

ya kukuza uwezo huu miongoni mwa wanafunzi. Hata muhtasari wa Kiswahili unaotumika hivi sasa nchini Rwanda, unasisitiza uwezo huu kwa kuurejelea kama uwezo wa jumla (REB, 2015)

Fasihi inatazamwa kama mshituo wa tafakari ya kibinafsi na uelewa wa mitazamo mingine, ambayo ni kama njia ya kufikia na kupitisha maoni mapya (Wakala wa Kitaifa wa Elimu wa Uswidi, 2012 katika Wintersparv, 2020 : 58). Wakala huu unafafanua malengo ya kuingiza fasihi katika mtaala wa taifa la Uswidi kwa kusema :

> A closer look at how the literary part is framed reveals the aim to develop students' ability to work with different kinds of texts, their understanding of the distinctive as well as the temporally and spatially universal values and characteristics of literature.
>
> Kwa mtazamo wa kimakini kuhusu jinsi ambavyo sehemu ya fasihi imeandaliwa inaonyesha lengo la kukuza uwezo wa wanafunzi wa kufanya kazi na matini za namna tofauti, uelewa wao wa kuonesha utofauti vilevile kwa muda fulani na hata kwa thamani na sifa za fasihi za kiulimwengu [Tafsiri Yetu]

Uswidi ni nchi mojawapo inayotumia mtaala unaoegemea katika uwezo kama ilivyo kwa nchi ya Rwanda. Maoni ya Wakala wa Kitaifa wa Elimu wa Uswidi nafafanua lengo la kuingiza kipengele cha fasihi katika mtaala wao kwa shule za sekondari. Malengo yao ni kukuza uwezo wa mwanafunzi usio wa kiwango cha darasani tu bali pia kwa kiwango cha kiulimwengu kupitia fasihi. Hoja hii inaendana na ile ya ujenzi wa uwezo wa mtu ambaye anafaa kushindana kwenye soko la ajira la kiulimwengu. Kama inavyoelezwa na UNICEF (2019), mshindani bora kwenye soko la ajira la kiulimwengu ni yule mwenye stadi za karne ya 21 ambazo wengine huziita stadi za maisha, stadi zinazohamishika au ujuzi laini. Stadi hizo ni pamoja na utatuzi wa matatizo, majadiliano, kudhibiti hisia, huruma na mawasiliano miongoni mwa mengine, kufanya kazi kwa kuunganisha maarifa na thamani, kuimarisha, na kuendeleza ujuzi mwingine na kujenga maarifa zaidi (UNICEF, 2019). Hivyo basi, hatuna budi kusema kwamba lengo kuu la mtaala unaoegemea katika uwezo ni kumsaidia mwanafunzi kukuza stadi za karne ya 21 ambazo zitamwezesha kushindania kazi popote afikapo. Pamoja na maelezo haya yote mazuri, bado haielezwi ni kwa namna gani fasihi inaweza kutumiwa

kukuza uwezo huu wa muhimu katika maisha ya mwanafunzi ya sasa na katika maisha yake yote kwa ujumla.

Kama inavyoelezwa na REB (2015), mtaala unaoegemea katika uwezo nchini Rwanda, unatarajiwa kukuza uwezo ufuatao: Mosi, uwezo wa mwanafunzi katika kufikiria kwa umakini kuhusu mambo yanayojitokeza na yale anayoweza kukutana nayo maishani haswa kuendana na mabadiliko ya ulimwengu (tafakuri tunduizi). Pili, uwezo wa kuendeleza mchakato wa kutafuta na kupata masuluhu ya maswali na matatizo yanayoweza kumkabili mwanafunzi katika lugha na hata maishani (utafiti na utatuzi wa matatizo). Tatu, uwezo wa kujenga mawazo mapya na kuvumbua mambo yanayohitajika katika jamii yake na hata nje ya jamii (ubunifu na ugunduzi). Nne, uwezo wa kutumia na kuzungumza lugha inayofaa kulingana na muktadha anaoufikia mwanafunzi (stadi za mawasiliano). Tano, ujuzi muhimu wa kuishi vizuri na watu wengine wa jamii yoyote ile anayoifikia katika mchakato wa ujishughulishaji binafsi na urizikaji wa mahitaji yake ya kila siku (ushirikiano, utawala binafsi na stadi za maisha). Sita, uelewa wa kwamba elimu haina mpaka yaani anatarajiwa kujifunza kila wakati kutoka watu wa jamii yake, shuleni, vitabu na makala, mtandaoni na namna nyingine zinazoweza kumsaidia kupata ujuzi na maarifa mapya (ujifunzaji usio na mpaka) (REB, 2015). Hivyo, hata kwa upande wa REB (Ihj), wanatusaidia tu kubainisha uwezo muhimu unaopaswa kukuzwa na kujengwa miongoni mwa wanafunzi lakini hatuelezwi ni namna gani uwezo huu unaweza kukuzwa.

### 1.3 Tamko la Tatizo la Utafiti

Elimu ya kisasa imeegemezwa katika uwezo wa mwanafunzi ambapo mwanafunzi anaandaliwa kukabiliana na changamoto za ulimwengu halisi (UNESCO, 2017; Kabombwena Mulenga, 2019). Nchi nyingi ikiwepo Rwanda, zilianzisha mtaala unaoegemea katika uwezo kwa lengo kuu la kuandaa mtu afaaye katika soko la ajira la kiulimwengu (REB & MINEDUC, 2015). Mtaala unaoegemea uwezo ulioanzishwa nchini Rwanda unakabiliwa na changamoto za ukuzaji wa uwezo wa jumla miongoni mwa wanafunzi na ujumuishaji wa maswala mtambuka katika kila somo (Nsengimana, 2021; Urunana rw'abarezi, 2018).

Aidha, kutokana na mawazo ya wataalamu kama Lazar (1993) na Hapsari (2011), fasihi ni nyenzo isiyo ya kufundishia lugha tu bali hukuza uwezo wa mwanafunzi na kujumuisha mitazamo na mwenendo mwema kwa watumizi wake. Hata hivyo, hakuna maandiko wala tafiti zinazoeleza nafasi ya fasihi katika ufundishaji wa lugha ya pili kwa upande mmoja na

utekelezaji wa mtaala unaoegemea uwezo kwa upande mwingine. Hivyo basi, utafiti uliofanyika ulichunguza ufaafu wa fasihi na namna inavyoweza kutumiwa kama nyenzo ya ufundishaji wa lugha ya pili na utekelezaji wa mtaala unaoegemea katika uwezo kupitia wanafunzi wa lugha katika shule za sekondari nchini Rwanda, Wilayani Rusizi.

### 1.4 Malengo ya Utafiti

Utafiti uliofanyika uliongozwa na malengo ya aina mbili ambayo ni: Lengo la jumla moja na malengo mahususi mawili.

#### 1.4.1 Lengo la Jumla

Utafiti ulilenga kuchunguza nafasi ya fasihi sio tu kama nyenzo ya ufundishaji na ujifunzaji wa lugha ya pili bali kama nyenzo ya utekelezaji wa mtaala unaoegemea katika uwezo katika shule za sekondari nchini Rwanda zinazofundisha Kiswahili.

#### 1.4.2 Malengo Mahususi

Malengo mahususi ya utafiti uliofanyika ni haya yafuatayo:

a) Kutathimini ufaafu wa fasihi katika ufundishaji wa lugha ya pili kwenye muktadha wa mtaala unaoegemea katika uwezo kwa wanafunzi wa Kiswahili wa kidato cha tano; na
b) Kubainisha namna fasihi inavyoweza kutumika katika ufundishaji wa lugha ya pili kwa upande mmoja na utekelezaji wa mtaala unaoegemea katika uwezo kwa upande mwingine kwa wanafunzi wa Kiswahili wa kidato cha tano.

### 1.5 Maswali ya Utafiti

Maswali yaliyouongoza utafiti ni yafuatayo:

a. Kwa kiwango gani fasihi inaweza kufaa kutumiwa katika ufundishaji wa lugha ya pili kwenye muktadha wa mtaala unaoegemea katika uwezo?
b. Ni namna gani fasihi inaweza kutumika katika ufundishaji lugha ya pili na utekelezaji wa mtaala unaoegemea katika uwezo kwa wakati mmoja?

## 1.6 Manufaa ya Utafiti

Katika miongo kadhaa iliyopita, taaluma ya isimu na ufundishaji na ujifunzaji wa lugha imekuwa maeneo ya kufanyia tafiti nyingi. Tafiti hizi hadi leo zinaendelea kuchangia sana katika uendelezaji na uboreshaji wa ufundishaji na ujifunzaji wa lugha ya pili (Dubiner, 2020). Kwa hivyo, utafiti uliofanyika kuhusu uboreshaji wa ufundishaji na ujifunzaji wa lugha ya pili na utekelezaji wa mtaala unaoegemea katika uwezo ni muhimu sana kwa sababu zifuatazo:

Mosi, utumizi wa fasihi kama nyenzo ya kufundishia lugha unaweza kufanya mataifa na wadau wa elimu kufikiria tena kuhusu nafasi ya fasihi, jinsi ya kuitumia ipasavyo, kuunda na kutoa rasilimali za fasihi zinazofaa kwa kufundishia lugha na kusaidia katika utekelezaji wa mtaala unaoegemea katika uwezo.

Pili, matokeo ya utafiti huu yataweka wazi athari za fasihi katika ufundishaji na utekelezaji wa mtaala unaoegemea katika uwezo kwa kuwasaidia watunga mitaala kufikiria, kuthamini na kuingiza fasihi kama nyenzo ya kufundishia lugha katika mtaala unaoegemea katika uwezo.

Tatu, matokeo ya utafiti yatazichochea taasisi za kielimu na shule kwa kukagua walimu na washiriki wengine wa moja kwa moja katika elimu ya wanafunzi kuthamini fasihi na kuitumia katika ufundishaji wa lugha kwa wanafunzi, kuandaa na kutumia nyenzo na vifaa vya kifasihi.

Nne, utafiti utaeleza jinsi ya kutumia fasihi katika ufundishaji wa lugha ya pili kwa kuwasaidia walimu na wanafunzi wa lugha kupata uelewa kuhusu ufundishaji na ujifunzaji wa lugha kupitia fasihi. hivyo basi, utafiti huu utawaongezea walimu na wanafunzi uwezo wa kihakiki kuhusu fasihi na kuweza kujichagulia fasihi inayofaa kwa kufundishia kiwango fulani cha wanafunzi.

Tano, utafiti huu utaweka wazi nafasi ya fasihi na jinsi ya kuitumia katika kufanikisha ufundishaji wa lugha ya pili na utekelezaji wa mtaala unaoegemea katika uwezo. Hii itasaidia jamii kubwa ya ulimwengu katika kuendeleza na kuongeza fursa ya upataji, uzungumzaji na utumizi wa lugha mbalimbali katika ufanikishaji wa shughuli za kimaisha.

### 1.7 Mawanda ya Utafiti

Utafiti wowote unatakiwa uwekewe mipaka (Ponera, 2019). Hii ndiyo maana utafiti uliofanyika ulijielekeza katika kuchunguza nafasi ya fasihi katika ufundishaji waKiswahili ambayo ni lugha ya pili kwa watafitiwa walengwa. Utafiti ulilenga kutathmini jinsi fasihi inavyoweza kutumiwa katikaa kufanikisha ujifunzaji wa lugha na utekelezaji wa mtaala unaoegemea katika uwezo. Pia, utafiti uligusia athari za fasihi kwa wanafunzi wa Kiswahili Wilayani Rusizi. Ulichunguza kiwango ambacho fasihi inaweza kufaa katika ufundishaji wa lugha na utekelezaji wa mtaala unaoegemea uwezo. Utafiti huu ulitumia baadhi ya kazi za fasihi simulizi na andishi zinazopatikana katika kitabu cha Kiswahili kwa mwanafunzi kidato cha tano katika shule za sekondari nchini Rwanda. Aidha, utafiti huu haukuingilia uchambuzi na uhakiki wa vipengele vya fani na maudhui vya kazi zilizotumiwa.

### 1.8 Muhtasari wa Sura ya Kwanza

Sura hii imefafanua istilahi muhimu zilizotumika katika utafiti uliofanyika, usuli wa tatizo la utafiti, tamko la tatizo la utafiti, malengo ya utafiti, maswali ya utafiti, manufaa ya utafiti, na mawanda ya utafiti. Sura inayofuata inahusiana na mapitio ya maandiko, na kiunzi cha nadharia.

# SURA YA PILI

# MAPITIO YA MAANDIKO NA KIUNZI CHA NADHARIA

## 2.1 Utangulizi

Sehemu hii inahusu mapitio mbalimbali yaliyopitiwa na kutumiwa katika utafiti huu. Mapitio hayo yamegawanyika katika makundi sita. Makundi hayo ni: mapitio kuhusu fasihi, mapitio kuhusu lugha, mapitio kuhusu ufundishaji wa lugha ya pili, mapitio kuhusu utumizi wa fasihi katika ufundishaji wa lugha ya pili, mapitio kuhusu mtaala unaoegemea katika uwezo na mapitio kuhusu nafasi ya fasihi katika ukuzaji wa uwezo wa mwanafunzi.

## 2.2 Mapitio kuhusu Fasihi

Wataalamu wengi walioshughulikia swala la maana ya neno fasihi wangali wanaendeleza mjadala huu. Senkoro (1995) anaeleza kuwa mjadala huu haujafikia mwisho wake kwa sababu maswali mengi kuhusu maana ya fasihi hayajapatiwa majibu kikamilifu. Fasihi ni kioo cha maisha ya jamii. Fasihi inaonekana kuwa kitu kipana ambacho kinahitaji tafiti nyingi zaidi kutokana na utata wake. Utata huo wa kimaana unaleta athari nyingi katika taaluma mbalimbali haswa za kielimu. Athari hizi mara nyingi zinatokana na kwamba wahusika wa fasihi kama somo hawaelewi kwa uwazi mambo mengi yanayohusiana na fasihi kwa jumla.

Ntarangwi (2004) na Wamitila (2004) wanakubaliana kwamba fasihi ni sanaa inayotumia lugha kwa kutoa picha halisi ya maisha ya mwanadamu akiwa maishani mwake; mahusiano yake na viumbe wengine, migogoro yake na mazingira, shida zake, raha zake, matumaini yake, na jinsi anavyopiga hatua katika maendeleo yake. Ni sanaa inayotumia lugha katika kuwasilisha ujumbe wa mdomo au wa maandishi (Williady, 2015). Wataalamu hawa wote wanatumia maneno kama vile "sanaa inayotumia lugha" na "binadamu au jamii." Hii inamaanisha kwamba ili sanaa fulani iitwe fasihi ni lazima iwe inatumia lugha kiubunifu kwa kuwasilisha maisha ya mwanadamu au jamii ya watu. Hivyo basi, tunaweza kusema kwamba fasihi ni aina ya ufundi unaotumia lugha ili kugusia na kuwasilisha maisha ya mwanadamu ya kila siku. Kutokana na maelezo ya wataalamu hawa, tunaangazia mambo mawili muhimu. Mosi, tunaona kwamba fasihi na lugha ni mambo yanayofungamana ambayo hayawezi kuachana. Kwa hivyo, tunamulikiwa kwamba ni rahisi kufundisha lugha kupitia fasihi kwa

kuwa fasihi yoyote ile inatumia lugha. Pili, kutokana na wazo la kwamba fasihi hugusia sehemu zote za maisha ya mwanadamu, ni dhahiri kuwa inaweza kusaidia sana katika utekelezaji wa mtaala unaoegemea katika uwezo.

## 2.3 Lugha

Crystal (1992) anasema kuwa lugha ni mfumo wa sauti nasibu, ishara au maandishi kwa ajili ya mawasiliano na kujieleza katika jamii ya watu. Mambo muhimu yanayojenga fasili ya lugha kama inavyoelezwa na wataalamu hawa, ni pamoja na sauti nasibu, pia kuwasiliana na jamii ya watu. Lugha ni mfumo kwani ina mpangilio maalum ambao unathibitishwa na wanalugha husika kama kanuni za kuitumia kimazungumzo na kimaandishi. Hali hii ndiyo inayowafanya watu kuwa wagumu kujifunza lugha. Hii inamaanisha kuwa kila lugha isingekuwa na mpangilio wake maalum, watu wangezungumza kila lugha bila kujifunza. Lugha ni sauti nasibu kwa kuwa mtu hazaliwi nayo, ila anaikuta katika jamii. Hali hii ndiyo inawafanya watu kuzungumza lugha tofauti kutokana na sehemu za kijiografia au jamii. Lugha ni chombo cha mawasiliano, kwa sababu watu wanashirikisha na kupokea hisia, mawazo, mahitaji, maoni, na mitazamo yao kupitia lugha. Hapa ieleweke vizuri kwamba lugha huwa na kazi ya kuunganisha wanajamii au watumiaji wa lugha husika. Hivyo basi, bila lugha ni vigumu kupata maendeleo wala kufanya tendo fulani kwa ufanisi. Hii ni kutokana na ukweli kwamba “kidole kimoja hakivunji chawa” na pia “umoja ni nguvu.” Lugha ni njia ya kujenga ushirikiano. Mwisho, lugha ni mali ya watu kwa sababu hupaswa kutumiwa na jamii ya watu. Hii ni kutokana na ukweli kwamba wanyama hawazungumzi lugha (Anderson, 2019).

Kutokana na unasibu wa lugha, kumekuwa na lugha nyingi duniani zinazotokana najamii pamoja na sehemu za kijiografia ambazo ni nyingi pia. Hii inasababisha watu kulazimika kujifunza lugha ya jamii fulani kwa ajili ya faida za kimatumizi za lugha husika. Siku hizi, ufundishaji na ujifunzaji unazidi kupiga hatua. Hii mara nyingi hutokana na utandawazi ambapo dunia imekuwa kama kijiji kimoja na kumlazimisha mtu kukutana na watu wengi wenye lugha tofauti.

## 2.4 Ufundishaji wa Lugha ya Pili

Richard na Rodgers (2001) na Richard na Renandya (2002) wanaeleza kuwa karne yote ya 20 ilitawaliwa na tafiti kuhusu mbinu za ufundishaji na ujifunzaji wa lugha ili kutafuta mbinu

moja muafaka ya ufundishaji na ujifunzaji wa lugha. Hata hivyo, wataalamu na watafiti mbalimbali walishindwa kupata mbinu inayofaa kwa mazingira yote ya ufundishaji wa lugha. Kutokana na maandiko haya, inaonekana kwamba hakuna mbinu wala njia hata moja inayojitosheleza katika ufundishaji wa lugha ya pili. Hali hii inaelekeza moja kwa moja kwenye wazo la kwambaupuuzaji wabaadhi ya mbinu katika ufundishaji na ujifunzaji wa lugha ni makosa.

Achillah (2010) alifanya utafiti kuhusu matumizi ya mbinu ya kimuktadha katika ufundishaji wa msamiati wa Kiswahili katika shule za upili za Wilaya ya Kakamega. Utafiti wake ulibaini kwamba walimu wa lugha walitumia fasihi kwa kiwango kikubwa badala ya matini za ufahamu. Utafiti uliofanyika ulichunguza mbinu tofauti zinazotumiwa na walimu katika ufundishaji wa lugha tu bila kutazama upande wa ukuzaji wa uwezo wa jumla kwa mwanafunzi. Hii ndiyo maana katika matokeo ya utafiti wa Achillah (khj) matini za ufahamu zilipata nafasi ya kwanza badala ya fasihi. Kwa hivyo, kama utafiti wake ungechunguza mbinu zinazotumiwa na walimu katika ufundishaji wa lugha kwa upande mmoja na ukuzaji wa uwezo wa jumla kwa upande mwingine, fasihi ingepata nafasi ya kwanza. Kutokana na andiko hili, inaonekana kwamba mwalimu anatarajiwa kujaribu mbinu kadhaa katika mchakato wa ufundishaji na ujifunzaji wa lugha. Hivyo basi, ni vigumu kusema kuwa utumizi wa fasihi ni njia inayojitosheleza. Ila hakuna shaka juu ya umuhimu wake katika ujifunzaji wa lugha kwa upande mmoja na utekelezaji wa mtaala unaoegemea katika uwezo kwa upande mwingine.

Brett (2004) anaeleza kuhusu utafiti uliofanywa na Kituo cha Masomo ya Lugha Uingereza. Nasi, tunaeleza kwamba kuna sababu zaidi ya 700 za kujifunza lugha. Sababu kuu ni pamoja na faida za kibinafsi na starehe ambayo watu hupata kutokana na kujifunza lugha. Watu wengi hujifunza lugha ili kuitumia katika kufanikisha shughuli zao za kimaisha na wengine hujifunza lugha kwa ajili ya kutaka heshima kwani mtu mwenye uwezo wa kuzungumza lugha nyingi huheshimiwa katika jamii. Kutokana na andiko hili, inaonekana kwamba kila mwanafunzi huwa na sababu zake za kujifunza lugha fulani ambazo huweza kuwa ni tofauti na zile za mwenzake. Kwa hiyo, mbinu moja haiwezi kufaa kwa wanafunzi wote. Mwalimu anatarajiwa kuwa na uelewa juu ya mbinu na njia tofauti za ufundishaji wa lugha pamoja na uwezo wa kuchagua mbinu mwafaka kwa kila mwanafunzi kutokana na mahitaji yake ya ujifunzaji wa lugha lengwa. Ndiyo maana utafiti uliofanyika utachangia kwa kuongeza uelewa

juu ya mbinu na njia kadhaa za ufundishaji wa lugha kwa kujihusisha na uchunguzi wa utumizi wa fasihi katika ufundishaji wa lugha.

Jacobs na Farrel (2003) wanaeleza kuwa mbinu za ufundishaji wa lugha katika zama za sasa ni mwendelezo tu wa mbinu ya ufundishaji wa lugha kimawasiliano. Kutokana na andiko la Jacobs na Farrel, inaonekana kwamba wazo la kuendeleza mbinu hii ya ufundishaji wa lugha kimawasiliano lilitokana na sababu ya kwamba watu wengi hujifunza lugha kwa ajili ya kuitumia kwa kufanikisha shughuli zao za maisha ya kila siku. Shughuli hizo zinafanikishwa kwa ajili ya mawasiliano na siyo kuwa na lugha kichwani bila kuizungumza. Kwa hivyo, msingi wa mbinu ya ufundishaji wa lugha kimawasiliano ni uwekaji matendoni lugha ambayo mtu anajifunza. Msingi huu unahusiana moja kwa moja na lengo la mtaala unaoegemea katika uwezo ambao ndio mtaala wa elimu ya kisasa. Hivyo basi, ufundishaji wa lugha katika zama za sasa hauwezi kukwepa misingi ya mtaala unaoegemea katika uwezo ambayo inasisitiza uwasilishaji wa ujuzi katika maisha halisi. Kutokana na wazo la kwamba fasihi ndiyo taaluma inayotumia lugha kwa kutoa picha halisi ya maisha halisi ya mwanadamu, tunaangaziwa kwamba ni bora kuchunguza ufaafu wake katika ufundishaji wa lugha wa zama za sasa kwa upande mmoja na utekelezaji wa mtaala unaoegemea katika uwezo kwa upande mwingine.

**2.5 Utumizi wa Fasihi katika Ufundishaji wa Lugha ya Pili**

Starja (2015: 432) anaeleza kwamba utumizi wa fasihi katika ufundishaji wa lugha ya pili ulikuwepo tangu zamani japo leo unatazamwa kama njia ya kijadi. Anasema:

> Through the review of literature, we can reiterate and properly estimate thetraditional role of literary texts in our teaching process but it is through ourpracticalconsiderations and efforts within the classroom setting, throughdetailed and conspicious patterns of literature that we can feel its immensepowerandresults on ourstudents.

> Kupitia fasihi tunaweza kurudia tena na kukadiria vizuri jukumu la kijadi la maandishi ya kifasihi katika mchakato wetu wa kufundisha lakini ni kupitia maoni yetu ya kivitendo na juhudi katika mazingira ya darasa, kupitia miundo ya fasihi ya kina na ya kushangaza

tunaweza kuhisi nguvu yake kubwa na matokeo kwa wanafunzi wetu [Tafsiri yangu].

Kwa kurejelea andiko hili, katika zama za kale fasihi ilikuwa na nafasi kubwa katika ufundishaji na ujifunzaji wa lugha ya pili lakini kwa bahati mbaya ilipoteza thamani na ladha yake katika ufundishaji wa lugha katika zama za sasa. Kutokana na andiko hili, tunamulikiwa kwamba juhudi za watafiti, wataalamu, wanaisimu, taasisi, mashirika ya kielimu na walimu wa lugha ndio huweza kurudisha thamani ya fasihi katika ufundishaji wa lugha ya pili. Andiko hili linasukuma hoja yetu ya kushughulikia kipengele cha fasihi kama nyenzo ya kufundishia na kujifunzia lugha.

Hapsari (2016) na Rahman (2018) wanaeleza kuwa utumizi wa fasihi katika ufundishaji na ujifunzaji wa lugha ya pili ulipuuzwa kutokana na uendelezaji wa Mbinu ya Ufundishaji wa Lugha Kimawasiliano. Wataalamu hawa wanasema kwamba waamini wa mikabala ya kidhima na kimuundo ya ufundishaji wa lugha wanaituhumu mbinu hii kuwa haina mifano wala miktadha halisi ya kimatumizi ya lugha. Uzuri ni kwamba wataalamu hawa nao hawakubaliani na wazo hili. Kwa maoni yetu, waamini wa mikabala hii walishindwa kuunganisha misingi ya mbinu ya ufundishaji wa lugha kimawasiliano na mihimili ya mikabala ya ufundishaji lugha inayoegemea muundo na dhima ya lugha. Ifahamike kwamba hatupingi wazo la kwamba ufundishaji wa lugha unaoegemea mbinu ya ufundishaji wa lugha kimawasiliano unazingatia utendaji wa kimatumizi wa lugha ya kawaida. Ila pia hatukubaliani na wazo la kwamba lugha ya fasihi haiwezi kutumika katika mawasiliano ya kila siku. Hii ni kwa sababu ujifunzaji wa lugha hauhusu kufanya unukuzi wa moja kwa moja wa mifumo fulani ya lugha. Hivyo basi, kutokana na lugha iliyotumika katika fasihi, mwanafunzi anaweza kujiundia mifumo ya lugha husika katika mawasiliano yake ya kawaida.

Brumfitna Carter (1986) na Lazar (1993) wanakataa wazo la kuwapo kwa lugha maalum ya fasihi. Wanadai kwamba lugha inayotumiwa katika matini za fasihi ni lugha ya kawaida yenye mkusanyiko mkubwa wa sifa za kiisimu kama sitiari, tashibiha na leksimu za kishairi. Naye, Rahman (2018) anathibitisha kuwa usomaji wa fasihi bila shaka, ni shughuli ya kimawasiliano na maandishi ya fasihi ambayo huwa mifano halisi ya matumizi ya lugha. Kwa hivyo, misingi yenyewe ya mbinu ya ufundishaji wa lugha kimawasiliano (ambayo ni pamoja na kutilia maanani katika maingiliano na mawasiliano halisi wakati wa ufundishaji wa lugha) haipuuzi utumizi wa fasihi. Mitazamo na mawazo ya baadhi ya mikabala na walimu wa lugha ndiyo wakati mwingine hupuuza fasihi katika ufundishaji wa lugha.

Grellet (1981), Collie na Slater (1987) na Rahman (2018) wanakubaliana kwamba utumizi wa fasihi kwa kufundishia lugha una manufaa mengi yanayohusiana moja kwa moja na upataji na ukuzaji wa lugha lengwa. Kama nilivyogusia awali, utumizi wa fasihi kama nyenzo ya ufundishaji wa lugha ulipuuzwa kimakosa kwa kufikiri kuwa fasihi haina miktadha ya maingiliano na mawasiliano ya utumizi wa lugha halisi.

Inaonekana kuwa kuna haja ya kuondosha dosari hizo kwa kujiegemeza katika mawazo kadhaa ya watafiti na wataalamu mbalimbali. Rahaman (2018:159) anatetea wazo la kwamba fasihi inahitajika kutumiwa kama nyenzo ya ufundishaji wa lugha. Mtaalamu huyu anaweka msisitizo kwenye miktadha ya fasihi ya kimaingiliano na kimawasiliano halisi; anasema:

> In the first place, the linguistic criterion defends that literature should be used in language teaching, because it provides the learners with genuine, authentic samples of language, and also with real samples of a wide range of styles, text types and registers. It is extremely important for foreign language learners to be trained in a variety of registers, styles and genres and to be able to discern the function of each of them. The second criterion is methodological and refers to the fact that a literary text has multiple interpretations, these generate different opinions among the learners and this leads to real, motivated interaction with the text, with the fellow students and with the teacher.

> Kwanza, kigezo cha kiisimu kinatetea kuwa fasihi inapaswa kutumiwa katika kufundisha lugha, kwa sababu huwapatia wanafunzi sampuli halisi za lugha, sampuli halisi za mitindo anuwai, aina za matini na rejesta. Ni muhimu sana kwa wanafunzi wa lugha ya kigeni kufundishwa katika rejesta, mitindo na tanzu tofauti ili waweze kupambanua dhima ya kimojawapo. Kigezo cha pili, ni cha kimbinu na hurejelea ukweli kwamba matini ya kifasihi huwa na maana nyingi, huzalisha maoni tofauti miongoni mwa wanafunzi na hivyo kusababisha maingiliano baina ya: wanafunzi na matini, wanafunzi kwa wanafunzi au wanafunzi dhidi ya mwalimu kuwa halisi na yenye kumotisha [Tafsiri yetu].

Andiko hili linatusaidia kuepukana na fikira za kwamba fasihi haiwezi kuwa na lugha ya kimawasiliano halisi. Kutokana na andiko hili, tunapaswa kuepukana na mawazo ya kuituhumu mbinu ya ufundishaji wa lugha kimawasiliano kuwa inapuuza utumizi wa fasihi

katika ufundishaji na ujifunzaji wa lugha. Hata hivyo, pengo la andiko hili ni kwamba linaishia kujadili nafasi ya fasihi katika mbinu ya ufundishaji wa lugha kimawasiliano na haligusii nafasi yake katika utekelezaji wa mtaala unaoegemea katika uwezo kama mtaala wa kisasa unaoandamana na mbinu hiyo.

Ipara (2006), Opunde (2012), na Opunde (2015) wanaeleza kuwa mwalimu anaweza kufundisha mada za lugha na sarufi anapofundisha fasihi. Kwa mfano, ufundishaji wa matumizi ya wakati, nafsi, ukanushi, miundo ya sentensi, nakadhalika. Kwa hivyo, kumbe fasihi haijengi miktadha ya kimaingiliano na kimawasiliano tu bali inajenga miktadha ya kufundishia sarufi. Kutokana na andiko hili, tunapata mwelekeo kidogo wa kutumia fasihi kama nyenzo ya ufundishaji wa lugha. Mawazo ya wataalamu wa maandiko ya hapo juu, yanaishia tu kujadili nafasi ya fasihi katika ufundishaji wa lugha ya pili lakini hayazungumzii namna fasihi inavyoweza kutumiwa haswa katika utekelezaji wa mtaala unaoegemea katika uwezo kama mtaala unaozingatia mbinu ya kisasa katika ufundishaji wa lugha ya pili. Hivyo, utafiti huu ulitarajia kuuziba mwanya uliobainishwa huku ukijadili kwa kina namna ambavyo fasihi inaweza kutumiwa pamoja na ufaafu wake katika ufundishaji na ujifunzaji wa lugha ya pili kwa upande mmoja na utekelezaji wa mtaala unaoegemea katika uwezo kwa upande mwingine.

## 2.6 Mtaala Unaoegemea katika Uwezo

Nodine (2015) anafafanua kuwa mtaala unaoegemea katika uwezo uliibuka na kutumiwa huko Marekani mnamo miaka ya 1960 ukijulikana kwa jina la elimu inayoegemea katika uwezo**.** Mtaalamu huyu anawataja wataalamu wengine waliowahi kugusia na kujadili mtaala huu kabla ya miaka ya 1960. Wataalamu wanaotajwa ni pamoja na Ralph (1940) na Bloom (1956). Malan (2000) anaeleza kwamba mtaala unaoegemea katika uwezo, umehusishwa na juhudi za muda mrefu za kutambua na kufikia matokeo ya wanafunzi katika ufundishaji na ujifunzaji. Mtaalamu huyu alitumia neno “matokeo” kwa kumaanisha “uwezo” ambao unahusu ujuzi unaooneshwa na kuwasilishwa na mwanafunzi wakati na baada ya ujifunzaji wake. Kutokana na andiko hili, tunaona kwamba utumizi wa mtaala unaoegemea katika uwezo si mbinu mpya inayolenga kupuuza heshima na thamani ya mwalimu katika mchakato wa ufundishaji na ujifunzaji kama baadhi ya walimu wanavyofikiria. Utumizi wa mtaala huu unalenga kumshirikisha mwanafunzi kwa kina katika ujifunzaji ili kukuza uwezo wake kwa kutumia maarifa na ujuzi alio nao. Hivyo basi, kwa muktadha wa ufundishaji wa lugha ya pili, kazi ya mwalimu ni kumpatia mwanafunzi mifano ya mifumo tofauti ya lugha lengwa na

kumwongoza kuitumia kwa kufanikisha shughuli na mahitaji yake ya kimawasiliano katika maisha yake ya kila siku.

Nzima (2016) anaeleza kuwa mtaala unaoegemea katika uwezo unaweza kudhaniwa kama aina ya mtaala unaolenga kuwezesha wanafunzi kukuza, kuunganisha na kutumia uwezo unaohitajika, kama vile utatuzi wa matatizo, tafakuri tunduizi, ubunifu, teknolojia ya habari, ushirikiano na ujifunzaji usio na mpaka. Aina hii ya mtaala inasisitiza uwezo ambao wahitimu wanaweza kutumia katika shughuli tofauti za kazi na maisha katika jamii zao badala ya kulenga tu kupata na kuzaa maarifa. Unalenga kuwaweka wanafunzi katika hali halisi ambayo wanapaswa kuonyesha ikiwa wanaweza kutatua matatizo fulani au kufanya shughuli fulani na jinsi wanavyoweza kuzifanya. Mawazo ya Nzima (khj) yanashabihiana na ya UNESCO (2017) katika Kabombwena Mulenga (2019). Kwao, mtaala unaoegemea katika uwezo ni mtaala ambao unasisitiza kile wanafunzi wanachotarajiwa kufanya badala ya kuzingatia zaidi kile wanachotarajiwa kujua. Kutokana na wataalamu hawa, tunaweza kusema kuwa kutokana na mtaala unaoegemea katika uwezo, nguvu zinawekwa katika matendo ya ujuzi na maarifa ya mwanafunzi kutokana na kile alichojifunza kuliko kushangilia ujuzi na maarifa aliyo nayo.

Kitta na Tilya (2010) wanaeleza kuwa ufundishaji unaotegemea uwezo wa mwanafunzi hujihusisha na mazingira ambayo huzingatia sana maarifa, ujuzi, mitazamo, na imani ambazo wanafunzi huleta katika mchakato wa ufundishaji na ujifunzaji. Kutokana na mawazo ya mtaalamu huyu, inaeleweka zaidi kuwa katika mbinu inayoegemea uwezo, mwanafunzi ndiye kitovu cha maarifa na siyo mwalimu. Hivyo basi, ili kukaribisha mchango wa wanafunzi kama wahusika wakuu katika ufundishaji na ujifunzaji, ni lazima kuwajengea miktadha ya kujisikia watu wenye thamani ili waweze kuchangia zaidi.

Kutokana na andiko la Kitta na Tlya (whj) tunaweza kusema kwamba, sababu ya wanafunzi kupewa nafasi na fursa ya kushiriki katika ufundishaji na ujifunzaji kwa kina, ni kulenga kujenga miktadha ya kuwaruhusu kuonesha tofauti na uwezo wao. Uwezo wa mwanafunzi wa kukabiliana na tofauti za watu wengine ndiyo Kitta na Tlya (whj) wanaona kama msingi wa utekelezaji wa mbinu inayoegemea uwezo. Hivyo basi, mwanafunzi hatarajiwi kujiamini kwamba anajua mengi au amepata mengi kutokana na elimu fulani bali anatarajiwa kijivunia kuonesha hayo anayoyajua katika kuleta mchango wa kimaendeleo kwake binafsi, kwa jamii yake, kwa nchi hadi kwa dunia yote. Kwa hivyo, uwezo wa lugha kwa mwanafunzi hauonekani wakati wa ufundishaji na ujifunzaji wa darasani na utendaji wake haufanyiwi darasani. Hivyo basi, mwalimu anahitajika kufundisha lugha kwa kujenga fursa na mazingira

yanayomhamasisha mwanafunzi kuzoea kujijengea mifumo tofauti ya lugha lengwa na kuitumia katika maisha ya nje.

Nodine (2015) anafafanua kuwa taasisi za elimu zinazotumia mbinu inayoegemea katika uwezo zinakabiliwa na changamoto mbili zaidi ambazo ni kuamua maana ya neno "uwezo" katika kila eneo la somo na kutambua njia za wanafunzi za kuonesha uwezo huo. Chu na wenzake (2020) wanatoa mchango katika ufafanuzi wa uwezo kwa kusema kuwa uwezo ni seti ya ujuzi, maarifa na tabia ambazo mtu anahitaji kuwa nazo ili kufanya majukumu mbalimbali, kazi au shughuli katika ulimwengu wa kazi. Mawazo ya wataalamu hawa yanaelekeza kueleza kwamba uwezo ni jumla ya nguvu za kiakili zinazomsaidia mtu kutatua na kupata suluhu za matatizo ya kimaisha katika maeneo tofauti. Hivyo basi, kila somo linajumuisha uwezo wa kuendelezwa kwa wanafunzi. Tumechagua kutumia neno "kuendelezwa" kwa sababu mwanafunzi anakuja kujifunza akiwa na kiwango fulani cha uwezo unaotarajiwa (Chomsky, 1957 katika Aljoundi, 2014). Kutokana na mawazo ya wataalamu hawa, tunaangaziwa kuhusu mambo mawili. Mosi, tunaona kwamba mara nyingi, utendaji wa uwezo unapatikana nje ya darasa yaani katika jamii na familia. Hivyo basi, mwanafunzi anaanza somo fulani akiwa na kiasi fulani cha uwezo unaotarajiwa kuendelezwa kutokana na somo hilo. Pili, lengo kuu la ufundishaji na ujifunzaji unaoegemea katika uwezo hauhusu kumwezesha mwanafunzi kupata alama nyingi darasani. Uwezo huu unalenga kumwezesha kuhamisha ujuzi na maarifa aliyojifunza darasani kwa kuyaweka katika muktadha wa kimaisha ili kuyatumia katika upataji wa suluhu za matatizo ya kimaisha.

Bloom (1968) katika Nodine (2015) anaona kuwa changamoto kuu ya ujifunzaji wa uwezo ni pamoja na "kutambua jinsi tofauti za wanafunzi zinavyoweza kuhusishwa na mchakato wa ufundishaji na ujifunzaji. Kutokana na kipaumbele kilichowekwa katika ufundishaji unaosisitiza onyesho la ujuzi wa mwanafunzi na maarifa yake, ufundishaji na ujifunzaji pia huendana na mahitaji ya mwanafunzi pamoja na kile anachotaka kujifunza zaidi. Hivyo basi, mwalimu asiamue kile kinachotarajiwa kuwa matokeo ya ufundishaji na ujifunzaji kwani hakuna mpaka wala kanuni zinazoeleza kile anachotarajiwa kuonesha mwanafunzi. Mawazo ya Bloom yana mashiko japo changamoto anayoibainisha ni lazima ijitokeze. Hii ni kutokana na ukweli kwamba wanafunzi ni tofauti; uwezo wao wa kiakili, mbinu zao za kujifunza, usuli wao wa kijamii na kielimu unatofautiana. Tunaona kwamba suluhu ya tatizo hili linahusu ushirikiano mkubwa wa washiriki wote wa elimu ili kila mwanafunzi aweze kufuatiliwa na kusikilizwa. Suluhu yenyewe inahusu kujenga madarasa mengi ili kupunguza idadi kubwa ya

wanafunzi katika darasa moja kwa mwalimu mmoja, kuajiri walimu wanaofaa kiujuzi na kiidadi, mafunzo kwa walimu na vifaa vinavyoegemea uwezo na vinavyotosha, juhudi za wanafunzi na za wazazi, nakadhalika.

Kutokana mawazo yaliyomo katika maandiko yanayohusu mtaala unaoegemea katika uwezo, tunaweza kusema kwamba mtaala huu unalenga kujenga ustadi wa wanafunzi kwa kusisitiza utendaji wa maarifa badala ya kujua tu mambo kichwani bila matumizi yake. Unasisitiza mwanafunzi kuhusisha kile anachojifunza darasani na hali halisi ya maisha anayoyaishi au anayoyafikia. Nia yake kubwa ni kumuandaa mwanafunzi kuwa wa vitendo, ubunifu na kutumia ubongo wake katika kutatua shida tofauti na sio kuutumia kubana kile alichoambiwa au kujifunza. Maandiko haya ni ya muhimu sana kwa sababu yanatuangazia kufanya utafiti kuhusu utekelezaji wa mtaala unaoegemea katika uwezo. Mwangaza huo, unatokana na pengo lililopo la kwamba maandiko haya yanaishia tu kutoa maelezo juu ya mtaala unaoegemea katika uwezo na utekelezaji wake bila kueleza nafasi ya fasihi katika utekelezaji wa mtaala huu. Kwa hivyo, utafiti huu ulilenga kuziba pengo hili kwa kuchunguza ufaafu wa fasihi na namna inavyoweza kutumiwa katika utekelezaji wa mtaala unaoegemea katika uwezo.

## 2.7 Nafasi ya Fasihi katika Ukuzaji wa Uwezo wa Mwanafunzi

McRae (1991), Daskalovskana Dimova (2012) wanakubaliana kuwa ujuzi uliopatikana wakati wa kusoma maandishi ya fasihi utasaidia wanafunzi kuwa watu bora wenye uwezo wa kutathmini ulimwengu wanaouishi na kuhimiza ujifunzaji wenye mabadiliko ambao unawahusisha wanafunzi kujifunza kwa kuchangia na kuonyesha ubinafsi iwezekanavyo. Mawazo ya wataalamu hawa yanahusiana na ukuzaji wa baadhi ya uwezo wa jumla unaotarajiwa kuendelezwa katika mtaala unaoegemea uwezo kama vile; kukuza uwezo wa tafakuri tunduizi, ubunifu na ugunduzi, utafiti na utatuzi wa matatizo, mawasiliano katika lugha rasmi, ushirikiano, utawala binafsi na stadi za maisha na ujifunzaji usio na mpaka. Tatizo lililopo katika maandiko ya Mc Rae (Khj) na Daskalovskana Dimova (Khj) ni kwamba hawaoneshi kwa vitendo ni namna gani fasihi inaweza kukuza stadi hizi wanazobainisha miongoni mwa wanafunzi.

Kabombwena Mulenga (2019) wanaeleza kwamba utumizi wa michezo ya kuigiza ni njia bora ya kufundishia historia ya taifa ili kufundisha wanafunzi utaifa na uzalendo. Mawazo yao yanashahibiana na yale ya Lazar (1993) katika Hapsari (2011). Kwa mtazamo wake, kuweka mbali fasihi katika ufundishaji wa lugha ni kupunguza nafasi ya "kumwelimisha mtu kwa

ukamilifu." Ni kazi za fasihi ambazo zinatoa fursa ya kumshirikisha mtu katika kupata uzoefu fulani wa kihisia, kuhoji maadili fulani, na kumhimiza kutoa wazo juu ya utamaduni uliodhihirika katika kazi hizo. Kwa kiasi fulani, andiko hili linagusia kidogo umuhimu wa fasihi katika kufanikisha baadhi ya malengo ya mtaala unaoegemea katika uwezo. Hata hivyo, andiko hili nalo bado halielezi kiwango ambacho fasihi inaweza kufaa katika utekelezaji wa mtaala unaoegemea uwezo. Kutokana na mawazo ya wataalamu hawa, tunaona kuwa yanahusiana na lengo kuu la mtaala unaoegemea katika uwezo nchini Rwanda. Kama tulivyoona, lengo kuu la mtaala huu ni pamoja na kuwapa wahitimu wa shule uwezo wa kukabiliana na mahitaji yanayohusiana na kazi kwa kuwawezesha kuwa washindani wazuri wa kazi katika soko la ajira la kiulimwengu na kujenga raia ambaye anafaa kwa jamii na nchi yake (REB na MINEDUC, 2015; Nsengimana, 2021).

Kutokana na maandiko yote yaliyopitiwa kuhusu nafasi ya fasihi katika ukuzaji wa uwezo wa mwanafunzi, tunaweza kusema kwamba yote ni muhimu kwa sababu yanatuangazia kuhusu pengo la kuzibwa na utafiti wetu. Pengo hilo linatokana na kwamba maandiko husika hayaelezi ufaafu wa fasihi katika utekelezaji wa mtaala unaoegemea uwezo. Kwa hivyo, utafiti huu ulitarajia kuziba mwanya huu kwa kuchunguza na kueleza namna fasihi inavyoweza kutumiwa na kiwango inachoweza kufaa katika utekelezaji wa mtaala unaoegemea katika uwezo hususan kwa mazingira ya Rwanda.

## 2.8 Mapengo Yanayojitokeza Kutokana na Mapitio ya Maandiko

Katika maisha ya kawaida, mtu akiwa na mtazamo fulani wenye faida kwa umati wa watu, anaueleza kinagaubaga kwa kuwashawishi wahusika wake ili waweze kumuunga mkono katika utekelezaji wa mtazamo huo muhimu. Baadhi ya maandiko yaliyopitiwa yanaishia tu kujadili nafasi ya fasihi katika ufundishaji wa lugha, mengine yanaishia tu kujadili nafasi ya fasihi katika ukuzaji wa uwezo wa mwanafunzi. Hata hivyo, pengo la kwanza ni kwamba hayaelezi kiwango ambacho fasihi inaweza kufaa katika ufundishaji wa lugha ya pili. Pengo la pili, hayaelezi nafasi ya fasihi katika utekelezaji wa mtaala unaoegemea katika uwezo. Pengo la tatu, hayaelezi namna fasihi inavyoweza kutumiwa katika ufundishaji wa lugha kwa upande mmoja na utekelezaji wa mtaala unaoegemea katika uwezo kwa upande mwingine. Utafiti uliofanyika ulilenga kuziba mapengo yaliyobainishwa hapo juu kwa kutathmini namna fasihi inavyoweza kutumiwa na kuchunguza ufaafu wake katika ufundishaji wa lugha na utekelezaji wa mtaala unaoegemea katika uwezo haswa kwa kuihusisha na ufundishaji wa Kiswahili katika mazingira ya Rwanda.

### 2.9 Kiunzi cha Nadharia za Utafiti

Katika kueleza kipengele hiki ni bora kwanza kufafanua dhana ya nadharia kwa kuegemea katika mitazamo ya wataalamu kadhaa na kisha kueleza maana ya kiunzi cha nadharia kama kipengele kimojawapo cha vipengele vilivyoongoza utafiti wetu.

Ponera (2019) anafafanua nadharia katika dhana tatu. Mosi, nadharia huweza kumaanisha seti ya kanuni na maelezo kuhusu jambo fulani. Pili, huweza kuchukuliwa kama lenzi au dira ya kuendeshea tafiti, tahakiki, na/au mijadala kuhusu mada mbalimbali. Tatu, nadharia huweza kutazamwa kama nyenzo ya kufikia mahitimisho ya kimjadala kuhusu dhana mbalimbali za sayansi za jamii. Katika taaluma za Sayansi za Jamii na Insia, nadharia hutumika kwa kueleza 'vipi'na 'kwa nini' mambo hutokea kwa jinsi yatokeavyo (Johnson na Christense, 2008, Ponera, 2016 katika Ponera, 2019).

Ponera (Khj) anaeleza kiunzi cha nadharia kama ruwaza (namna na mawanda) maalumu ya utumiwaji wa nadharia katika kuendesha jambo fulani. Hivyo, kiunzi cha nadharia humsaidia mtafiti au mhakiki kuliunda na kuendesha duara zima la kazi yake (Ponera, 2019). Utafiti uliofanyika uliongozwa na nadharia mbili ambazo ni Nadharia ya Utambuzi na Nadharia ya Mwingiliano-jamii. Uteuzi wa nadharia hizi umetokana na ukweli kwamba, misingi yake inahusiana na malengo ya utafiti huu. Hivyo, hatua za utafiti kama vile uundaji wa malengo, mbinu za utafiti, ukusanyaji wa data, uchambuzi na uwasilishaji wake uliongozwa na nadharia hizi mbili.

#### 2.9.1 Nadharia ya Utambuzi

Nadharia ya utambuzi iliasisiwa na Noam Chomsky mnamo 1959. Saikolojia ya utambuzi inajishughulisha na namna watu wanavyopokea habari, kuzielewa, kuzitathmini na kuzihakiki (Costley na Nelson 2013). Kutokana na Nadharia ya Utambuzi, mtazamo juu ya habari unaathiriwa na hisia pamoja na asili ya kijamii na kiutamaduni. Utambuzi unahusu uelewa juu ya habari na utambuzi wa michakato ya kiakili kwa kusisitiza upekee pamoja na utofauti wa watu katika fikra, uamzi na utoaji wa mawazo. Tunapohakiki msingi wa hapo juu, tunaangaziwa kwamba unajihusisha na ukuzaji wa tafakuri tunduizi. Uwezo huu wa tafakuri tunduizi ni muhimu sana katika ujifunzaji wa lugha ya pili na utekelezaji wa mtaala unaoegemea katika uwezo.

Wanasaikolojia wa utambuzi wanaamini kuwa akili ni kichakato cha habari. Watu wanapokea habari kupitia hisi za mwili, wanajaribu kuelewa habari hizo pamoja na uhusiano wake, ndipo kisha wanazisambaza kwa wengine (Fulcher, 2003). Kutokana na wazo hili, ni bora kumpa mwanafunzi fursa ya kufikiria, kuelewa na kuhakiki habari anazozipokea kutoka kwa mwalimu, wanarika au watu wengine ili aweze kuzitolea maoni akiwa huru. Msingi huu unahusiana na mojawapo ya misingi ya ufundishaji unaoegemea uwezo ambayo inasisitiza wazo la kwamba ukosoaji wa makosa ya wanafunzi wa lugha ni mchakato. Ni bora mwalimu ajenge fursa ambazo zinalenga kumwezesha mwanafunzi kujikosoa mwenyenye.

Nadharia ya Utambuzi haipingani na umuhimu wa mazingira katika ujifunzaji, wala haipingani na wazo la kwamba mtu huzaliwa na uwezo wa kujifunza lugha. Kwa mujibu wa wanautambuzi, mchakato wa kujifunza lugha na uchakataji wa data kichwani sio jambo la kubahatisha kwani wanadamu wana uhulka wa lugha kutokana na kifaa cha upataji wa lugha wanachozaliwa nacho. Wazo hili linaelezea kwamba mwalimu hapaswi kuwachukulia wanafunzi kama watu wasioweza kuwa na mchango mkubwa katika ufundishaji na ujifunzaji. Mwalimu anatarajiwa kujishughulisha na kuwashirikisha wanafunzi kwa kiasi kikubwa kama wahusika muhimu katika ujifunzaji. Msingi huu unahusiana sana na ujifunzaji wa lugha unaoegemea katika uwezo. Hii ni kutokana na ukweli kwamba tunapoheshimu wanafunzi na kuwashirikisha kwa kiwango cha juu katika ufundishaji bila shaka tutakuwa katika njia za utekelezaji wa mtaala unaoegemea katika uwezo. Hivyo basi, nadharia hii ilitusaidia kuendeleza utafiti wetu kwani msingi wake wa hapo juu unahusiana na ufundishaji wa lugha pamoja na utekelezaji wa mtaala unaoegemea katika uwezo.

Nadharia ya Utambuzi inahusiana sana na utafiti wetu kutokana na misingi yake ya ukuzaji wa tafakuri tunduizi katika ujifunzaji wa lugha, kumruhusu mwanafunzi kufikiria na kutumia lugha yake. Nadharia hii inazingatia nafasi ya mwanafunzi katika utoaji wa maoni na mawazo katika ufundishaji na ujifunzaji pamoja na kuthamini mchango wa maingiliano ya mazingira katika ujifunzaji. Hivyo basi, utumizi wa Nadharia ya Utambuzi, ni muhimu sana katika mchakato wa utafiti wetu kwa sababu unalenga ufundishaji wa lugha ya pili na utekelezaji wa mtaala unaoegemea katika uwezo. Mawazo ya Nadharia ya Utambuzi yanaweka msisitizo juu ya upekee wa mwanafunzi na ushirikiano wake na wa nje katika ujifunzaji wa lugha ya pili. Msisitizo huu juu ya nafasi ya mtu binafsi pamoja na watu wa nje, unalenga kukuza uwezo wa tafakuri tunduizi, utatuzi wa matatizo, ushirikiano na ujifunzaji usio na mpaka, utafiti na

ubunifu. Kwa hivyo, tunaweza kuitumia katika hatua za utafiti huu kama vile; uundaji wa malengo, mbinu za utafiti, ukusanyaji wa data, uchambuzi na uwasilishaji wa data.

Kulingana na utafiti uliofanyika wenye mada ya "kuchunguza nafasi ya fasihi katika ufundishaji wa lugha ya pili na utekelezaji wa mtaala unaoegemea katika uwezo," tunaona kwamba Nadharia ya Utambuzi pekee yake isingeweza kukamilishaa utafiti kwa ukamilifu. Hii inatokana na ukweli kwamba nadharia hii inatazama sana upande wa mtu binafsi, zaidi ya maingiliano ya kimazingira katika mchakato wa ujifunzaji lugha. Hali hii inasababisha kushughulikia sana kipengele cha ufundishaji wa lugha zaidi ya utekelezaji wa mtaala unaoegemea katika uwezo. Hivyo basi, ilionekanani bora kuongeza nadharia itakayoikamilisha Nadharia ya Utambuzi kwa kuegemea katika misingi ya utekelezaji wa mtaala unaoegemea uwezo kama vile; ushirikiano, utendaji, uwasilianaji, uraia nakadhalika.

### 2.9.2 Nadharia ya Maingiliano ya Tamaduni-jamii

Nadharia ya Maingiliano-jamii iliasisiwa na Lev Vygotsky mnamo 1920 na 1930. Nadharia ya Vygotsky ilikuwa inazingatia sana tafakuri tunduizi, mawazo ya kibusara, utatuzi wa matatizo, upangaji, utengenezaji wa maana, nakadhalika (Fahim na Haghani, 2012). Nadharia ya Maingiliano-jamii inaamini kuwa utambuzi binafsi wa mwanadamu unakuzwa kupitia ushirikiano wa kijamii na shughuli za kitamaduni na watu wengine, vitu, na matukio au visa mbalimbali (Bruce, & Hughes, 2011). Kutokana na misingi hii ya Nadharia ya Maingiliano ya Tamaduni-jamii tunaangaziwa kwamba inasisitiza ukuzaji wa uwezo binafsi wa mwanafunzi pamoja na utendaji wake katika maisha halisi ambayo ndiyo malengo ya mtaala unaoegemea katika uwezo.

Mitazamo ya Nadharia ya Kimaingiliano-jamii inatofautiana kimsingi na mitazamo mingine juu ya upataji wa lugha ya pili. Hii ni kutokana na ufahamu wake kwamba mazingira ya kijamii sio somo, lakini ni chanzo cha ukuaji wa akili (Swain na Deters, 2007). Wakati huohuo, mitazamo mingine huzingatia mtu binafsi na kile anachokifanya. Wazo hili linasisitiza umuhimu wa jamii kama uwanja wa utendaji. Hapa tunaangaziwa kwamba msingi huu unahusiana na ule wa mtaala unaoegemea katika uwezo wa kwamba masomo yaliyofundishwa darasani yanapaswa kuhusianishwa na kutendwa katika maisha halisi yaani katika jamii kama uwanja wa utendaji. Kutokana na mawazo haya, ni bora mwalimu wa lugha darasani ajenge fursa kwa wanafunzi za kutenda lugha waliyojifunza darasani.

Misingi ya mtaala unaoegemea katika uwezo pamoja na misingi ya Nadharia ya Maingiliano-jamii yote husisitiza utendaji wa lugha katika maisha halisi ya kijamii siyo ya darasani. Hivyo basi, misingi hii ilitusaidia kuendeleza utafiti kutokana na wazo la kwamba fasihi huweza kujenga fursa ya utendaji wa lugha katika jamii. Hii ni kutokana na ukweli kwamba fasihi hujishughulisha na jamii ya binadamu pamoja na shughuli zake za kimaisha, yaani hutoa picha halisi ya maisha ya mwanadamu (Ntarangwi, 2004 na Wamitila, 2004).

Nadharia ya Maingiliano-jamii inazingatia maingiliano tofauti yanayoweza kujitokeza kati ya mtu anayejifunza lugha na nyenzo za ujifunzaji kwa njia ya upatanishi na muktadha wa kijamii (Lantolf & Thorne, 2007 katika Mustafa na wenzake, 2017). Kwa maneno mengine, nadharia hii inashughulikia suala la zana ambazo mtu anatumia kujifunza na wapi ujifunzaji hufanyika, na kwanini mtu huyo anajifunza. Misingi hii ilitusaidia kuendeleza utafiti wetu hasahasa katika ukusanyaji wa data ambapo mara nyingi tulikuwa tunatafuta data kutoka katika jamii kama zana na mahali pa ujifunzaji na upataji wa lugha. Pia, utafiti uliofanyika ulijishughulisha na data zinazojihusisha na swali la kwa nini mtu hujifunza lugha ambapo tutapata data zinazohusiana na dhima ya lugha zikiwemo mawasiliano na ufanikishaji wa shughuli za kimaisha. Hivyo basi, hatuna shaka kwamba misingi ya Nadharia ya Maingiliano ya Tamaduni-jamii ya hapo juu ilitoa msaada mkubwa katika uendelezaji na ufanikishaji wa utafiti wetu.

Utafiti wetu ulihusika na mambo mawili muhimu. Mambo hayo ni pamoja na ufundishaji wa lugha na utekelezaji wa mtaala unaoegemea katika uwezo. Hatukupendelea kujihusisha na sehemu moja zaidi ya sehemu nyingine japo tulipenda sehemu zote zishughulikiwe kwa usawa. Hivyo basi, Nadharia ya Maingiliano-jamii, nayo ina upungufu wa kujiegemeza zaidi katika athari za kimazingira katika ujifunzaji wa lugha ya pili. Msingi huu unaohusu athari na nguvu za nje katika ujifunzaji wa lugha, unasisitiza utekelezaji wa mtaala unaoegemea katika uwezo zaidi ya ukuzaji wa tafakuri tunduizi, ubunifu na utatuzi wa matatizo kwa mtu binafsi. Ndiyo maana katika utafiti huu, Nadharia ya Utambuzi ilitusaidia kujishughulisha na nguvu za upekee wa mtu binafsi katika ujifunzaji. Nayo, Nadharia ya Maingiliano-jamii ilichangia kwa kusisitiza nguvu za nje katika mchakato huu wa ujifunzaji.

### 2.9.3 Jinsi Nadharia ya Utambuzi na Maingiliano ya Tamaduni-jamii Zilivyotumika

Misingi yote ya nadharia hizi ni muhimu kwa utafiti uliofanyika lakini kila nadharia inajengeka kwa msingi wa mawazo mapana. Hivyo basi, utafiti huu ulitumia misingi miwili tu

ya nadharia hizi katika mchakato wake wa ukusanyaji wa data, uchanganuzi wa data na katika uendeshaji wa mjadala wa utafiti. Mosi, ni misingi inayohusiana na upekee wa mtu na kuheshimu utofauti wa watu katika mchakato wa ufundishaji na ujifunzaji kwa ujumla. Pili, ni misingi inayohusiana na umuhimu wa mazingira na jamii katika ukuzaji wa uwezo wake. Hii siyo kwa suala la ufundishaji na ujifunzaji wa lugha tu, bali na hata katika shughuli za maisha ya kawaida ya watu. Tulichagua misingi hii, kutokana na ukweli kwamba inaandamana na misingi pamoja na malengo ya ufundishaji wa lugha kwa upande mmoja na utekelezaji wa mtaala unaoegemea katika uwezo kwa upande mwingine. Uzuri zaidi wa misingi iliyochaguliwa ni kwamba inalenga kugusia nafasi ya fasihi kama nyenzo ya kueleza jamii na binadamu. Hii ni kutokana na ukweli kwamba wakati tunapojishughulisha na suala la ufundishaji na ujifunzaji wa lugha kwa kuegemea mtaala unaoegemea katika uwezo, hatuwezi kuweka kando fasihi. Hivyo basi, misingi ya Nadharia ya Utambuzi na Maingiliano ya Utamaduni-jamii inakamilishana kwa kufanikisha utafiti wetu. Misingi ya Nadharia ya Utambuzi husisitiza upekee na mchango wa binafsi wa mwanafunzi katika ujifunzaji. Misingi ya Nadharia ya Maingiliano ya Tamaduni-jamii nayo inasisitiza mchango wa mazingira na jamii katika ujifunzaji wa mwanafunzi. Hivyo basi, misingi ya nadharia mbili inahusu kuheshimu upekee na kukuza uwezo wa mwanafunzi usio tu kwa kiwango cha darasa lakini pia kwa kiwango cha kijamii na ulimwengu halisi.

## 2.10 Muhtasari wa Sura ya Pili

Sura ya pili imeeleza kuhusu maandiko kuhusiana na mada ya utafiti pamoja na mapengo yaliyojitokeza katika maandiko yaliyopitiwa. Pia, tulijadili kiunzi cha Nadharia ya Utambuzi na Nadharia ya Maingiliano ya utamaduni-jamii na kueleza jinsi zilivyotumika katika utafiti huu. Sura inayofuata inaelezea methodolojia ya utafiti.

## SURA YA TATU: METHODOLOJIA YA UTAFITI

### 3.1 Utangulizi

Sura hii inafafanua methodolojia iliyotumika katika mchakato mzima wa utafiti haswa katika ukusanyaji, uchanganuzi, na uwasilishaji wa matokeo ya utafiti. Vipengele vilivyofafanuliwa katika sura hii ni pamoja na usanifu wa utafiti, eneo la utafiti, wango na sampuli ya utafiti, ukusanyaji wa data, uchanganuzi na uwasilishaji wa data, masuala ya kuthibiti ubora wa utafiti, itikeli ya utafiti, mpangilio wa ripoti ya utafiti, na hitimisho.

### 3.2 Usanifu wa Utafiti

Usanifu wa utafiti ni kipengele muhimu kwa sababu kinahusu kueleza mpango-kazi wa utafiti mzima kwa kutoa picha ya shughuli za utafiti wote. Cresswel (2007) katika Ponera (2019) anafafanua kuwa usanifu wa utafiti ni kipengele kinachohusika na upangaji wa mazingira ya ukusanyaji na uchunguzi wa data kwa namna inayolenga kuhusisha uhalisi wa malengo ya utafiti na uwezo wa kumudu mchakato wa utafiti. Hivyo basi, kwanza utafiti wetu ulikusanya data za kitaamuli kwa kuongozwa na paradima ya ujengaji. Honebein (1996) kama anavyonukuliwa na Adom na wenzake (2016) anaeleza dhana ya kifalsafa ya ujengaji kama mkabala ambao unadai kwamba watu hujenga ufahamu wao wenyewe na maarifa ya ulimwengu kupitia mambo ambayo wameyazoea na hutafakari kuhusu uzoefu huo.

Hivyo basi, kwa kuongozwa na falsafa hii, utafiti ulichunguza jinsi fasihi inavyoweza kuwa mojawapo ya mazoea ya wanafunzi katika ujifunzaji wao wa lugha na ukuzaji wa uwezo walionao awali. Aidha, utafiti ulijihusisha na ukusanyaji wa data za kitaamuli, kutokana na ukweli kwamba watafitiwa walikuwa na uhuru wa kusema chochote kile kuhusiana na maswali watakayoulizwa kuhusu utafiti. Kingine ni kwamba mtafiti alikuwa kwenye uwanja wa taarifa ambapo alikusanya data zinazotoka kwa watafitiwa moja kwa moja. Aidha, mtafiti alijishugulisha na ukusanyaji wa data zinazohusu nafasi ya fasihi katika ujifunzaji wa lugha ya pili na utekelezaji wa mtaala unaoegemea katika uwezo kupitia ufundishaji na ujifunzaji wa Kiswahili katika shule za upili wilayani Rusizi nchini Rwanda.

### 3.3 Eneo la Utafiti

Kipengele hiki cha methodolojia ya utafiti kinahusu mwelekeo wa kijiografia na wa kitaaluma kulingana na asili ya mada yenyewe (Ponera, Khj). Tunaweza kusema kwamba kipengele hiki

kinahusu kujibu maswali kama vile: "Ni wapi utafiti ulifanyika?" na ni maeneo gani ya kitaaluma yaliyoshughulikiwa?" Eneo la kijiografia katika utafiti wetu lilikuwa ni shule za sekondari zinazofundisha fasihi ya Kiswahili wilayani Rusizi nchini Rwanda. Shule za sekondari zilichaguliwa kutokana na sababu ya kwamba ndicho ngazi ambayo hushughilikia ujifunzaji wa lugha ya Kiswahili. Lakini kitu cha muhimu zaidi ni kwamba shule za sekondari hushughulikia tanzu zote mbili za fasihi yaani fasihi simulizi na fasihi andishi katika Kiswahili.

Wilaya ya Rusizi nayo ilichaguliwa kutokana na eneo lake la kijiografia ambapo hugusia mipaka ya nchi mbili (Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo na Burundi). Kwa hivyo, ni dhahiri kwamba huwa na athari tofauti za ujifunzaji wa lugha ya Kiswahili kwa wanafunzi wa wilaya hii. Eneo la kitaaluma ni baadhi ya kazi za fasihi andishi na fasihi simulizi zinazopatikana katika vitabu vya Kiswahili kwa wanafunzi wa kidato cha tano nchini Rwanda.

### 3.4 Wango na Sampuli ya Utafiti

Kwa mujibu wa Ponera (Khj) wango la utafiti ni jamii pana inayotafitiwa, wakati sampuli ni sehemu teule ya jamii hiyo pana.

#### 3.4.1 Wango la Utafiti

Neno "wango" linafafanuliwa kuwa namna ya kuhesabu; au idadi ya vitu au watu (*Kamusi ya Kiswahili Sanifu* iliyoandikwa na TUKI (2004). Kwa hivyo, wango la watu katika utafiti wetu lilikuwa ni walimu na wanafunzi wa shule zinazofundisha fasihi ya Kiswahili wilayani Rusizi. Wango la vitu ni kazi za fasihi simulizi na andishi zinazopatikana katika kitabu cha Kiswahili kwa mwanafunzi wa kidato cha tano mchepuo wa Kiswahili nchini Rwanda.

#### 3.4.2 Sampuli na Usampulishaji wa Utafiti

Ponera (2019) akiwanukuuu Kothari (2009) na Dawson (2002) anaifafanuwa sampuli kama sehemu ya wango inayoteuliwa ili itumike katika kusaka majibu ya tatizo. Usampulishaji nao ni kitendo cha kuteua sampuli ambayo itawakilisha watafitiwa wote wanaolengwa katika utafiti unaotarajiwa kufanyika (Cresswell, 2000). Hivyo, sampuli katika utafiti ilipatikana kwa kutumia usampulishaji sinasibu, hususani usampulishaji lengwa. Kwa kutumia mbinu hii, sampuli katika utafiti wetu ilikuwa walimu wanne wanaofundisha fasihi ya Kiswahili katika kidato cha tano pamoja na wanafunzi arobaini wanaojifunza fasihi ya Kiswahili katika kidato

cha tano kutoka shule nne zenye michepuo ya Kiswahili. Idadi ya arobaini ya wanafunzi ilichaguliwa kutokana na hoja ya kwamba shule nyingi hazizidishi idadi hii ya wanafunzi katika darasa zao za kidato cha tano. Kwa hivyo, tuliangaaziwa kwamba ndiyo idadi ambayo huweza kutupa taarifa za kutosha kwa kufanikisha utafiti wetu.

Sampuli ya kazi zilizoteuliwa ni hadithi fupi simulizi 4, hadithi fupi andishi 2, wimbo mmoja, shairi moja na kazi nyingine mbalimbali za fasihi kama vile vitendawili, methali nahau na misemo. Kazi zilizoteuliwa zote zinapatikana katika kitabu cha Kiswahili kwa mwanafunzi wa kidato cha tano mchepuo wa Kiswahili. Walimu na wanafunzi wa Kiswahili katika kidato cha tano walitafitiwa kwa kuwa ndio wanaojishughulisha na tanzu mbili za fasihi (fasihi simulizi na fasihi andishi) katika masomo yao. Hivyo basi, hawa ndio walikuwa na uwezo wa kufafanua kwa kina athari ya fasihi katika ukuzaji wa lugha yao na uwezo mbalimbali wa kimaisha.

Shule zilizoteuliwa ni shule tatu za kutwa na nyingine moja ya bweni. Shule hizo tatu za kutwa ni Shule ya Sekondari ya Murehe, Shule ya Sekondari ya Mashesha na Shule ya Sekondari ya Muganza. Shule ya bweni ni College de Nkanka. Shule zote hizi zina michepuo ya Kiswahili. Kwa hivyo, zilichaguliwa kutokana na kwamba zinajumuisha masomo ya fasihi ya Kiswahili katika ratiba zao.

Shule ya Sekondari Muganza na Shule ya Sekondari ya Murehe zilichaguliwa kwa sababu wanafunzi wake wengi hutoka karibu ya mpaka wa Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo na Rwanda. Baadhi ya wanafunzi hawa wanazungumza lahaja ya Kingwana. Koleji ya Nkanka ilichaguliwa kwa sababu wanafunzi wake wengi wanatoka mjini Kamembe na Gihundwe. Shule ya Sekondari ya Mashesha nayo ilichaguliwa kwa sababu ni shule ya kijijini. Kutokana na sampuli zilizoteuliwa, tunaona kwamba zinatofautiana kijiografia. Kwa hivyo, kutofautiana huku kijiografia kunawafanya hata na wanafunzi wake watofautiane kitabia na kimaisha. Hali hii ilitusaidia kupata data tofauti ambazo zilituelekeza moja kwa moja katika kufanikisha utafiti wetu.

### 3.5 Ukusanyaji wa Data

Katika utafiti uliofanyika, zilikusanywa data za aina mbili ambazo ni data za awali na data za upili. Data za awali pia huitwa data ghafi. Hizi ni data ambazo mtafiti huzikusanya, kuziibua na kuzidhihirisha mwenyewe kwa mara ya kwanza. Data za upili ni zile ambazo mtafiti huzikuta mahali fulani zikiwa tayari zimeibuliwa na wataalamu au watafiti waliotangulia

kuhusu mada husika (Ponera, 2019). Utafiti ulikusanya aina zote mbili kama zilivyobainishwa hapo juu. Data za upili zilitusaidia kutambua pengo lililopo katika kazi za watafiti na wataalamu watangulizi wa utafiti huu. Data za awali nazo zilichangia kwa kiwango kikubwa hasa katika ufafanuzi wa tatizo la utafiti na utatuzi wake. Utafiti huu ulitumia mbinu tatu katika ukusanyaji wake wa data. Njia hizo ni pamoja na ushuhudiaji, uchambuzi matini na usaili.

Katika mchakato wa ushuhudiaji, mtafiti alichunguza jinsi walimu wanavyojumuisha fasihi wakati wa ufundishaji wa lugha au wakati wa ukuzaji wa uwezo fulani miongoni mwa wanafunzi. Mtafiti alishuhudia katika tendo la ufundishaji na ujifunzaji darasani. Katika uchanganuzi wa matini, mtafiti alichanganua matini tofauti zinazohusiana na mada yetu ili kutafuta misingi, maoni na mawazo ya wataalamu wengine juu ya swala la utafiti. Katika usaili, mtafiti alihojiana na watafitiwa kuhusu maswali yaliyoandaliwa kwa ajili ya kujibu maswali ya utafiti. Mahojiano yalifanywa kwa lugha mbili ambazo ni lugha ya Kiswahili na Kinyarwanda (lugha mama ya mtafiti na watafitiwa). Kiswahili kilitumika kwa walimu wa Kiswahili na Kinywarwanda kwa wanafunzi ili kuwapa fursa ya kueleza maoni yao bila kizuizi cha lugha.

### 3.5.1 Njia ya Ushuhudiaji

Ushuhudiaji ni njia ya ukusanyaji wa data ambapo mtafiti huwa katika eneo halisi la utafiti na kufuatilia jambo kwa karibu na ana kwa ana (Ponera, Khj). Ushuhudiaji hauhusu tu kuangalia au kusikiliza, bali ni zaidi ya hayo kwani ni uchunguzi wa kimfumo wa hadharani (Stenhouse, 1975 katika Kabir, 2016). Hii ina maana ya kwamba mtafiti hutumia milango yake ya ufahamu yote kwa kuchunguza watafitiwa husika katika mazingira yao halisi au hali halisi zinazowatokea.

Katika utafiti huu, njia ya ushuhudiaji ilitumika kwa walimu wakiwa na wanafunzi darasani. Njia hii ilitumika ili kukusanya data zilizotusaidia kubainisha namna fasihi inavyoweza kutumika katika ufundishaji wa lugha ya pili na utekelezaji wa mtaala unaoegemea katika uwezo kwa wanafunzi wa Kiswahili wa kidato cha tano. Mtafiti aliienda katika maeneo ya walimu na wanafunzi (darasani) ili kuchunguza hali halisi ya ufundishaji na ujifunzaji wa Kiswahili. Mtafiti alikusanya data za ushuhudiaji darasani walimu na wanafunzi wakitumia fasihi katika ufundishaji na ujifunzaji wa lugha ya pili. Mtafiti alikuwa na vifaa kama vile;

rekoda, kinasa picha, kalamu, daftari na vinginevyo kwa kuhifadhi data kutoka eneo halisi (darasani) ili asipate tatizo la kukosa baadhi ya data wakati wa uchunguzi wake.

Njia hii ilitusaidia kukusanya data za kitaamuli za kuonekana ambazo zilitupatia mwelekeo katika kuchunguza tabia, maoni, sifa, na mawazo ya watafitiwa hasahasa wanafunzi na kuyalinganisha kutokana na nyakati mbili tofauti (wakati wa utumizi wa fasihi na wakati wa utumizi wa kazi za ufahamu).

### 3.5.2 Njia ya Uchanganuzi wa Matini

Kwa mujibu wa Ponera (2019), njia ya uchanganuzi wa matini ni njia ambayo mtafiti hupitia matini mbalimbali. Kombo na Tromph (2006) wanaeleza kuwa uchanganuzi wa matini ni mbinu ya kukusanya data kwa kusoma matini ili kupata taarifa muhimu katika utafiti. Katika utafiti huu, mbinu hii ilitumiwa na mtafiti mwenyewe ambapo alisoma kihakiki vitabu, magazeti, majarida, tasnifu, kamusi na mambo mengine yanayotoa habari kuhusu athari za fasihi katika ufundishaji na ujifunzaji wa lugha hususani Kiswahili na utekelezaji wa mtaala unaoegemea uwezo.

### 3.5.3 Njia ya Usaili

Ponera (2019) anafafanua usaili kama njia ya ukusanyaji wa taarifa ambayo inahusisha mazungumzo baina ya mtafiti na watafitiwa wake kuhusu mambo ambayo mtafiti anataka kuyafahamu. Kutokana na majilio ya teknolojia, usaili unaweza kufanywa kwa njia ya vifaa vya kiteknolojia kama vile simu au kompyuta. Hivyo basi, usaili unaweza kufanyika kupitia simu ya moja kwa moja au kupitia njia ya video kwenye mitandao ya kijamii kama vile WhatsApp, Skype, au Telegram (Ponera, Khj). Utafiti ulitumia njia ya usaili kwa wanafunzi na walimu. Mtafiti alikuwa pamoja na watafitiwa wake yaani usaili ulifanyika kwa njia ya ana kwa ana. Hali hii ilitusaidia kukusanya data zilizotusaidia kutathimini ufaafu wa fasihi katika ufundishaji wa lugha ya pili na utekelezaji wa mtaala unaoegemea katika uwezo na kubainisha namna fasihi inavyoweza kutumika katika ufundishaji wa lugha ya pili na utekelezaji wa mtaala unaoegemea katika uwezo kwa wanafunzi wa Kiswahili wa kidato cha tano.

## 3.6 Uchanganuzi wa Data

Uchambuzi wa data ni kitendo cha kupanga, kuchagua, kulinganisha na kutolea maelezo data zilizokusanywa ili ziweze kujibu maswali ya utafiti uliokusudiwa. Utafiti uliofanyika ulitumia

mkabala wa kimaelezo. Huu ni mkabala ambao hutumika kuchambua data za utafiti kwa kuzitolea maelezo ya kina kwa mwelekeo ambao unasaidia kutimiza malengo mahususi ya utafiti. Data za utafiti huu ziliwasilishwa kwa njia ya madondoo na kisha kuchambuliwa kwa madondoo hayo kwa kutolewa maelezo ya kina yaliyojibu maswali ya utafiti.

Wakati wa uchanganuzi wa data, utafiti ulitumia mbinu zisizo za kikompyuta japo mtafiti alitumia kompyuta kuandika nukuu zilizochukuliwa wakati wa ukusanyaji wa data, kuhifadhi nyaraka na rekodi mbalimbali, kuhariri nyaraka mbalimbali, kuchora picha na michoro mbalimbali inayohusiana na utafiti na kuandika tasnifu.

Katika uchambuzi wa data, si vizuri kutaja majina ya watafitiwa. Hivyo basi, misimbo ndiyo ilitumika ili kutofautisha watafitiwa wetu wa utafiti. Tulitumia A1 kuwakilisha shule ya kwanza tukihusisha mwalimu wa Kiswahili kwenye shule ya kwanza. Tulitumia A2 kwa kuwakilisha mwanafunzi wa Kiswahili katika shule ya kwanza. B inawakilisha shule ya pili. Hivyo basi, B1 inawakilisha mwalimu wa Kiswahili kwenye shule ya pili na B2 inawakilisha mwanafunzi wa Kiswahili kwenye shule ya pili. C nayo, inawakilisha shule ya tatu, C1 ni mwalimu wa Kiswahili kwenye shule ya tatu na C2 ni mwanafunzi wa Kiswahili kwenye shule ya tatu.  D inawakilisha shule ya nne D1 inawakilisha mwalimu wa Kiswahili kwenye shule hiyo na D2 inawakilisha mwanafunzi wa Kiswahili kwenye shule hiyo. Uchambuzi na ufasili wa data uliongozwa na Nadharia ya Utambuzi na Maingiliano ya Tamaduni-jamii.

### 3.7 Itikeli za Utafiti

Parveen na Showkat (2017) wanafafanua itikeli kama kanuni za kimaadili zinazotawala tabia ya mtu. Kwa hivyo, itikeli ya utafiti inaweza kutazamwa kama kufanya kile ambacho kinakubaliwa kimaadili na kisheria katika utafiti (Parveen na Showkat, Whj). Itikeli ya utafiti ni kipengele cha utafiti kinacholenga kuweka urazini wa mtafiti kuhusu thamani, haki na hadhi za watafitiwa wake (Ponera, 2019). Katika utafiti huu kama inavyotarajiwa kuwa katika utafiti wowote, itikeli za utafiti zinapaswa kupewa thamani yake. Hii ndiyo maana hatua zifuatazo zilifuatiliwa ili kuhakikisha kwamba itikeli hizo zimefuatwa.

Mosi, mtafiti alifanya utafiti akiwa na ruhusa ya kufanya utafiti wake aliyopewa na Chuo Kikuu cha Rwanda pamoja na ruhusa kutoka kwa Mkuu wa Wilaya ya Rusizi. Ruhusa hizi mbili zilikuwa zinampa uwezo wa kuingia maeneo ya watafitiwa wake na kuwa na mawasiliano nao. Pili, mtafiti aliwaelezea kuhusu utafiti na malengo yake na kuwaomba ridhaa ya kujisikia huru kushiriki katika utafiti. Tatu, mtafiti aliwaomba ruhusa la kurekodi

data na kuwaahidi kwamba hakuna aina yoyote ya madhara iwe ya kimwili, kisaikolojia, kiafya au kisheria itakayowakumba wala kuwajia kutokana na utafiti wakati wa ukusanyaji wa data. Nne, mtafiti aliondoa kabisa uwezekano wa kutokea kwa hatari kwa watafitiwa wakati na baada ya utafiti. Tano, mtafiti aliwajuza watafitiwa kuwa huru kushiriki katika utafiti iwezekanavyo mpaka mwisho wake. Sita, mtafiti alitunza vizuri siri za taarifa za utafiti na kuficha majina ya watoa taarifa kadiri ya matakwa yao. Saba, mtafiti alizingatia maadili ya jamii za watafitiwa wake na kuepuka udanganyifu wa taarifa.

### 3.8. Uhalali na Uthabiti wa Utafiti

Uhalali na uthabiti unaeleza jinsi data zilizokusanywa zinavyoshughulikia vyema eneo halisi la utafiti (Ghauri na Gronhaug, 2005 katika Taherdoost, 2016). Uhalali na uthabiti wa utafiti ulihusu kuweka bayana malengo ya utafiti kwa watafitiwa ili waelewe lengo la utafiti ni lipi na utafiti utatoa mchango upi katika uga wa elimu. Pili, mtafiti alitumia lugha rahisi na ya kawaida katika zana za kukusanyia data ili washiriki wasitatizwe na uelewa wa habari au ujumbe uliomo au mwongozo wa matokeo yanayotarajiwa. Hii iliwasaidia washiriki wa utafiti kujibu vizuri maswali waliyoulizwa na mtafiti kwa upande mmoja na mtafiti alifaidika kupata matokeo aliyoyatarajia ambayo yalijielekeza moja kwa moja kwenye malengo ya utafiti. Tatu, kama inavyoelezwa na Kothari (2008) matumizi ya njia mseto katika ukusanyaji wa data, huongeza kiwango cha uthabiti na kuaminika kwa utafiti. Hivyo basi, mtafiti alitumia mchanganyiko wa njia mbalimbali za kukusanyia data kama vile mahojiano na ushuhudiaji. Mtafiti pia aliepukana na matumizi ya hisia binafsi na upendeleo kiasi cha kuathiri mwelekeo wa utafiti. Kulingana na hatua zilizozingatiwa hapo juu kama zilivyofuatiliwa katika utafiti, hatuna budi kuwa uhalali na uthabiti wa utafiti wetu ulikuwa bora.

### 3.9Muhtasari wa Sura ya Tatu

Sura hii ilihusu methodolojia ya utafiti. Ilishughulikia uwasilishaji wa mbinu na zana mbalimbali za kukusanyia na kuchambua data. Katika kukamilisha mbinu za utafiti, vipengele vya usanifu wa utafiti, eneo la utafiti, aina ya utafiti wango, sampuli na usampulishaji, aina ya data, mbinu za kukusanyia data, uchanganuzi wa data na itikeli, uhalali na uthabiti wa utafiti vilielezwa. Sura inayofuata inahusu uwasilishaji, uchambuzi wa data na mjadala wa matokeo ya utafiti.

## SURA YA NNE: UWASILISHAJI, UCHAMBUZI WA DATA NA MJADALA WA MATOKEO.

### 4.1 Utangulizi

Utafiti uliofanyika ulisukumwa na wazo la kwamba suala la fasihi kama nyenzo ya kufundishia lugha ya pili kwa upande mmoja na utekelezaji wa mtaala unaoegemea katika uwezo, halijashughulikiwa vema. Utafiti ulikusudia kutimiza malengo mahususi mawili. Mosi, ni kutathimini ufaafu wa fasihi katika ufundishaji wa lugha ya pili na utekelezaji wa mtaala unaoegemea katika uwezo kwa wanafunzi wa Kiswahili wa kidato cha tano. Pili, ni kubainisha namna fasihi inavyoweza kutumika katika ufundishaji wa lugha ya pili na utekelezaji wa mtaala unaoegemea katika uwezo kwa wanafunzi wa Kiswahili wa kidato cha tano.

Katika sehemu ya nne tulifanya mawasilisho ya mjadala wa matokeo ya utafiti. Sura hii inajumuisha sehemu zifuatazo. Sehemu ya kwanza ni utangulizi. Sehemu ya pili ni kutathmini ufaafu wa fasihi kama nyenzo ya ufundishaji wa lugha ya pili. Sehemu ya tatu inatathmini ufaafu wa fasihi katika utekelezaji wa mtaala unaoegemea katika uwezo. Sehemu ya nne nayo inahusu kuchunguza namna fasihi inavyoweza kutumiwa kama nyenzo ya kufundishia lugha. Kisha sehemu ya tano inachunguza namna fasihi inavyoweza kutumiwa kama nyenzo ya utekelezaji wa mtaala unaoegemea katika uwezo. Sehemu ya mwisho ni muhtasari wa sura ya nne.

### 4.2 Ufaafu wa Fasihi katika Ufundishaji wa Lugha ya Pili kwenye Muktadha wa Utekelezaji wa Mtaala Unaoegemea katika Uwezo.

Kutokana na wazo la kwamba fasihi hutumia lugha kwa kushughulikia maisha ya mwanadamu Ntarangwi (2004) na Wamitila (2004), tuna haja ya kwamba fasihi pia huweza kufaa kwa kufundishia lugha na kutekeleza mtaala unaoegemea katika uwezo kwa wakati mmoja. Hivyo basi, ni bora kutathimini namna ambavyo fasihi huweza kufaa kufundisha vipengele vya lugha kama vile msamiati halisi na sarufi pamoja na stadi za lugha. Kwa upande mwingine ni bora kutathimini namna ambavyo fasihi huweza kufaa kufundisha uwezo wa jumla, maswala mtambuka pamoja na mitazamo na thamani kwa wanafunzi husika.

### 4.2.1 Utayari wa Walimu katika Utumizi wa Fasihi Kufundishia Lugha na Kutekeleza Mtaala

Data za ushuhudiaji na usaili zilionesha kwamba tatizo kubwa lipo kwa upande wa walimu. Tatizo lenyewe linatokana na ujuzi mdogo wa ufundishaji wa lugha ya pili pamoja na uelewa juu ya fasihi. Hali hii huwafanya walimu kutotambua wala kujua jinsi ya kutumia fasihi kama nyenzo sio ya kufundishia lugha tu lakini pia kama nyenzo ya kukuza uwezo wa jumla kwa mwanafunzi. Kwanza kabisa, walimu wa lugha ya Kiswahili wanapaswa kuelewa maana ya fasihi na kuitofautisha na sanaa nyingine. Hata hivyo, matokeo ya usaili yalionesha kwamba hata maana ya fasihi yenyewe bado huwasumbua. Hali hii ililetamashaka makubwa kwetu juu ya utumizi wa fasihi kama nyenzo ya ufundishaji na ujifunzaji wa lugha na utekelezaji wa mtaala unaoegemea katika uwezo. Haya ni maelezo ya mwalimu C1 kuhusu maana ya fasihi:

> Fasihi ni sanaa zimulikazo mila, desturi na utamaduni wa wanadamu.

Fasili ya mwalimu huyu juu ya fasihi, inaonesha upungufu katika utofautishaji wa fasihi na sanaa nyingine. Hii ni kutokana na ukweli kwamba fasihi haiwezi kupewa jina hili ‘fasihi’ wakati haitumii lugha. Hali hii huwakilisha uhusiano wa kikaribu uliopo kati ya fasihi na lugha. Hivyo basi, maana iliyotolewa hapo juu, inapuuza uhusiano huu wa fasihi na lugha. Hali hii inasababisha pia walimu wa lugha kupuuza fasihi katika ufundishaji wa lugha kwani hawajui uhusiano kati ya lugha na fasihi.

Baadhi ya wanafunzi huitazama fasihi kama sanaa za kijadi ambazo zinawasilisha utamaduni asilia wa jamii husika. Haya ni maoni ya mwanafunzi mmoja. Anasema:

> Fasihi ni sanaa zenye umuhimu kwa sababu zinatusaidia kujua tamaduni na maisha ya jamii za zamani ambazo mababu zetu walikuwa wanaishi.

Dondoo hili linatuonesha kwamba baadhi ya wanafunzi huitazama fasihi kama historia yaani haielezi maisha halisi ya sasa. Hili ni tatizo katika ufundishaji na ukuzaji wa stadi za Karne ya Ishirini na Moja kwani fasihi inapotenganishwa na maisha ya watu wa sasa, basi haiwezi kutiliwa maanani wakati wa ufundishaji na ujifunzaji.

Utumizi wa fasihi hususan fasihi simulizi huwamotisha wanafunzi wa kidato cha tano kujifunza Kiswahili. Hapa tuna maoni ya mwanafunzi mmoja akisema:

> Fasihi hasa fasihi simulizi mara nyingi hutumia lugha nyepesi na msamiati rahisi. Kingine, ni kwamba huwa na wahusika wa kustaajabisha ambao mara nyingi ni wanyama. Lakini pia, fasihi simulizi huwa fupi yaani haitufanyi kuchoka kila wakati tunaposoma hadithi inakwisha bila sisi kutarajia mwisho wake.

Dondoo hili linaonesha kwamba wanafunzi wanafurahia kazi za fasihi ya Kiswahili. Hivyo basi, mwalimu wa lugha angetumia fursa hii kwa kufuatilia mchakato wa kuwafundisha lugha na kuwakuzia uwezo wa jumla kupitia fasihi. Utumizi wa kazi zenye lugha rahisi ambayo wanaielewa huweza kuwafanya kuelewa mambo mengi kuhusiana na lugha au uwezo mwingine.

### 4.2.2 Fasihi na Ufundishaji wa Lugha ya Pili

Fasihi ni sanaa inayotumia lugha kwa kutoa picha halisi ya maisha ya mwanadamu (Ntarangwi 2004; Wamitila, 2004). Kutokana na fasili hiyo, inaonekana kwamba, kuna uwezekano mkubwa wa kufundisha lugha kupitia fasihi. Kwa hivyo, katika sehemu inayofuata tutajadili ufaafu wa fasihi kama nyenzo ya kufundishia sarufi, msamiati, stadi za kuandika, kusoma, kusikiliza, na kuzungumza.

#### 4.2.2.1 Fasihi kama Nyenzo ya Kufundishia Sarufi

Kwa mujibu wa muhtasari, wa Kiswahili wa REB (2015) katika kidato cha tano unaotumiwa leo, fasihi inajitokeza kwa sehemu kubwa kuliko sehemu nyingine yoyote ile inayopaswa kufundishwa katika kidato hiki. Hata hivyo, kwa kila mada ya fasihi kuna kipengele cha sarufi. Hivyo basi, kuna fursa ya kufundisha sarufi kupitia fasihi. Wataalamu mbalimbali nao wanatetea ufaafu wa fasihi kama nyenzo ya kufundishia sarufi. Hili ni dondoo kutoka Elkiliç na wenzake (2011: 492). Wanasema:

> Therefore, it is essential that language teachers bring the literature into language classroom especially for teaching structures of grammar, morphology, phonology and syntax of the target language, using their own imagination and developing the own creativity of the students.

> Kwa hivyo, ni muhimu kwamba walimu wa lugha walete fasihi katika darasa la lugha haswa kwa kufundishia miundo ya sarufi, mofolojia,

> fonolojia na sintaksia ya lugha lengwa, kutumia mawazo yao wenyewe na kuendeleza ubunifu binafsi wa wanafunzi [Tafsiri Yetu].

Data za usaili na ushuhudiaji zilizokusanywa na utafiti wetu nazo zinaonyesha kwamba utumizi wa kazi za fasihi ya Kiswahili au fasihi kwa Kiswahili unaweza kuwasaidia wanafunzi kujifunza mifumo na miundo mbalimbali ya lugha ya Kiswahili kama vile miundo ya maneno, miundo ya vishazi na sentensi, miundo ya aya na kuwakuzia uwezo wa kutengeneza kazi zao binafsi katika lugha ya Kiswahili. Hapa chini tuna dondoo la mwanafunzi B2 tulipomwuliza “Je, fasihi ya Kiswahili inaweza kukusaidiaje kujifunza sarufi ya Kiswahili”.

> Fasihi inaweza kunisaidia sana kujifunza sarufi kwa sababu sarufi ni matumizi sahihi ya lugha. Fasihi inatumia sentensi nyingi ambazo tunaweza kuiga ili tuweze kutengeneza zetu. Pia, katika fasihi tunapata mifano ya matumizi ya mambo ya kisarufi kama vile matumizi ya aina za maneno (vivumishi, vielezi, vitenzi, viwakilishi n.k) na matumizi ya ngeli za majina. Hayo yote tunaweza kuyakuta katika kazi fulani za fasihi.

Kutokana na maoni ya mwanafunzi B2 inaonekana kuwa hata wanafunzi wanaona fursa zilizopo katika utumizi wa fasihi katika kuwafundishia lugha. Kwa kuegemea hoja yaNadharia ya Utambuzi ya kwamba utambuzi unahusu uelewa juu ya habari na utambuzi wa michakato ya kiakili kwa kusisitiza upekee pamoja na utofauti wa watu katika fikra, uamuzi na utoaji wa mawazo, uchambuzi wa data zetu kutoka usaili, uchanganuzi wa matini na ushuhudiaji kuhusu fasihi na ufundishaji wa sarufi, ulionesha matokeo yafuatayo:

i. Fasihi inaweza kutoa taarifa za maana zinazosaidia ujifunzaji wa miundo ya kisarufi. Kwa hivyo, fasihi inaweza kusababisha ujifunzaji kwa uangalifu wa kisarufi.
ii. Wanafunzi wanaweza kuhimizwa kuwasiliana kwa maana.
iii. Fasihi inaweza kutoa mifano thabiti ya kisarufi ambayo inaweza kuigwa na mwanafunzi katika ujifunzaji wa sarufi ya lugha lengwa.
iv. Uwezo wa wanafunzi kuelewa, kuchambua na kufasili unaweza kuboreshwa.
v. Uhuru wa mwanafunzi katika ujifunzaji wa sarufi unaweza kuongezwa.
vi. Stadi na mikakati ya wanafunzi ya kusoma na kuandika inaweza kuboreshwa.

Matokeo kuhusu matumizi ya fasihi katika ufundishaji wa lugha, yalipatikana kwa kuchambua data zinazohusu mifano ya kifasihi na uchakataji wa ubongo wa mwanafunzi kwa ajili ya kuielewa mifano hiyo. Uchambuzi na uhusishaji wa data hizo, uliegemeakatika msingi

wa Nadharia ya Utambuzi juu ya ujifunzaji lugha. Msingi huo ni kwamba binadamu ana uwezo wa kuunda sentensi nyingi kutokana na maneno machache aliyonayo. Hivyo basi, Nadharia ya Utambuzi ilitusaidia kuchambua mifano inayotokana na fasihi na kuiunganisha na uwezo alio nao mwanafunzi wa kujifunza na kupanua uwezo wake wa kisarufi kupitia mifano aliyopewa.

#### 4.2.2.2 Ufaafu wa Fasihi katika Ufundishaji wa Msamiati

Ujifunzaji wa msamiati ni sehemu muhimu katika mchakato wa ujifunzaji wa lugha ya kigeni. Msamiati unajikita kueleza au kuelewa maana za maneno mapya. Mara nyingi sehemu hii husisitizwa katika ufundishaji na ujifunzaji wa lugha. Pia, ni kitovu cha ufundishaji wa lugha na ni muhimu sana kwa mwanafunzi wa lugha. Matokeo ya utafiti yanaonyesha kwamba walimu na wanafunzi waliotafitiwa, wanaelewa umuhimu wa kipengele hiki katika ujifunzaji wa lugha ya pili. Pia, wanaonesha jinsi fasihi inavyoweza kuchangia katika ufundishaji wa kipengele hiki miongoni mwa wanafunzi husika. Haya ni maoni ya mwanafunzi A2.

> Fasihi inaweza kunisaidia kujifunza msamiati sana kwani kazi za fasihi hubeba msamiati kadhaa ambao mara nyingi hutumiwa katika mazungumzo yetu ya kila siku. Msamiati huo ni muhimu kwetu ila aghalabu hatuuelewi. Hivyo basi, kutokana na kazi ya fasihi tunayoshughulikia, tunaweza kujifunza na kuelewa msamiati uliomo. Mwalimu pia hawezi kutufundisha kamusi hata nasi hatuvutiwi na kamusi kutokana na orodha ya maneno mengi yaliyomo. Hivyo basi, tunapovutiwa na kusoma, tutakuwa na hamu ya kutafuta msamiati unaotusumbua ili kuelewa maana nzima ya hadithi ambayo tunasoma.

Kutokana na dondoo la hapo juu inaonekana kwamba wanafunzi wanajua kwamba kipengele cha msamiati ni muhimu sana hasa katika umilisi wa kimawasiliano. Pia, wanafunzi hawa wanahakikisha mchango wa fasihi katika ufundishaji wake kwa kuilinganisha na kamusi. Kwao, wanaona kamusi haiwavutii kujifunza msamiati kama kazi ya fasihi. Hii ni kutokana na ukweli kwamba kamusi inajumuisha orodha ya maneno tu bila wahusika wala masimulizi ya kuchekesha na kuvutia wala kumhamasisha mwanafunzi kujifunza msamiati husika.

Hata silabasi ya Kiswahili inapendekeza kufundisha msamiati kutokana na kazi fulani ya fasihi inayoshughulikiwa. Hii inathibitishwa na kwamba baada ya mada ya kifasihi katika muhtasari wa Kiswahili, kunasehemu ya msamiati kama anwani ya kushughulikiwa kwa kueleza baadhi ya msamiati uliomo katika kifungu cha fasihi husika.

Walimu nao wanathibitisha kuwa fasihi inawasaidia kufundisha msamiati mwingi kuliko vifungu vya aina nyingine za habari. Haya ni maelezo ya mwalimu C1 akieleza uwezekano wa fasihi kujumuisha mifano ya ufundishaji wa msamiati.

> Fasihi inatufafanulia juu ya ufundishaji wa msamiati kwani tunakutana na msamiati mwingi tena muhimu kwa mazungumzo ya watu wengi. Nadhani kuwa hali hii inatokana na jukumu la fasihi la kuwasilisha maisha halisi ya watu. Kutokana na jukumu hili, fasihi inatupa msamiati wa kutumia katika maisha yetu ya kila siku. Hii ni fursa ya kushirikisha na kufundisha msamiati husika kwa wanafunzi wetu.

Kutokana na dondoo kutoka mwalimu C1, inaonekana kuwa walimu wanaamini fasihi kuwa na mifano ya msamiati halisi wa kutumia katika mazungumzo ya kila siku. Pia, wanakubali kuwa fasihi inaweza kuwa nyenzo mwafaka ya kufundishia msamiati husika.

Henrietta na Antonela (2021:1) wanachangia katika kueleza nafasi ya msamiati katika ujifunzaji wa lugha ya pili na nafasi ya fasihi katika ujifunzaji wa sehemu hii katika ujifunzaji wa lugha. Wanafafanua hivi:

> Without assimilating enough vocabulary, students cannot have relevant communication, cannot express their ideas and cannot understand each other. On the other way, literature unites the past with the present and makes us aware of our value. It not only provides information but also provides a closer look at things. It reflects the state of a society, its values, strengths and weaknesses. literature is an authentic material that exposes the student to everyday vocabulary.

> Bila kuingiza msamiati wa kutosha, wanafunzi hawawezi kuwa na mawasiliano yenye maana, hawawezi kueleza mawazo yao na hawawezi kuelewana. Kwa upande mwingine, fasihi inaunganisha yaliyopita na ya sasa na kutufanya tufahamu thamani yetu. Inatoa sio habari tu, bali pia hutoa uangalizi wa mambo kwa ukaribu. Inaakisi hali ya jamii, maadili, nguvu na udhaifu wake. Fasihi ni nyenzo halisi inayomfichulia mwanafunzi msamiati wa kila siku [Tafsiri Yetu].

Kutokana maoni ya Henrietta na Antonela (Khj) pamoja na matokeo ya data zilizokusanywa uwandani, tuliona kwamba fasihi inaweza kuwa nyenzo mwafaka ya kufundishia msamiati

iwapo inatumiwa ipasavyo. Hata maoni ya wanafunzi watafitiwa yanapendekeza utumizi wa kazi za fasihi katika kuwafundishia msamiati. Hata hivyo, ubora wa utumizi wa fasihi katika ufundishaji wa msamiati unatokana na mifano yake ya msamiati halisi kama inavyoelezwa na data zilizokusanywa.

Katika tasnifu hii, tumechambua hali ya fasihi ya kushughulikia maisha halisi ya watu ambayo inaisababisha kuzingatia msamiati halisi wa shughuli zao. Uchambuzi huu unahusisha malengo ya mtaala unaoegemea katika uwezo juu ya lugha na msamiati halisi unaotokana na fasihi. Uhakiki huu wa kuhusisha malengo ya mtaala juu ya lugha na kile kilichomo katika fasihi kuhusu lugha na utekelezaji wa mtaala, ni uhakiki unaoegemea Nadharia ya Maingiliano ya Tamaduni-jamii.

#### 4.2.2.3 Fasihi katika Ufundishaji wa Stadi ya Kusoma

Stadi ya kusoma ni uwezo wa utambuzi ambao mtu anaweza kuitumia wakati wa kuingiliana na maandishi yaliyoandikwa (Grabe, 2009). Matumizi ya fasihi katika ufundishaji wa stadi yakusoma ni mbinu mojawapo ya kufundishia ujuzi wa msingi katika lugha lengwa na ujuzi wa lugha nzima kwa wakati mmoja (Minardi, 1994). Ni njia bora kwa walimu ambao wanataka kufanya mabadiliko ya wanafunzi kutoka katika ujuzi wa msingi kwenda kwa ujumla wa lugha zaidi.

Minardi (khj) anaorodhesha faida za kutumia fasihi katika ufundishaji wa stadi ya kusoma kama ifuatavyo. Mosi, ni kuwezesha ukuzaji wa lugha. Pili, ni kuongeza ufaulu wa kusoma na kuimarisha ujuzi na mikakati ya kusoma miongoni mwa wanafunzi. Tatu, ni kukuza stadi na mitindo ya uandishi. Nne, ni kuhimiza fikra za hali ya juu. Tano, ni kuimarisha muunganisho wa stadi nne za lugha. Sita, ni kuhamasisha wanafunzi kusoma. Na saba, ni kuhimiza ushiriki wa wanafunzi katika somo.

Kutokana na data za usaili kati ya mtafiti na walimu wa Kiswahili, fasihi inasaidia walimu kufundisha stadi za kusoma kama inavyoelezwa na mwalimu D1.

> Fasihi inatusaidia sana kukuza uwezo wa wanafunzi wa kusoma. Kutokana na utamu pamoja na motisha iliopo katika usomaji wa kazi za fasihi, wanafunzi wanapenda kusoma kazi za fasihi kuliko vifungu vingine vya habari. Sisi mara nyingi tunatafsiri kazi simulizi za fasihi ya Kinyarwanda katika Kiswahili. Kazi hizo wanafunzi wanazipenda mno kwani wanazisoma wakiwa na hamu ya kujua Kiswahili cha mambo

> wanayoyajua katika Kinyarwanda. Hata hivyo, wanafunzi huvutiwa na kusoma kazi za fasihi kutokana na hamu ya kujua nini kitafuata hasa kutokana na migogoro kati ya wahusika waliomo katika kazi husika.

Dondoo hili linatuonesha kwamba walimu wanaona fursa iliopo katika fasihi kwa kufundisha stadi za kusoma. Wanaelewa sababu ya kutumia fursa hiyo kwa kuwafundisha wanafunzi stadi za kusoma. Fursa iliyopo si nyingine ila ni ule utamu na motisha kwa wanafunzi.

Wanafunzi nao wanathibitisha wazo la kwamba fasihi inawamotisha na kuwafurahisha sana wakati wa kusoma. Haya ni maoni ya mwanafunzi C2.

> Aghalabu fasihi huwa na wahusika wa kufurahisha na kuchekesha. Matendo yao humvutia mtu wakati wa kusoma. Kingine ni kwamba mwalimu au mwanafunzi mwenzetu anaposoma nasi tunafuata ili tusikie habari yote.

Kutokana na maoni ya mwanafunzi C2 inaonekana kuwa wanafunzi hufurahia hadithi za kifasihi kutokana na wahusika pamoja na migogoro kati yao. Hivyo basi, ni bora kutumia fursa hii kwa kuwafundisha stadi za kusoma na kuwahimiza kupenda tabia na thamani za kusoma.

Hata wakati wa ushuhudiaji, mtafiti aliona kwamba madarasa yaliyokuwa yakitumia hadithi za kifasihi, wanafunzi walikuwa wachangamfu na wenye furaha tofauti na madarasa yaliyotumia vifungu vya habari visivyo vya kifasihi. Kila mwanafunzi alikuwa akitaka kufika mbele ya wenzake ili kuwasomea hadithi inayoshughulikiwa. Wengine walikuwa wakifuatilia vizuri wakati mwenzao alipokuwa akisoma.

Sehemu hii, ilichambua mamlaka na motisha ya fasihi kuhusu usomaji na kuihusisha na mahitaji pamoja na uwezo wa mwanafunzi juu ya usomaji. Uhakiki huu wa kutambua motisha na mamlaka iliyomo katika kazi za fasihi na kuihusisha na kile ambacho mwanafunzi anakipenda na kukitamani kutoka usomaji, ni uhakiki wa kiutambuzi.

#### 4.2.2.4 Fasihi kama Nyenzo ya Kufundishia Stadi ya Kuandika

Fasili za kuandika zinaweza kugawanywa katika kategoria tatu kulingana na mikabala ya ufundishaji wa stadi ya kuandika. Mikabala hiyo ni pamoja na mkabala unaozingatia msomaji na aina ya kazi, mkabala unaozingatia mchakato na utambuzi, na pia mkabala unaozingatia matokeo na maandishi (Yi, 2009).

Kwa mujibu wa mkabala unaozingatia msomaji na aina ya kazi, stadi ya kuandikainafafanuliwa kama uwezo wa kujibu kichocheo fulani kulingana na ufafanuzi wa mamlaka fulani kuhusu jibu sahihi (Nunan, 1999 katika Yi, 2009). Kulingana na mkabala unaozingatia mchakato na utambuzi, ustadi wa kuandika hufafanuliwa kama uwezo wa kuanzisha na kuendeleza mawazo na kisha kutumia uhakiki fulani na mazoezi ya kuyahariri ili kuyakuza hadi kukomaa katika muktadha fulani (Yi, khj). Mkabala huu unazingatia matokeo na maandishi. Ni mkabala unaodai kuwa ustadi wa kuandika ni uwezo wa kufanya kazi za uandishi zinazotosheleza majadiliano ya jumuiya maalum na kuzingatia muundo na maudhui ya majadiliano na mawasiliano ya kiutendaji. Kutokana na mikabala hii mitatu, inawezekana kusema kwa kifupi kwamba stadi ya kuandika ni uwezo wa kuchakata na kutoa matokeo kwa kutumia maandishi. Fasihi inaweza kufaa kwa kukuza ustadi wa kuandika kulingana na mahitaji ya kila mkabala miongoni mwa mikabala mitatu kama ilivyobainishwa hapo juu.

Wataalamu kadhaa wamejadili juu ya ufaafu wa fasihi katika ufundishaji wa stadi za kuandika Babaee na Yahya (2014:82) wanasema:

> Literature is a valuable and reliable source for developing writing skills in foreign language classes. Literature provides the learners with a model that provokes them to write like the original work in content, theme, style and organization. Also, literature embodies variety of themes to write on. Thus, it can give enough ideas to the learners to start their writing with.

> Fasihi ni chanzo muhimu na cha kutegemewa kwa kukuza ustadi wa kuandika katika madarasa ya lugha ya kigeni. Fasihi huwapa wanafunzi mfano unaowachochea kuandika kama kazi asilia kimaudhui, kidhamira, kimtindo na kimpangilio. Pia, fasihi hujumuisha maudhui mbalimbali ya kufanyia maandishi. Hivyo, inaweza kutoa mawazo ya kutosha kwa wanafunzi ili nao waanze kuandika [Tafsiri Yetu].

Maoni ya watafitiwa wa utafiti uliofanyika, nayo hayatofautiani na mawazo ya wataalamu wa hapo juu. Data za usaili zilionesha kwamba watafitiwa wanahakikisha kwamba fasihi inashiriki kwa kiasi kukubwa katika ukuzaji wa stadi za kuandika; ziwe za maandishi sahihi ya kawaida au maandishi ya kitaaluma. Utafiti ulipata dondoo la mwanafunzi B2. Anasema:

> Tunaposoma kazi za fasihi, mara nyingi tunafanya mihtasari yetu ili tuweze kuzielewa zaidi. Wakati huo wa kutengeneza mihtasari yetu, tunajifunza mengi yahusuyo kuandika. Tunazoea maandishi sahihi ya

> herufi fulani lakini pia tunajifunza namna ya kuandika kitaaluma kupitia fasihi kwa kufanya utangulizi, kiini chenye mawazo mbalimbali na hitimisho.

Dondoo hili linathibitisha mawazo ya wataalamu mbalimbali kama vile Wissinger na wenzake (2020) wakisema kuwa katika kipindi cha miaka kumi iliyopita, tafiti zinaonesha kuwa ni bora kuweka nguvu zaidi katika ufundishaji wa stadi ya kuandika kuliko stadi nyingine za lugha. Hali hii inatokana na ukweli kwamba mwanafunzi anayejua kuandika neno, au herufi fulani ni rahisi kwake kujua namna ya kuisoma na kuitumia katika mazungumzo na hata kuisikiliza wakati inapotumiwa katika mawasiliano fulani. Ni kweli kwamba stadi ya kuandika itiliwe nguvu zaidi kuliko stadi nyingine zote zile kwani ni nguzo na msingi wa lugha yoyote. Hivyo basi, walimu wa lugha wanatarajiwa kusisitiza stadi hii kwa kutumia nadharia, mikabala, mbinu na mikakati mbalimbali ili kuwafanya wanafunzi kuumudu ustadi huu.

Katika mchakato wa kuyapata matokeo ya hapo juu, kuna haja ya kuegemea katika misingi ya Nadharia ya Utambuzi ya kwamba lugha ni matokeo ya uchakataji wa ubongoni, na kwamba mtu huchakata kwa kukumbuka na kuiga mifano fulani ya lugha. Misingi hii ilisaidia kuhusianisha mifano ya kimaandishi inayotolewa na fasihi na uelewa wa mwanafunzi juu yake kutokana na uchakataji wake wa ubongoni kwa ajili ya kutoa kitu kipya. Pia, kutokana na Nadharia ya Utambuzi, ilihusishwa matokeo ya kimaandishi ya mwanafunzi mwenyewe na uchakataji kumbukumbu zake ili kuyasoma, kuyasikiliza na kuyazungumza. Na hapa ndipo tuliona kwamba stadi ya kuandika ndiyo msingi wa stadi nyingine za lugha.

#### 4.2.2.5 Fasihi na Ufundishaji wa Stadi za Kuzungumza na Kusikiliza

Stadi za kuzungumza na kusikiliza ni zana muhimu katika maisha ya mwanafunzi ya kila siku, nyumbani, kazini, na katika jamii. Hali hii inatokana na ukweli kwamba stadi hizi ndizo mzazi wa lengo kuu la ufundishaji na ujifunzaji wa lugha ambalo ni mawasiliano. Mawasiliano hayawezi kufanikishwa wakati hakuna kusikiliza wala kuzungumza.

Ikiwa huwezi kusikia lugha vizuri, utapata ugumu wa kuwasiliana au pengine huwezi kufanya kazi ya kusikiliza. Kwa hakika, mara nyingi wanafunzi hupewa au huchukua misingi isiyo imara katika ujifunzaji wa stadi za kusikiliza na kuzungumza. Hali hii inawasababishakuelekea kwenye matokeo mabaya ya lugha.

Bila shaka, shughuli za kidrama kama vile uigizaji ni muhimu kwa wanafunzi wa lugha ya pili kwani huwawezesha kuharakisha ukuzaji wa ustadi wa kutumia mdomo wakati wa kuzungumza, huhamasisha wanafunzi kupata ufahamu wa wazi na kina kwa kazi zenye ushawishi kupitia masikio na ubongo (Hişmanoğlu, 2005).

Wakati wa usaili, wanafunzi nao walithibitisha wazo la Hişmanoğlu (Khj) kwamba fasihi inawapa fursa ya kuzungumza zaidi na huwahamasisha kutega masikio ya mwili na akili. Hapa tuna dondoo kutoka mwanafunzi A2 kuhusu mjadala huu. Anasema:

> Wakati wa kusoma hadithi za kifasihi tunatega masikio kwa kina wakati huu, mimi najaribu kuchakata kichwani maana za yale wanayosoma. Baada ya kuisoma kazi husika, kila mwanafuzi anatengeneza muhtasari wake binafsi na kuushirikisha kwa wenzake mbele kwa mdomo. Mara nyingi tunaigiza michezo kwa kupewa majukumu mbalimbali yanayohusu mchezo huo kisha tunauigiza mbele ya wanafunzi wengine. Hali hii inatusaidia kuzungumza sana. Ingawa tuna msamiati mdogo lakini tunajaribu kuutumia iwezekanavyo.

Wanafunzi wote waliohojiwa kuhusu ufundishaji wa stadi za kusikiliza na kuzungumza, walieleza kuwa wengi wanaweza kusikiliza mambo mengi katika Kiswahili. Wanasema kwamba tatizo kubwa walilo nalo ni kuzungumza. Hata hivyo, fasihi inawaundia mazingira ya kuchangamka wakazungumza kama wanavyoweza. Kwa kuegemea Nadharia ya Maingiliano ya Tamaduni-jamii, inaonekana kwamba hali ya kuchangamka na kuzungumza kwa wanafunzi kutokana na kazi za fasihi, hutokana na sababu kadhaa. Mosi, ni athari za wahusika wanaojitokeza wakibeba sifa na tabia zinazopatikana katika jamii halisi za wanafunzi. Pili, ni maingiliano ya mwalimu na wanafunzi juu ya kazi husika. Tatu, ni athari na tabia za mwalimu na wanafunzi kama mifano kwa wanafunzi wengine juu ya kazi husika.  Hali ya uchangamfu ni msingi imara katika mchakato wa ujifunzaji wa lugha kwani humfanya mwanafunzi kutoogopa kufanya makosa ya kimazungumzo. Hali hii hukuza umilisi wa kuzungumza ambao ndio lengo kuu la ujifunzaji wa lugha yoyote ile.

Mchango huu wa fasihi katika uwezeshaji wa uzungumzaji miongoni mwa wanafunzi, unathibitishwa na walimu kama inavyoelezwa na mwalimu B1.

> Wakati wa kushughulikia kazi fulani ya fasihi huwa tofauti na nyakati nyingine za kushughulikia mada nyinginezo kama vile sarufi, insha nakadhalika. Hii ni kwa sababu, wakati wa kusoma na kuhakiki kazi fulani

> ya fasihi hususan hadithi, wanafunzi wanachangamka sana, wakasema yaani ukaona kuwa hali siyo ya kawaida. Tunaposoma, wanafunzi huwa makini na watulivu sana. Wanajibu wanapoulizwa na wanatoa maoni wanapoombwa kuyatoa.

Dondoo la hapo juu linatuonesha kuwa ufundishaji wa mada za kisarufi na insha, hutenganishwa na ule wa sarufi. Hata hivyo, walimu wana uhakika kwamba sehemu ya fasihi hususani usomaji na uhakiki wa kazi za fasihi huonesha tofauti kwa sehemu nyinginezo. Tofauti wanayoeleza ni ujengaji wa mazingira na umotishaji wa wanafunzi katika kuzungumza. Jambo lingine muhimu ni uvutiaji ambao unawafanya wanafunzi kutulia na kusikiliza kwa umakini. Utulivu huo si ule wa kawaida bali ni ule unaotokana na mamlaka ya utamu wa kazi za fasihi. Mamlaka hiyo huisukuma hadhira kufuata hatua kwa hatua ili isitolokwe na jambo hata moja katika mtiririko wa visa na matukio vilivyomo katika kazi husika.

Uchambuzi wa data za hapo juu kuhusu utumizi wa fasihi kwa kufundisha stadi za kusikiliza na kuzungumza, ulijikita kuhakiki uwezo wa mwanafunzi wa kukumbuka kile alichokiona au kukisikiliza. Kisha, ulihusisha uwezo huo na kile kilichomo katika kazi za fasihi ambacho humsukuma kukumbuka mifano ya lugha aliyopewa kutoka kazi hizo. Uhakiki huu ni wa kiutambuzi. Aidha, uzungumzaji na usikilizaji unazingatia maingiliano ya watu. Hali hii ilitusukuma kuegemea katika Nadharia ya Maingiliano ya Tamaduni-jamii ili kuchambua mambo yanayozungumziwa katika fasihi yahusuyo kumwunganisha mtu na jamii yake, kisha tuliyahusisha na hali ya ukuzaji wa stadi za kusikiliza na kuzungumza.

### 4.2.3 Ufaafu wa Fasihi katika Utekelezaji wa Mtaala Unaoegemea katika Uwezo

Mtaala unaoegemea katika uwezo unalenga kukuza uwezo wa mwanafunzi kwa kusisitiza kile anachoweza kufanya mwanafunzi kuliko kile anachojua (REB, 2015). Kwa mujibu wa Nzima (2016), mtaala unaoegemea katika uwezo unalenga kumwezesha mwanafunzi kukuza, kuunganisha na kutumia uwezo unaohitajika, kama vile utatuzi wa matatizo, tafakuri tunduizi, ubunifu, teknolojia ya habari, ushirikiano na ujifunzaji usio na mpaka. Katika utafiti huu, tulishughulikia ufaafu wa fasihi katika utekelezaji wa mtaala unaoegemea katika uwezo kupitia ukuzaji wa uwezo wa jumla kama ulivyotajwa na REB (Khj). Uwezo huo ni pamoja na tafakuri tunduizi, utafiti na utatuzi wa matatizo, ubunifu na ugunduzi, stadi za mawasiliano, utawala binafsi, ushirikiano na stadi za maisha, na ujifunzaji usio na mpaka. Katika utathmini wa ufaafu wa fasihi katika utekelezaji wa mtaala unaoegemea katika uwezo, pia

tulishughulikia swala la ujumuishaji wa maswala mtambuka yakiwemo thamani na mwenendo mwema kama baadhi ya vipengele muhimu katika utekelezaji wa mtaala huu.

#### 4.2.3.1 Fasihi katika Ukuzaji wa Tafakuri Tunduizi

Katika karne ya Ishirini na Moja, tafakuri tunduizi inasisitizwa katika mitaala ya elimu ya leo kwa matumaini ya kwamba wanafunzi wakiwa na uwezo huu, basi wanaweza kufanya kazi vizuri katika maisha yao halisi (Braun, 2004 katika Chang na Tung, 2009). Hali hii inatokana na kwamba uwezo wa tafakuri tunduizi huchukuliwa kama upataji wa uamuzi kutokana na kile kinachohitajika (Tosuncuoglu, 2018). Aidha, Huitt (1998) anaeleza kwamba stadi ya tafakuri tunduizi ni kipengele muhimu sana katika elimu ya Karne ya Ishirini na Moja kwani kiwango na matendo yoyote ya binadamu hutambuliwa na fikra zake ambazo ndizo tafakuri tunduizi. Kwa hivyo, tafakuri tunduizi huchukuliwa kama msingi wa uwezo mwingine wowote ule.

Tung na Chang (2009) wanasema kwamba fasihi ni muhimu sana katika ukuzaji wa tafakuri tuduizi. Wataalamu hawawanafafanua sababu za fasihi kuwa msingi na muhimu katika ukuzaji wa tafakuri tunduizi. Wanatoa sababu zifuatazo: mosi, mchakato wa kiakili wa usomaji wa fasihi unahitaji uwezo wa tafakuri tunduizi kwani ni mchakato changamano unaohitaji wasomaji kukumbuka, kurejesha na kutafakari tajriba zao za awali au kumbukumbu ili kujenga maana za matini. Pili, mada, mazingira na lugha ya kazi ya fasihi huwapa wasomaji aina mbalimbali za matukio ya ulimwengu halisi ili kujenga na kuendeleza maana ya kibinafsi na ya kimaisha. Ufundishaji wa lugha kupitia fasihi ndio mahali pazuri pa kuanzia kwa kukuza uwezo wa tafakuri tunduizi (Abida, 2016).

Sababu zinazobainishwa hapo juu, zinathibitishwa na matokeo ya utafiti kutoka ushuhudiaji ambapo wanafunzi na walimu watafitiwa walituonesha kuwa usomaji wa kazi za fasihi huwasaidia kukuza stadi za tafakuri tunduizi kama vile kutoa maelezo na kufafanua maoni na mitazamo ya mwanafunzi juu ya jambo fulani, kuchambua, kutafsiri, kutathmini na kukuza uwezo wa utatuzi wa matatizo.

Katika utafiti uliofanyika, mtafiti alifanyaushuhudiaji katika madarasa yanayosoma na kuhakiki kazi za fasihi. Mtafiti aliona kwamba wanafunzi walishiriki vema sana katika kutoa maoni kuhusiana na kazi zinazoshughulikiwa haswa katika utoaji wa hitimisho au utoaji wa mapendekezo juu ya mwisho wa kazi inayoshughulikiwa, uendelezaji wa visa na matukio, utoaji wa suluhisho za migogoro kati ya wahusika nakadhalika. Hali hii ilikuwa inatofautiana

na hali ya madarasa yaliyokuwa yanashughulikia sarufi na mada nyinginezo bila utumiaji wa fasihi.

Mchango na ufaafu wa fasihi katika ukuzaji wa tafakuri tunduizi unadhihirishwa pia na maoni ya mwalimu C1 kutoka usaili kama yanavyopatikana hapa chini.

> Wakati wa ufundishaji na ujifunzaji wa fasihi wanafunzi wanafikiri zaidi. Mimi nafurahi wakati tunapojifunza hadithi inayoeleweka kwa wanafunzi kwani wanaleta mambo mapya katika mchakato wa ufundishaji na ujifunzaji. Wakati wanapoelewa kazi inayoshughulikiwa wanajibu kila swali linaloulizwa kuhusu kazi hiyo. Wanaweza kutoa utatuzi sahihi wa migogoro kati ya wahusika au kutoa mwisho wenye manufaa kwa jamii nzima.

Dondoo la hapo juu linatuonesha kwamba changamoto inaweza kutokana na uchaguzi wa kazi ifaayo kwa wanafunzi. Hata hivyo, kwa kuegemea katika Nadharia ya Utambuzi na Nadharia ya Maingiliano ya Tamaduni-jamii zilizoongoza utafiti huu, tunaona kwamba utumizi wa kazi yafasihi inayofaa kwa kiwango cha mwanafunzi katika kumfundisha huwa ufunguo wa kutafakari na kujenga mawazo yenye busara na yenye manufaa kwa jamii halisi.

#### 4.2.3.2 Fasihi na Ukuzaji wa Utafiti na Utatuzi wa Matatizo

Shute na wenzake (2016) wanafafanua utatuzi wa matatizo kama ujuzi wa upataji wa kanuni na utumiaji wa kanuni hizo na kuoanisha ujuzi huo na hatua ya utatuzi wa matatizo. Upataji wa kanuni unalinganishwa na hatua ya kuchanganua suluhu zinazopatikana na vikwazo vinavyoweza kujitokeza. Utendaji wa kanuni unahusiana na hatua za kupanga njia ya suluhisho kwa kutumia zana na rasilimali kwa ufanisi na kufuatilia utathmini wa maendeleo ya utatuzi wa tatizo. Uwezo wa utafiti nao unahusu ujuzi wa kukusanya taarifa kuhusu swala au tatizo fulani, kukagua taarifa hizo, kuzichambua na kuzifasili kwa namna ambayo huleta kwenye suluhu. Hivyo basi, uwezo wa utafiti nao unahusu kupata jibu la swali au suluhu la tatizo.

Wanafunzi wanapokuwa na tafakuri tunduizi huwa wajasiri katika kukabiliana na hali mpya au hata kupata masuluhu ya kiubunifu kwa matatizo mapya (Chang, 2009). Wazo hili linathibitisha kwamba mtu anapokuwa na uwezo wa tafakuri tunduizi, basi papo hapo huwa na ule wa utatuzi wa matatizo moja kwa moja.

Hali ya fasihi na ukuzaji wa utafiti na utatuzi wa matatizo inathibitishwa na maelezo ya baadhi ya wanafunzi watafitiwa wetu. Hili ni dondoo kutokamwanafunzi C2.

> Wakati tunaposoma kazi za fasihi mara nyingi tunalenga kuelewa maana ya mtunzi. Hali hii inatusaidia kupata maana yenyewe ambayo mtunzi anataka itufikie kama hadhira yake. Katika mchakato huu, tunajifunza mengi kutokana na kazi yote aghalabu kutokana na wahusika. Kwa mfano: katika hadithi ya Nyambere, tuliona kwamba Mariya alikuwa anamchukia sana nduguye Nyambere. Lakini, Nyambere hakukata tamaa kuandamana na nduguye kwa ajili ya mapenzi aliyokuwa nayo juu ya nduguye. Tuliona kwamba Mariya ndiye alimwokoa katika hatari ya kuliwa na zimwi (mme wake Mariya). Hadithi ilinifanya kupata uelewa wa kwamba "damu nzito kuliko maji." Mimi siwezi kugombana wala kumchukia ndugu yangu. Basi, mimi hata anichukie lakini wakati wote nitamwonyesha kwamba nilisoma hadithi ya Nyambere na Mariya. Kingine ni kwamba yule unayemchukia unaweza kumwomba msaada wa kipekee ambao huwezi kupata mahali pengine. Maisha ni matembezi.

Mawazo ya hapo juu, yanatuonesha sifa ya fasihi ya kujumuisha mifano ya matatizo halisi ambayo inaibua fikra za wanafunzi katika utatuzi wa matatizo wanayoweza kukutana nayo katika maisha yao halisi. Kutokana na hadithi waliyosoma darasani, wanafunzi wa shule C walipata suluhu ya tatizo la ugomvi na chuki miongoni mwa ndugu na hata wanajamii kwa jumla. Suluhisho hilo ni kuepuka kitu chochote kinachoweza kuleta ugomvi au chuki kati yao na ndugu zao au watu wengine. Wakati wanapowachukia, basi wao watavumilia na kuwapenda wale wanaowachukia. Hili ni suluhisho la tatizo linalokabili jamii na familia nyingi duniani. Hivyo basi, wanafunzi wakitekeleza mkakati huu kwa ufanisi, watachangia pakubwa katika kujenga amani, ushikamano na umoja ulimwenguni.

#### 4.2.3.3 Fasihi kama Nyenzo ya Ukuzaji wa Ubunifu na Ugunduzi

Ubunifu na ugunduzi ni mojawapo ya sababu za kibinadamu yaani binadamu anatarajiwa kuwa mbunifu na mgunduzi katika maisha yake yote (Nosratinia & Zaker, 2014 katika Zaker, 2016). Wanadamu wa leo wako katika enzi mpya ambapo mawazo ya ubunifu yanahitajika kwa kiasi kikubwa kuliko enzi zilizopita. Kutokana na data zilizokusanywa kutokana na uchanganuzi wa data, ushuhudiaji na usaili, inaonekana kuwa uwezo wa ubunifu na ugunduzi huweza kukuzwa kupitia fasihi kutokana na utumizi wa mikakati tofauti kama vile kutafakari

juu ya kazi husika ya fasihi, uorodheshaji wa maswali kuhusu kazi husika na ujishughulishaji wa majibu kwa wanafunzi, ubadilishaji wa sifa za kazi na wahusika, maswali ya msomaji, maswali ya mtihani ya wanafunzi, kutayarisha mwisho wa hadithi inayotumiwa, kuisimulia hadithi hiyo kwa upya na kadhalika (Zaker, 2016).

Mwalimu D1 alitoa maoni yake juu ya ukuzaji wa uwezo wa ubunifu na ugundunzi miongoni mwa wanafunzi kupitia fasihi.

> Mara nyingi fasihi simulizi ya Afrika hutumia sungura kama mnyama mwenye ubunifu na ugunduzi sana. Uwezo huu mara nyingi humwokoa mwenyewe katika matanga kadha na kwa wakati mwingine anautumia kuokoa wahusika wengine. Vitendawili na mafumbo pia huwasaidia wanafunzi kuwa wabunifu kutokana na sifa yake ya ufumbuzi. Hali hii huwafundisha kutopata uamzi kiholela holela juu ya swala au tatizo fulani linalotarajiwa kutafutiwa suluhisho katika maisha yao ya kila siku. Kingine ni kwamba kazi hizi huwahamasisha kufikiria mbali kwa kutumia busara katika kuleta kitu kipya kiwe wazo, tendo au kitu kingine cha kugusiwa au kutogusiwa lakini chenye manufaa kwao binafsi na kwa wanajamii kwa jumla.

Dondoo la hapo juu linaonesha kwamba walimu wanaona athari ya fasihi katika ukuzaji wa uwezo wa ubunifu na ugunduzi miongoni mwa wanafunzi. Inaonekana kwamba fasihi inajumuisha mifano ya utatuzi wa matatizo halisi ambayo wanafunzi wanaweza kuiiga na kuitekeleza katika shughuli zao halisi. Hivyo basi, utumizi wa fasihi kama nyenzo ya kufundishia lugha ni njia isiyo ya kutoa tu kanuni mbalimbali za sarufi, sintaksia na fonolojia lakini pia kuboresha ubunifu wa wanafunzi (Elkiliç na wenzake, 2011).

#### 4.2.3.4 Fasihi katika Ukuzaji wa Stadi za Mawasiliano

Stadi za mawasiliano zinahusu uwezo wa mtu kwa kujumuisha na kutumia ujuzi mbalimbali ili kila mtu anayehusika na mawasiliano yake aweze kuelewa. Ujuzi huo wa kujumuishwa ni kama vile kufikiria la kusema, kutafuta njia bora ya kulisema, kutafuta maneno sahihi, kuelewa mtu au watu ambao mnawasiliana na muktadha wa kuwasiliana, kuhakikisha kuwa mtu husika anaelewa na kuzingatia chochote alichokisema hata wakati wa kumjibu (Wambui, 2016). Maana hii inatueleza moja kwa moja kuwa stadi za mawasiliano hazihusu tu kuzungumza wala kuitumia lugha, bali ni zaidi ya hayo. Hii ni kwa sababu mtu anaweza kujua kuitumia lugha hata katika miktadha yote lakini akashindwa kuzingatia washiriki wake wala

kuwashirikisha katika mawasiliano, kuhakikisha kwamba wanamwelewa au akashindwa kuwajibu wakati wanapohitaji majibu. Wakati huu mawasiliano hayafanywi kwa ufanisi kutokana na baadhi ya ujuzi usiojumuishwa wakati wa mawasiliano hayo.

Matokeo ya utafiti wetu yanatuhakikishia kwamba fasihi hujumuisha stadi nyingi za mawasiliano ambazo watu wangeweza kuiga au kutekeleza katika mawasiliano yao ya kila siku. Hali hii inathibitishwa na maoni ya mwanafunzi A2. Alisema:

> Baadhi ya kazi za fasihi zinatufundisha ujuzi tofauti wa kuwasiliana na watu tofauti kulingana na umri wao kama vile wazee, vijana, watoto, wazazi nakadhalika. Pia, zinajumuisha mawasiliano katika miktadha mbalimbali kama vile kanisani, darasani, msibani, nyumbani, mezani nakadhalika. Katika kazi za fasihi, tunaweza kupata mifano ya utumizi wa viungo vya mwili wakati wa mawasiliano kama vile kutikisa kichwa kwa kukataa au kukubali, kufunga macho kwa viganja kwa kuonesha aibu, kutumia vidole kwa kukataa au kukubali, kutumia tamathali za usemi na tanakali za sauti nakadhalika. Nasi tunajaribu kuiga mifano inayotumiwa katika fasihi kwa kujenga mazungumzo yetu katika mawasiliano ya kawaida.

Maoni kutoka baadhi ya watafitiwa kama yanavyobainishwa hapo juu, yanajadili mifano ya ujuzi wa mawasiliano unaoweza kupatikana katika kazi za fasihi. Inaonekana kuwa fasihi hujumuisha mifano ya matumizi ya lugha katika miktadha mbalimbali. Hali hii ni ujuzi muhimu katika lugha kwani watu wengi huweza kuharibu mambo kutokana na matumizi mabaya ya lugha kimuktadha. Hivyo basi, fasihi haizingatii mifano ya miundo ya lugha na vipengele vyake tu bali inazingatia pia matumizi yake kimuktadha. Ujumuishaji wa mifano ya utumizi wa lugha kulingana na miktadha mbalimbali ni jambo muhimu katika umilisi wa stadi za mawasiliano kwani hufanikisha mawasiliano mahsusi. Kwa hivyo, kutokana na fasihi wanafunzi wanaweza kuhamisha ujuzi kutoka kazi za fasihi na kuutekeleza katika mawasiliano yao halisi.

#### 4.2.3.5 Ukuzaji wa Ushirikiano, Utawala Binafsi na Stadi za Maisha Kupitia Fasihi

Uwezo wa ushirikiano, utawala binafsi na stadi za maisha ni muungano wa uwezo mbalimbali. Matos na Afsarmanesh (2008) wanaeleza ushirikiano kama mchakato ambamo viumbe hushirikishana habari, rasilimali na majukumu kwa kupanga jambo fulani, kutekeleza, na kutathmini mpango wa shughuli ili kufikia lengo la pamoja. Stent na Staden (2018)

wanafafanua utawala binafsi kama uwezo muhimu wa kutawala ambao unajumuisha uchukuaji wa majukumu juu ya vitendo na tabia za kibinafsi. Utawala binafsi hurejelea tabia ambayo mtu anapaswa kuwa nayo ili aone mabadiliko yanayotakiwa maishani mwake na sehemu anapofanyia kazi (Alsemgeest na wenzake, 2017 katika Sajeevanie, 2020). Stadi za maisha nazo huweza kuelezwa kama uwezo wa kuwa na tabia nzuri ya kukubali mabadiliko na inayomwezesha mtu kushughulikia mahitaji na changamoto za maisha ya kila siku ipasavyo. Kiukweli, binadamu hawezi kujitegemea kwa kila kitu ila hapaswi kutegemea watu wengine kwa kila kitu. Hii ndiyo maana utawala binafsi ni lazima kwa binadamu yeyote. Stadi za maisha haziwezekani kwa mtu asiye na utawala binafsi.

Mawazo ya Matos na Afsarmanesh (Khj) yanafafanua jinsi ushirikiano unavyojumuisha habari, rasilimali na majukumu ili kufikia lengo sawa kati ya viumbe husika. Maisha hayawezi kufanikishwa bila ushirikiano. Hata hivyo, ushirikiano unawezekana kati ya viumbe vyenye lengo sawa juu ya ushirikiano husika. Mtu asiye na malengo maishani mwake, hana utawala binafsi wala stadi za maisha vilevile.

Jyotsna na Dwarakanath (2018:74) wanapendekeza fasihi kuwa nyenzo ya kukuza stadi za maisha. Kwa kusema:

> The fact is that literature suits the best to inform, persuade, motivate and inspire the young minds which works as a fuel to their passion, work and lives.
>
> Ukweli ni kwamba fasihi inafaa sana kwa kufahamisha, kushawishi, kumotisha na kuvutia akili changa ambazo hufanya kama kichocheo cha hamu, kazi na maisha yao [Tafsiri Yetu].

Kutokana na mawazo ya hapo juu, inaonekana kwamba fasihi inaweza kutumiwa na kuchangia katika kumbadilishia mtu maisha ambayo yalikuwa na ujinga fulani. Hali hii bila shaka, inaandamana na ukuzaji wa stadi za maisha. Dondoo la usaili kutoka walimu watafitiwa wetu nalo linasisitiza kwamba fasihi hufaa kwa kukuza uwezo wa ushirikiano, utawala binafsi na stadi za maisha. Haya ni maoni ya mwalimu B1:

> Fasihi inajumuisha mifano ya kukuza uwezo wa mtu wa kushirikiana na wengine, kuwa na utawala binafsi na kukuza stadi za maisha. Hapa ningependa kutoa mfano wa hadithi ya Nyambere tuliyosoma. Tuliona kwamba Nyambere alikuwa anamchukia sana nduguye Mariya. Lakini

> mama yao alijenga ushirikiano kati yao kisha Mariya akakubali kuongozana naye (huu ni ushirikiano). Nyambere hakutulia alipofika kwa mmewe Mariya ila alikuwa anachunguza kila kitu kinachofanyiwa hapo (huu ni utawala binafsi na stadi za maisha).

Kutokana na dondoo la hapo juu walimu watafitiwa wetu nao wanahakikisha kwamba fasihi inazingatia mifano ya ufundishaji wa kujitegemea katika hali maalum. Pia, inajumuisha mifano ya umuhimu wa ushirikiano ili kuendeleza stadi za maisha kama inavyoelezwa katika dondoo la hapo juu. Hivyo basi, tunaona kwamba matokeo ya data za usaili nayo hayaendi kando na maandiko ya wataalamu yaliopitiwa.

#### 4.2.3.6 Fasihi kama Nyenzo ya Ukuzaji wa Ujifunzaji usio na Mpaka

Ujifunzaji usio na mpaka ni maisha ya kiulimwengu, hiari na motisha ya kibinafsi ya kutafuta maarifa ya maisha halisi na ya kitaaluma (Ates na Alsal, 2012). Uwezo wa ujifunzaji usio na mpaka hauongezei tu ushikamano wa kijamii, uraia hai na maendeleo ya mtu binafsi, lakini pia huongeza uwezo wa kushindania ajira. Hivyo basi, uwezo huu wa ujifunzaji usio na mpaka ni muhimu sana hasa katika Karne ya Ishirini na Moja ambapo ajira imepewa kipaumbele zaidi. Hata katika mitaala ya kielimu katika nchi nyingi za ulimwenguni ikiwemo na Rwanda, husisitiza ukuzaji wa uwezo wa kupata ajira miongoni mwa wanafunzi. Kwa hivyo, uwezo wa ujifunzaji usio na mpaka unapofikiwa kwa ufanisi katika mtaala wa nchi mahsusi, basi hatuna shaka kusema kwamba mtaala huo umefikia malengo yake.

Data zilizokusanywa na utafiti wetu katika ushuhudiaji na usaili, wanafunzi wanatoa maoni yao kuhusu utumizi wa fasihi katika ukuzaji wa ujifunzaji usio na mpaka. Hili ni dondoo la mwanafunzi D2.

> Wakati tunapohakiki kazi za fasihi katika makundi, tunashirikishana mawazo mmoja baada ya mwingine. Kwa hivyo, mwanafunzi huweza kujifunza kutokana na mwenzake. Kuna kazi nyingi za fasihi ambazo huisha mhusika mbaya akikubali makosa yake na kuomba msamaha. Hali hii pia inatufanya kuona kwamba mtu anaweza kujiamini katika mawazo au matendo fulani wakati hayaendani na mahitaji ya jamii, au maisha ya kisasa. Hivyo, kila mtu analazimishwa kujifunza kila wakati.

Dondoo la hapo juu linatuelezea namna ambavyo wanafunzi wanavyoamini kwamba fasihi hujumuisha mifano na mafunzo juu ya ujifunzaji usio na mpaka.

Andrejević na Zecevic (2019: 392) nao wanakubali kwamba fasihi ni nyenzo ya kukuza uwezo wa ujifunzaji usio na mpaka. Wanasema:

> It is known that literature is very important for personal and civic aspects of education, but it should also satisfy the economic one and help students become capable of surviving in the 21st century and eager to be lifelong learners.
>
> Inajulikana kuwa fasihi ni muhimu sana kwa nyanja za kielimu binafsi na za kiraia, lakini inaweza pia kutosheleza uwanja wa kiuchumi na kuwasaidia wanafunzi kuwa na uwezo wa kuishi katika karne ya 21 na kuwa na hamu ya kuwa wajifunzaji wa maisha yote [Tafsiri Yetu].

Mawazo ya Andrejević na Zecevic (Khj) yanafafanua jinsi fasihi hukuza uwezo tofauti katika nyanja kadhaa za maisha ya mwanadamu. Mwishoni mwa wazo, wanaeleza namna ambavyo fasihi inaweza kuwa nyenzo ya kukuza stadi za Karne ya Ishirini na Moja hususan uwezo wa ujifunzaji usio na mpaka. Ukuzaji wa uwezo huu kupitia fasihi, hutokana na kwamba fasihi huwafanya wanafunzi kutumia maarifa yao hasa wakati wa kufanya kazi juu ya fasihi katika makundi, kujadili na kuchambua masuala kwa kutafakari, kuunganisha kazi za fasihi na baadhi ya vipengele vya kimataifa na vya kienyeji vya maisha yao ya kila siku, kutumia teknolojia ya habari kutafiti na kuwasilisha matokeo kwa baadhi ya njia mpya, kukubali na kupata majibu, uamuzi na kukuza haja ya kujitathmini. Hali hii huwafanya wanafunzi kupata maarifa mapya ambayo yanawahamasisha kuwa na hamu ya kujifunza wakati wote.

Walimu watafitiwa nao walitoa mawazo kuhusu jambo hili. Lifuatalo ni dondoo la mwalimu C1.

> Katika kazi nyingi za fasihi tunaona jinsi wahusika wabaya wanavyobadilika wakawa watu wazuri hasa katika tamthilia na michezo ya kuigiza. Huu ni mfano wa ujifunzaji usio na mpaka kwani unamshauri mtu kutosimama kwa mitazamo yake tu yaani anatarajiwa kukubali mabadiliko. Kingine ni kwamba siku hizi kazi nyingi za kifasihi hupatikana mtandaoni kutofautiana na nyakati za awali. Hali hii inawabidi watu kujifunza TEHAMA ili wazipate.

Mawazo ya mwalimu C1 yanaweka wazi mifano iliyomo katika kazi nyingi za fasihi. Yeye ameegemea upande wa wahusika na mabadiliko yao kulingana na hali. Mabadiliko ya

wahusika hutokana na ujifunzaji wao ambao unawasukuma kubadilika. Leo, kasi ya maendeleo na utandawazi wa dunia inatubidi kujifunza kila siku. Mwalimu huyu amedokeza TEHAMA na utandawazi kama sababu kuu za ujifunzaji wa kila wakati. Pia, mtu anapaswa kujifunza kutokana na jambo zuri na hata baya. Ni kweli kujifunza hutokana na kila hali. Mambo mazuri amfundishe mtu kuyatekeleza na kuwafanya watu wengine kuyapenda. Kwa upande mwingine, mambo mabaya yamfundishe mtu kwa kuyachukia, kuyaepuka na kuyachukiza watu wengine. Hivyo basi, si bora kugombana na hali au wakati kwa ajili ya kutokubali mabadiliko kama inavyojadiliwa katika dondoo la mwalimu C1.

Uchambuzi wa data za sehemu yote iliyolenga kutathmini ufaafu wa fasihi katika ukuzaji wa uwezo wa jumla, uliegemea misingi ya nadharia mbili; yaani Nadharia ya Utambuzi na Nadharia ya Maingiliano ya Tamaduni-jamii. Msingi wa Nadharia ya Utambuzi uliosaidia sana ni ule unaodai kwamba mtu ana nafasi na mchango mkubwa wa katika ujifunzaji wake. Misingi ya Nadharia ya Maingiliano ya Tamaduni-jamii iliyosaidia sana ni miwili. Mosi, ni kwamba jamii ni uwanja wa utendaji wa ujuzi wa mwanadamu. Pili, ni kwamba aghalabu mtu anatenda kwa namna fulani kutokana na athari za watu wengine, jamii au mazingira. Kwa kuegemea misingi hii, sehemu hii ilichambua mambo yaliyomo katika fasihi hususan lugha, muundo, wahusika, matumizi ya nafsi na mengineyo. Kisha, iliyahusishamambo hayo na hali ya upanuzi wa fikra za mwanafunzi ili kuyatambua na kuyaelewa. Aidha, sehemu hii ilihusisha hali ya mwanafuzi ya kutumia ubongo zaidi juu ya kazi za fasihi na mahitaji ya mtaala unaoegemea uwezo. Uhakiki huu uliegemea zaidi Nadharia ya Utambuzi.

Kwa upande mwingine, sehemu hii iliegemea Nadharia ya Maingiliano ya Tamaduni-jamii kwa kuchambua yaliyomo katika kazi za fasihi ambayo wakati wote huwakilisha maisha ya jamii na shughuli mbalimbali za watu na kuyahusisha na malengo ya mtaala unaoegemea katika uwezo juu ya ufundishaji na ujifunzaji.

### 4.2.4 Fasihi kama Njia ya Ufafanuzi wa Maswala Mtambuka

Mtaala unaoegemea katika uwezo unasisitiza ujumuishaji na ufundishaji wa maswala mtambuka katika kila somo. Aidha, matokeo ya ushuhudiaji yalionesha kwamba mara nyingi walimu hawafafanui maswala mtambuka katika somo. Ni bora kujadili namna fasihi inavyofaa kufundisha maswala mtambuka.

#### 4.2.4.1 Fasihi na Ujasiriamali

Ujasiriamali katika karne ya ishirini na moja hufungua fursa kwa watu ya kuelewa upya njia za kudhibiti biashara kutoka kwa mtazamo wa kimataifa na jinsi ya kutumia teknolojia ya kisasa yenye manufaa kwa binadamu wa leo (Sampene na wenzake, 2021). Hivyo basi, ujasiriamali unaonekana kuwa na mchango mkubwa katika maisha na maendeleo ya mtu wa kisasa. Utafiti ulikusanya dondoo la mwalimu B1 alipoulizwa ikiwa fasihi inaweza kujumuisha mifano ya kufundisha ujasiriamali miongoni mwa wanafunzi. Anasema:

> Kuna baadhi ya kazi za fasihi zinazotumia lugha au wahusika wanaohusiana na ujasiriamali. Kwa mfano: Riwaya ya *Adili na Nduguze* iliyoandikwa na Shaban (1952) huzungumza biashara na ujasiriamali katika njia tofauti. Kwa njia ya kwanza. Adili na nduguze walikuwa watu wenye hamu ya ujasiriamali. Kuna matumizi ya methali kama "mali bila daftari hupotea bila habari"

Kutokana na dondoo la mwalimu B1, tunaangaziwa juu ya mfano wa riwaya iliyondikwa na Shaban Robert na kuchapishwa mnamo mwaka wa 1952 lakini hadi sasa mifano inaokotolewa na ufafanuzi wa maswala mtambuka kutokana na riwaya hii. Hali hii inatokana na ukweli kwamba jamii ya watu haibadiliki kwa kiasi kikubwa hususan shughuli zao za kimaisha. Aidha, inaonekana kwamba riwaya ya *Adili na Nduguze* ni nyenzo bora ya kufundisha swala la ujasiriamali na kuleta mchango mkubwa katika maendeleo ya mtu wa kisasa na jamii kwa jumla. Hii ni kutokana na mfano uliomo katika riwaya hii ambapo Robert (Khj) alitaka kuwafundisha watu shughuli za kibiashara na ujasiriamali kupitia mhusika wake Adili. Hata methali aliyotumia "*Mali bila daftari hupotea bila habari" i*naweka wazi wazo la kwamba mafanikio ya biashara ni kuhifadhi habari zinazoihusu. Kuhifadhi bora ni kupitia maandishi kwa sababu hayasahuliki. Hata kama imepata hasara lazima ihifadhiwe na sababu zake ili kila wakatiiwe marejeleo ya kuepukana na hasara husika. Hivyo basi, kutokana na mfano huu, itakuwa rahisi sana kufundisha masuala mtambuka yanayohusiana na biashara au ujasiriamali.

#### 4.2.4.2 Fasihi na Usawa wa Jinsia

Usawa wa jinsia unachangia sana katika maisha ya ulimwengu wa kisasa. Joglekar (2013) anaeleza kwamba usawa wa jinsia umesababisha maendeleo katika kila nyanja za maisha. Hii ni kwa sababu majukumu ya mwanamke wa kisasa hayaishii tena kwa kupika, kuosha nguo, kufanya kazi za nyumbani, kutunza watoto. Zaidi ya hayo, mwanamke kama mwanaume hufanya kazi zinazoendeleza jamii, siasa, uchumi, teknolojia, ulimaji, ufugaji na nyanja

nyingine kama anavyoweza kuchangia mwanaume. Dondoo la mwalimu C1 hapo chini ni maoni ya mwalimu C1 alipoulizwa ikiwa fasihi huweza kujumuisha ya usawa wa jinsia.

> Katika tamthilia nyingi tunakuta mambo mengi yanayojadili usawa wa jinsia. Kwa mfano katika tamthilia ya *kilio cha haki* iliyoandikwa na Mazrui mnamo mwaka wa 1981 kuna wahusika wanaobeba usawa wa jinsia. Ila si rahisi mwanafunzi kuelewa mambo hayo kwa ajili ya ujuzi mdogo katika uhakiki.

Dondoo la hapo juu, nalo lilitumia mfano mzuri wa tamthilia inayoweza kumsaidia mwalimu kufafanua swala la usawa wa jinsi na athari zake katika maendeleo ya jamii na dunia kwa ujumla. Kutokana na dondoo la hapo juu, inaonekana kwamba upungufu uko kwa upande wa walimu. Hii ni kwa sababu wao wanaamini kwamba wanafunzi wao hawawana uwezo wa kuelewa maswala mtambuka kupitia fasihi. Hii inatuangazia kwamba walimu hawana uwezo wa kuchagua kazi za fasihi zinazofaa wala hawana mbinu na tekniniki mwafaka za kutumia katika ufafanuzi wa maswala mtambuka kupitia fasihi.

#### 4.2.4.3 Fasihi na Elimu kuhusu Ufahamu wa Jinsia na UKIMWI

Elimu kuhusu ufahamu wa jinsia huhitajika katika enzi hizi kutokana na umuhimu wake wa kusaidia watu kuepukana na magonjwa ya kuambukizwa kama vile UKIMWI FHI 360 (2005). Walimu watafiti walichangia kueleza ikiwa fasihi inaweza kujumuisha swala la mafunzo ya elimu kuhusu ufahamu wa jinsia na UKIMWI. Hapa chini kuna dondoo la mwalimu A1

> Kuna mashairi, misemo, methali nyingi zinazojadili swala la elimu kuhusu ufahamu wa ujinsi na UKIMWI, Nyimbo nyingi za Wanyarwanda wa leo zinazungumza sana swala la ufahamu wa ujinsi na kueleza hasara za udhibiti mbovu wa jinsi kama vile kupata mimba za awali, kuambukizwa UKIMWI, kuzaa watoto wengi pasipo uwezo wa kuwalea ipasavyo na kadhalika.

Kutokana na dondoo la hapo juu, ni dhahiri kwamba fasihi inajumuisha na kutoa mifano ya ufundishaji wa maswala la ufahamu wa jinsia na UKIMWI. Hivyo basi, fasihi inafaa kwa kutumiwa kama nyenzo ya kufundishia swala hili.

#### 4.2.4.4 Fasihi na Elimu kuhusu Utunzi wa Mazingira na Usafishaji

Mkakati wa utunzaji wa mazingira ni mwongozo muhimu katika kuleta maendeleo endelevu na kupunguza umaskini (Assey na wenzake 2007). Mazingira bora na usafi ni mambo muhimu sana katika maisha endelevu ya mtu. Hii ndiyo maana zama za sasa zinasisitiza utunzaji wa mazingira na usafishaji. Matokeo ya utafiti wetu katika mahojiano yalikusanya data zinaeleza namna fasihi inatoa mifano ya utunzi wa mazingira na usafishaji. Mwalimu C1 alisema:

> Kuna kazi za fasihi zinazoeleza swala la utunzi wa mazingira na umuhimu wake. Kwa mfano: riwaya ya *Adili na nduguze* ya Shaban Robert aliyoandika mnamo mwaka wa 1952, hueleza namna makomamanga yalivyokuwa chakula cha Mwelekevu katika mji wa mawe. Riwaya hii inaeleza utunzaji na umuhimu wa madini, miti, maji, mifugo, mimea, jabali na kadhalika.

Dondoo la hapo juu linaonesha kwamba baadhi ya kazi za fasihi hubeba mifano ya swala la utunzi wa mazingira na usafishaji. Katika riwaya iliyotumiwa katika dondoo la hapo juu tunaaelezewa namna mfalme Rai alivyosisitiza utunzi wa mazingira na usafi katika nchi yake. Nchi yake ilifanikiwa kutokana na utunzi wa wanyama na mifugo. Riwaya inaonesha umuhimu wa maji, jabali kama nyumba za wanyama wengine, umuhimu wa miti kama malighafi ya vifaa mbalimbali, umuhimu wa madini kama malighafi ya vitu vya thamani na kadhalika. Hivyo basi, riwaya hii inaweza kusaidia kufafanua swala la utunzi wa mazingira na usafishaji kwa wanafunzi husika.

Madondoo ya hapo juu, yote yanatuangazia kwamba walimu wanakubaliana juu ya mifano inayopatikana katika fasihi kuhusu maswala mtambuka. Kitu kingine ni kwamba madondoo haya yanathibitisha jambo la kwamba fasihi inazingatia mifano mbalimbali ya maswala mtambuka. Kuhusu thamani na mwenendo mwema, tuliona kwamba fasihi yoyote inajadili utamaduni wa wanajamii fulani. Utamaduni huo unazingatia thamani zao na kuwaeleza njia bora za kurekebisha tabia zinazokiuka kanuni za utamaduni wa jamii husika ili kuwapo kwa maadili na mwenendo mwema kwa kila mwanajamii.

#### 4.2.4.5 Fasihi na Thamani na Mitazamo

Kila fasihi hujadili utamaduni na thamani za jamii husika. Ikumbukwe kwamba kila utamaduni ni mzuri na bora kwa jamii yake. Hivyo basi, agahalabu kazi za fasihi hutungwa

kwa ajili ya marekebisho fulani ya kitamaduni kwa watu fulani juu ya mitazamo na thamani za wanajamii. Katika mahojiano, walimu walieleza kwamba kazi nyingi za fasihi huweza kubeba mifano ya thamani na mitazamo ya watu. Mwalimu B1 anasema:

> Nyimbo nyingi za Wanyarwanda zinazungumza sana swala la thamani za Wanyarwanda na mitazamo yao. Mara nyingi hueleza tabia na mwenendo mwema ambavyo humpambanua na watu wa nchi nyingine.

Dondoo la hapo juu hutuangazia ufaafu wa fasihi katika ufundishaji wa thamani na mitazamo ya watu. Utumizi wa fasihi huweza kumsaidia mwanafunzi kurekebisha na kuepukana tabia mbaya ambazo huweza kumkabili kama vile matumizi ya dawa za kulevya. Hii ni kwa sababu hali fasihi inamwezesha kuelewa kwamba matumizi ya dawa hizo hutofautiana na thamani ya Mnyarwanda. Jambo lingine ni kwamba fasihi humwezesha mwanafunzi kupata mtazamo fulani katika uamzi juu ya jambo maalum kama vile mtazamo wa kuepukana na vileo kama njia ya maendelo, uraia na uzalendo.

## 4.3 Namna ya Kuitumia Fasihi Kufundishia Lugha katika Muktadha wa Mtaala Unaoegemea katik Uwezo

Kutokana na wazo la kwamba fasihi hubeba mifano ya kufundishia lugha na kutekeleza mtaala unaoegemea katika uwezo, inaonekana kuwa bora kubainisha namna fasihi huweza kutumiwa katika ufundishaji wa lugha ya poli katika mazingira ya mtaala unaoegemea katika uwezo. Hivyo basi, ni bora kujadili namna fasihi inavyoweza kutumika kufundisha vipengele na stadi za lugha, kukuza uwezo wa jumla, kufundisha maswala mtambuka na namna ya kuitumia kufundisha mitazamo na thamani miongoni mwa wanafunzi husika.

### 4.3.1 Utumizi wa Fasihi katika Ufundishaji wa Sarufi

Utumizi wa fasihi katika ufundishaji wa lugha ya pili ulikuwa mkakati mwafaka katika kipindi cha umaarufu wa Mbinu ya Tafsiri Sarufi (Elkiliç na wenzake, 2011). Wakati huu, utumizi wa fasihi katika madarasa ya lugha ulisaidia wanafunzi wa lugha kujifunza lugha lengwa kupitia tafsiri ya sentensi kutoka lugha lengwa kwenda lugha ya kwanza na kutoka lugha ya kwanza kwenda lugha lengwa. Kutokana na fasihi, wanafunzi walipata nafasi ya kufanya mazoezi kuhusu kanuni za sarufi kuhusu lugha lengwa (Hall, 2005). Walimu wa lugha walitarajia wanafunzi wasome na kutafsiri matini za kifasihi kwani matini hizi zilidhaniwa kuwakilisha mifano ya uandishi mzuri na vielelezo vya kanuni za kisarufi za lugha (Duff & Maley, 1990 katika Elkiliçna wenzake, 2011).

Mbinu za zama hizi nazo zinahitaji kutumia fasihi katika ufundishaji wa lugha hususan ufundishaji wa sarufi. Hii hasa inatokana na sifa, malengo na mahitaji ya mtaala unaoegemea katika uwezo ambao unatumiwa enzi hizi. Sifa, malengo na mahitaji hayo, yanatoa fursa za utumizi wa fasihi zaidi katika ufundishaji wa lugha hususan sarufi kama ilivyodhihilika katika 4.1.2.1.

Katika utumizi wa fasihi kwa kufundishia sarufi, mwalimu wa lugha anapaswa kuzingatia sarufi na miundo ya lugha inayotumiwa na mwandishi. Hatimaye, anapaswa kuwahimiza wanafunzi kutafuta maoni ya ubunifu na kuwaalika kurekebisha, kupanua au kuongeza kwa maandishi kwa kuzingatia mifano ya kisarufi iliyotolewa katika kazi husika (Elkiliç na wenzake, Whj).

Data za utafiti zinaonesha kwamba wanafunzi nao wanapendekeza hatua bora kwao katika utumizi wa fasihi kwa kuwafundisha sarufi ya lugha lengwa. Mwanafunzi A2 anatoa maoni yake juu ya mjadala huu.

> Kutokana na andalio lake la somo kuhusu fasihi, mwalimu anaweza kuchagua kazi ya fasihi inayojumuisha mifano ya kisarufi anayotarajia kufundisha siku hiyo. Baada ya kutoa mifano hiyo, anaweza kuomba wanafunzi kuiiga ili kujenga sentensi na vifungu vyao. Kwa mfano, katika hadithi ya Nyambere ambayo tulijifunza jana, kuna sentensi inayosema *“Hapo zamani za kale palikuwa mwanamke <u>mmoja</u> ambaye alizaa watoto wa kike <u>wawili.</u>”* Maneno kama mmoja na wawili ni vivumishi vya idadi. Kwa hivyo, mfano uliopo katika hadiithi ya Nyambere inaweza kumsaidia mwalimu kufundisha matumizi ya vivumishi vya idadi.

Mfano wa sentensi iliyotolewa na mwanafunzi A2, inapatikana katika hadithi fupi simulizi iitwayo “Nyambere” ambayo inapatikana katika kitabu cha mwanafunzi wa kidato cha tano, mchepuo wa Kiswahili. Kutokana na mfano wa hapo juu, tunaona kwamba mwalimu anaweza kuutumia mfano huo kufundisha vipengele mbalimbali vya lugha kama vile muundo wa sentensi, vivumishi vya idadi, hesabu, msamiati nakadhalika.

### 4.3.2 Fasihi kama Nyenzo ya Kufundishia Msamiati

Kwa kuegemea kazi fulani ya fasihi, wanafunzi wanaweza kufundishwa mikakati ya kutambua msamiati muhimu kwao na kujifunza matumizi ya msamiati huo katika miktadha tofauti kulingana na fasihi inayoshughulikiwa (Dole na Trathen, 1995). Utaratibu na ujuzi huu

wa masharti kuhusu uchaguzi wa maneno muhimu na uamzi wa matumizi yake, humsaidia mwanafunzi kupata uelewa zaidi juu ya kazi za kifasihi.

Walimu na wanafunzi watafitiwa wa utafiti wetu nao wanatoa maoni yao juu ya utumizi wa fasihi kwa kufundishia msamiati. Wanaonesha jinsi fasihi inavyoweza kuchangia katika ufundishaji wa kipengele hiki miongoni mwa wanafunzi husika. Haya ni maoni ya mwanafunzi B2.

> Mwalimu anapoleta msamiati mmoja kila siku kutoka kichwa chake, hatuwezi kuendelea wala kukuza uwezo wetu wa kuzungumza kwa sababu mazungumzo yoyote yale hutumia msamiati kuliko sehemu nyingine zozote za lugha. Mwalimu pia hawezi kutufundisha kamusi hata nasi hatuvutiwi na kamusi kutokana na orodha ya maneno mengi yaliyomo. Hivyo basi, ni bora mwalimu atumie kazi ya fasihi ili tuvutiwe na kusoma. Tukivutiwa na kusoma, tutakuwa na hamu ya kutafuta msamiati unaotusumbua ili kuelewa maana nzima ya kazi ambayo tunasoma.

Kutokana na dondoo la hapo juu inaonekana kwamba wanafunzi wanajua kipengele cha msamiati ni muhimu sana hasa katika umilisi wa mawasiliano. Pia, inaonekana kuwa wanahakikisha mchango wa fasihi katika ufundishaji wa msamiati kwa kuilinganisha na kamusi. Kwao wanaona kamusi haiwavutii kama kazi ya fasihi. Hii ni kutokana na ukweli kwamba kamusi inajumuisha orodha ya maneno tu bila wahusika wala masimulizi ya kuchekesha na kuvutia.

Walimu nao wanaeleza jinsi wanavyofundisha msamiati kupitia fasihi. Hapa chini tunalo dondoo la mwalimu C1. Anasema:

> Wakati wa kufundisha msamiati kupitia fasihi, ni bora tusome kazi fulani kisha wanafunzi watumie kamusi kwa kutafuta maana ya msamiati ambao unawasumbua wanafunzi ili waelewe kazi hiyo. Ni bora mwalimu aombe wanafunzi kubuni kazi zao kwa kutumia baadhi ya msamiati wa kazi iliyosomwa na kuziwasilisha mbele ya darasa lote. Hali hii inawabidi wanafunzi kujitafutia msamiati mwingine ili waweze kuwa na kazi ya kuvutia na kupendeza hadhira yao. Wakati huu, mwanafunzi atawajibika kuvumbua msamiati mpya na wenzake wakafaidika kutokana na msamiati anaoleta darasani.

Dondoo la hapo juu linaonesha kwamba fasihi inawasaidia walimu kujenga mazingira ya utumizi wa msamiati uliomo katika kazi husika ya fasihi. Hata hivyo, kutokana na dondoo hili pamoja na data za ushuhudiaji, inaonekana kwamba walimu hufundisha kama somo linalojitegemea wala si kama nyenzo ya kufundishia msamiati. Hivyo basi, ufafanuzi wa maneno unaofanywa unalenga kuielewa kazi inayoshughulikiwa na siyo kujifunza msamiati unaotarajiwa. Aidha, fasihi ingetumiwa kama nyenzo ya kufundishia msamiati basi, mwalimu na wanafunzi wangekuwa na aina ya msamiati wanaotarajia kushughulikia kisha wakachagua kazi ya fasihi inayojumuisha mifano ya utumizi wa msamiati husika. Wakati huu, msamiati uliotajwa na wanafunzi wenyewe na kutamani kuufahamu, huwa rahisi kuelewa maana na matumizi yake kupitia mifano inayotolewa katika kazi ya fasihi. Hivyo basi, ni bora kumpa mwanafunzi fursa ya kupendekeza aina ya msamiati anaohitaji kujifunza. Hii ni kwa sababu katika Karne ya Ishirini na Moja, watu hujifunza lugha kwa madhumuni ya kufanikisha shughuli zao. Hii ndiyo maana mwanafunzi anapojifunza msamiati anaotaka kujifunza humfanya kuuelewa na kuutumia sana.

### 4.3.3 Jinsi ya Kuitumia Fasihi katika Ufundishaji wa Stadi za Lugha

Usomaji na uhakiki wa kazi za fasihi huwa na umuhimu mkubwa katika ufundishaji wa stadi za kuzungumza, kusikiliza, kusoma, na kuandika. Kwa kawaida, walimu wa lugha hufundisha kila ustadi kipwekepweke. Hapa inashauriwa kwambani bora kuzingatiwa kuwa inapotumiwa fasihi wakati wa ufundishijaji wa lugha yoyote ile, stadi nne (kuzungumza, kusikiliza, kusoma, na kuandika) zifundishwe kwa pamoja yaani pasipo kutenganishwa. Hata hivyo, wanafunzi na walimu wa lugha wanapaswa kuzingatia stadi hizi nne kama sehemu muhimu ya matumizi ya lugha ya mazungumzo na maandishi (Babaee na Yahya, 2014). Katika tasnifu hii kuna haja ya kujadili nafasi ya fasihi katika ufundishaji na ukuzaji wa stadi nne za lugha kama zilivyobainishwa hapo juu.

Babaee na Yahya (2014:82) wanatoa maoni yao kuhusu jinsi ambavyo walimu wangetumia fasihi katika ufundishaji na ujifunzaji wa stadi nne za lugha. Wanasema:

> Language instructors should choose a student-based and dynamic method towards understanding of literary texts. In reading classes, discussions can begin literally by asking questions about setting, characters, and plot of selected texts. When learners have literal understanding, then they can go to the inferential level in which they should have some investigations and interpretations of the characters, settings, and themes as well as the author’s

> view point. After understanding a literary text both literally and inferentially, learners should be ready for a group work in which they can share their assessments of the work. The individual evaluation motivates the learners to activate their imagination about the work and even find some solutions to their problems.
>
> Walimu wa lugha wanapaswa kuchagua mbinu inayomwegemea mwanafunzi na inayobadilika kuelekea uelewa wa matini za kifasihi. Katika madarasa ya kusoma, majadiliano yanaweza kuanza kisahili kwa kuuliza maswali kuhusu mandhari, wahusika, na muundo wa maandishi yaliyochaguliwa. Wanafunzi wanapokuwa na uelewa wa kisahili, basi wanaweza kwenda kwenye kiwango cha kufikiria zaidi juu ya kazi husika ambapo inapaswa kuwa na uchunguzi na tafsiri fulani za wahusika, mazingira, mandhari, dhamira pamoja na nafsi ya mwandishi. Baada ya kuelewa matini ya kisahili na kwa kifikra, wanafunzi wanapaswa kuwa tayari juu ya kazi ya makundi ambamo wanaweza kushirikisha tathmini zao za kazi. Tathmini ya kibinafsi huhamasisha wanafunzi kuamsha mawazo yao kuhusu kazi na hata kutafuta baadhi ya masuluhu kwa matatizo yao [Tafsiri Yetu].

Maoni ya Babaee na Yahya (Whj) yalijaribu kufafanua mchakato wa kufundisha stadi zote nne kwa wakati mmoja kupitia fasihi. (Ongeza maelezo kidogo hapa).

Matokeo ya data za ushuhudiaji zilizokusanywa na utafiti wetu zinaonesha kwamba ni walimu wachache ambao wanafundisha stadi nne kwa wakati mmoja. Muhtasari wa Kiswahili kuhusu ufundishaji wa stadi nne za lugha nao unakubali kwamba stadi hizi zifundishwe kwa pamoja. Hata hivyo, ilibainika kwamba walimu wengi hawafuati moja kwa moja maelezo ya muhtasari huu kuhusu ufundishaji wa stadi nne za lugha. Huu ni mfano kutoka data za ushuhudiaji; katika dakika 40 za ushuhudiaji darasani, mwalimu A1 alifundisha stadi za kusikiliza na kuzungumza tu. Mwalimu B1 alifundisha stadi za kusoma na kuzungumza tu. Mwalimu C1 ndiye alifundisha stadi nne yaani stadi za kusoma, kusikiliza, kuandika na kuzungumza. Mwalimu D1 alifundisha stadi za kusoma na kuzungumza tu. Hali hii inatuonesha kwamba walimu hawafundishi stadi zote za lugha kwa pamoja. Hata hivyo, fasihi ikitumiwa ipasavyo inaweza kufanikisha ufundishaji wa stadi nne za lugha kwa ufanisi. Kwa kuegemea data zilizokusanywa pamoja na Nadharia ya Utambuzi na Maingiliano ya Tamaduni-jamii, tunaenda kueleza namna ya kufundisha kila stadi katika kipindi cha somo kimoja.

#### 4.3.3.1 Utumizi wa Fasihi katika Ufundishaji wa Stadi ya Kuandika

Frank (1995) kama anavyonukuliwa na Ismailna na Sharan (2020) anaeleza kuwa fasihi ndiyo nyenzo bora ya kuwasaidia wanafunzi kuzalisha maandishi yenye ubunifu. Kulingana na Frank (khj) fasihi ni kichocheo bora na uhamasishaji wa kutawala ujuzi wa kuandika kwa wanafunzi. Aidha, wataalamu hawa wanashauri walimu wa lugha kuchukua fasihi kama kiunzi cha kuunganisha wanafunzi na maandishi. Haya ni maoni ya Ismail na Sharan (2020: 277) yanahusu kueleza nafasi ya mwalimu katika utumizi wa fasihi kwa kufundishia stadi za kuandika. Wanasema:

> The teacher should understand students' interest in their favorite type of literature and recommend them some extra material to read at home. Moreover, the teacher should link reading literature material by gaining extra marks on their exams. If teachers invest enough time and energy, they will lead students to produce better writing texts and create creative writers.

> Mwalimu anapaswa kuzingatia faida za wanafunzi kutokana na aina za kazi za fasihi wanazopenda. Kisha wapendekeze nyenzo za ziada za kusomea nyumbani. Aidha, mwalimu angepaswa kuunganisha nyenzo za kusoma fasihi kwa kuwapatia wanafunzi alama za ziada kwenye mitihani yao. Ikiwa walimu watawekeza muda na nguvu za kutosha katika jambo hili, watawaelekeza wanafunzi kutoa maandishi bora na kuwa waandishi wabunifu [Tafsiri Yetu].

Kutokana na mawazo ya hapo juu, inaonekana kwamba mwalimu huwa na nafasi kubwa katika ukuzaji wa mwanafunzi wa stadi za kuandika. Hii ni kwa sababu anatarajiwa kuelewa na kuzingatia aina na kazi za fasihi zinazowafurahisha na kuwavutia wanafunzi wao. Kisha, wazitumie kwa kuwajengea kazi za ujifunzaji. Elhabiri (2013) anaongeza katika mawazo ya Ismail na Sharan (whj) kwa kusema kuwa katika mchakato wa kufundisha stadi za kuandika kupitia fasihi, mwalimu anapaswa kuwaandalia na kuwapatia wanafunzi kazi za kuandika baada ya kusoma kazi fulani ya fasihi. Hali hii huwasaidia kuboresha baadhi ya uwezo wa lugha katika insha zao za uandishi, kuelewa yaliyomo katika kazi husika na kupata maarifa fulani ya kiisimu.

Kutokana na data za usaili, wanafunzi nao wanapendekeza njia inayoweza kuwafaa katika ufundishaji wao. Mwanafunzi C2 anasema:

> Ni bora mwalimu atusomee kwa mara ya kwanza nasi tumtegee masikio kwa kufanya uchambuzi wa maana iliyomo. Kisha, mwalimu atuongoze kuelewa maana ya maneno ambayo hatuyaelewi. Ni bora zaidi kila mwanafunzi atengeneze maandishi yake ya muhtasari unaozingatia yale aliyosikia kutoka katika habari iliyosomwa.

Kutokana na mawazo ya wanafunzi kama yanavyoonekana hapo juu, si vizuri mwalimu kuwapa wanafunzi majukumu yote na kubaki bila jukumu. Hii ina maana ya kwamba katika mchakato wa ufundishaji na ujifunzaji, mwalimu ana majukumu yake ambayo hutofautiana na yale ya mwanafunzi. Hivyo basi, wakati wa ufundishaji wa lugha kwa kutumia fasihi, mwalimu anatarajiwa kuwapa wanafunzi mfano wa kusoma kabla ya kuwaomba kusoma. Hali hii inakuza uwezo wa wanafunzi wa kusikiliza. Kingine ni kwamba bila mfano, mwanafunzi anaweza kufanya makosa mengi wakati wa kusoma na mwalimu hawezi kukosoakosoa kila kosa lifanywalo na mwanafunzi wakati wa kusoma. Hata hivyo, mwanafunzi anapofanya makosa ya usomaji bila kukosolewa, wanafunzi wengine watasikiliza na kuzingatia tahajia zisizo sahihi.

#### 4.3.3.2 Namna ya Ufundishaji wa Stadi ya Kusoma Kupitia Fasihi

Ujuzi wa kusoma ni mojawapo ya stadi muhimu zaidi kwa maendeleo ya wanafunzi kitaaluma, kufaulu na maendeleo katika taaluma zao za sasa na zijazo (Carrell ,1988 katika Mussa, 2020). Ili kufanya usomaji uwe wa kufurahisha na wenye manufaa zaidi, hatua tatu zifuatazo zinapaswa kufuatiliwa wakati wa uchaguzi uandalizi wa kazi ya kusoma. Mosi, usomaji wa kabla. Pili, ni usomaji wa wakati wa kusoma. Tatu ni usomaji wa baada ya kusoma (Harmer, 1998 na Lazar, 1993 katika Mussa, 2020). Aidha, mwalimu anatarajiwa kufanya uchunguzi na uchambuzi wa kazi inayoenda kutumiwa hasa kwa kujikita zaidi kwenye kiwango cha lugha cha wanafunzi, faida za kitaaluma za wanafunzi, fasihi na utamaduni wa wanafunzi (Lazar, 1993 katika Mussa, Khj),

Data za usaili zilitupatia maoni ya wanafunzi juu ya jinsi fasihi inavyofundishwa na jinsi ambavyo ingefundishwa. Hapa chini kuna mapendekezo ya mwanafunzi B2.

> Wakati wa kujifunza kazi fulani ya fasihi, mwalimu anatusomea kwa mara ya kwanza halafu anaomba mwanafunzi mmoja akasome kwa sauti baada ya mwingine. Kutoka wakati huo kila mwanafunzi anapata hiari na motisha ya kusoma kazi husika kwa ubinafsi wake. Ni bora mwalimu

atupe muda zaidi wa kusoama kwani wengi hatujajua kusoma Kiswahili kwa usahihi.

Dondoo hili linatuonesha kwamba wanafunzi wanakubaliana na wazo la kwamba fasihi huweza kuwa nyenzo mwafaka ya kufundishia ustadi wa kusoma. (Ongeza maelezo kidogo)

Meyer na Wardrop (1994) katika Amer (2012) wanaeleza kwamba kusoma kwa sauti kwa wanafunzi huwaandaa na kuwajengea msingi wa kujifunza kusoma. Hali hii inakuza uwezo wao wa kutumia mdomo katika utendaji wa lugha ambao unaathiri ustadi wao wa kusoma. Hali hii pia hukuza usuli wao wa maarifa, huwasaidia kufichua maana mpya za maneno na kuwakuzia ujifunzaji wa kimakusudi.

Maoni ya Meyer na Wardrop (khj) yanatuanganzia kwamba mwalimu akiwasomea wanafunzi kwa sauti, kisha nao wakapewa nafasi ya kusoma mmojammoja, wataiga mfano wake katika usomaji. Hali hii inatuonesha kwamba uwezo wa mwanafunzi wa kusoma, aghalabu hutokana na athari za mwalimu wake.

Maoni ya Babaee na Yahya (khj) na Meyer na Wardrop (1994) yanashabihiana na yale ya watafitiwa ambayo yanakubali kwamba utumizi wa kazi za fasihi huwamotisha kusoma na kukuza uwezo wao wa kusoma. Wanafunzi wanaona kwamba mwalimu akiwa na kazi za fasihi anapaswa kuchagua kazi inayofaa kwa kiwango cha wanafunzi husika. Wakati wa kujifunza kazi fulani ya fasihi, mwalimu anaweza kuwasomea wanafunzi kwa mara ya kwanza baada ya kuwasomea, akawaomba kusoma mmojammoja. Ni bora mwalimu awape wanafunzi nafasi na uhuru wa kusoma mara nyingi, kuwapa kazi za darasani na za nyumbani zinazohusu kusoma hadithi nyingi ili mwanafunzi azowee tabia ya kusoma.

#### 4.3.3.3 Jinsi ya Kuitumia Fasihi kama Nyenzo ya Ufundishaji wa Stadi za Kusikiliza na Kuzungumza

Katika maisha yetu ya kila siku, wengi huzungumza zaidi ya wanavyoandika. Hali hii inazifanya stadi za kuzungumza na kusikiliza kuwa utendaji wa lugha (Karim, 2020). Hivyo basi, haina budi kusemwa kwamba katika karne ya Ishirini na Moja stadi hizi ndizo malengo makuu ya ujifunzaji wa lugha yoyote ile. Karim (Khj) anasema kwamba ufundishaji wa stadi za kuzungumza na kusikiliza ni changamoto kubwa inayohitaji ufundi wa hali ya juu. Hali hii inatokana na kwamba wanafunzi wote huhitaji kuwa wazuri katika usikilizaji na uzungumzaji wa lugha lengwa. Kingine ni kwamba kila mwanafunzi hatosheki na kiwango chake cha uzungumzaji na usikilizaji wa lugha lengwa, yaani anahitaji maendeleo zaidi. Hali hii

inawabidi walimu wa lugha ya pili kuwa wabunifu na watafiti wa kiisimu ili waweze kubunina kutumia mikabala, mbinu, na mikakati tofauti ili kuwafikisha wanafunzi kwenye malengo ya ujifunzaji wa lugha lengwa.

Katika mchakato wa ufundishaji wa stadi za kusikiliza na kuzungumza, utoaji wa viwango tofauti vya kimaana vya matini za kifasihi kunatoa fursa za kukuza stadi za kuunda maana na kufasili ambazo wanafunzi wanahitaji. Hali hii huwasaidia wanafunzi kuelewa kila aina ya nyenzo za uwakilishi katika lugha, kufahamu zaidi lugha lengwa, kukuza ujuzi na mikakati wanayoweza kutumia katika hali na miktadha mingi tofauti, kuongezeka faida zao na motisha ya kimazungumzo, na kufanya ujifunzaji wa lugha kuwa uzoefu wa kufurahisha na kuwafaa zaidi (Daskalovska na Dimova, 2012).

Data za usaili na ushuhudiaji zilituonesha kwamba ufundishaji wa stadi za kuzungumza na kusikiliza Kiswahili huhitaji nguvu na marekebisho zaidi miongoni mwa walimu na wanafunzi wa Kiswahili. Hii ni kwa sababu walimu wengi huonesha ulegevu na kutokuwa na mikakati sahihi ya kuboresha na kuendeleza ujuzi wa kuzungumza na kusikiliza miongoni mwa wanafunzi. Hapa chini, utafiti ulipata maoni ya walimu A1 kuhusu namna wanavyofundisha stadi hizi.

> Wanafunzi wana shida sawa ya kunyamanza wakati wa somo la Kiswahili. Tunaona kwamba tatizo walilo nalo ni uoga kwa sababu wanafunzi wengine mara nyingi humcheka mwenzao anaposema lugha yenye makosa. Hivyo, anaogopa kusema ili asichekwe. Tunajaribu kuwaadhibu wanafunzi wanaowacheka wenzao lakini tatizo halitoeki. Tunawaonya wanafunzi wote kutumia lugha waliyo nayo licha ya upungufu wake lakini hawakubali.

Maoni ya mwalimu A1 yalisisitiza swala la uoga miongoni mwa wanafunzikama lilivyobainika hata wakati wa ushuhudiaji. Walimu wanafafanua kwamba tatizo hili linatokana na misingi au usuli wa elimu yao ambayo iliwasisitizia kusema wakiwa na uhakika wa kwamba wanachoenda kusema ni sahihi. Usuli huu ndio unawafanya kuchekana kati yao. Ili kuondoa tatizo hili, mwalimu anashauriwa kutumia kazi za fasihi zenye wahusika ambao wanakubali kujifunza bila kujali vicheko vya watu wengine. Ni bora mhusika huyu afikie malengo yake na avune matunda matamu kutokana na ujuzi aliookota. Kwa upande mwingine, ni bora wale waliomcheka wajute na kumwomba msamaha na ushauri ili nao wafuate mikakati yake wapate yale aliyojifunza wakati walipokuwa wanamcheka. Kingine,

shughuli za kusoma kwa sauti, uigizaji, michezo ya kuigiza, majadiliano, na shughuli za vikundi ni njia mwafaka za kupitia ili walimu wa lugha waboreshe usikilizaji na uzungumzaji wa wanafunzi (Babaee na Yahya, 2014).

Hata hivyo, data za ushuhudiaji na usaili zilituonesha kwamba kuna pengo kubwa kutoka kwa walimu kuhusu ushirikishaji na utumizi wa mikakatiinayokuza uwezo wa kuzungumza miongoni mwa wanafunzi. Hapa chini kuna dondoo la walimu kutoka mwalimu B1 kuhusu jinsi wanavyowasaidia wanafunzi kukuza uwezo wao wa kusikiliza na kuzungumza wakati wa ufundishaji na ujifunzaji wa fasihi.

> Mara nyingi wanafuata na kusikiliza kwa makini wakati tunaposoma hadithi darasani kwa sababu wanakuwa wakisubiri maendeleo au mwisho wa hadithi na suluhu kati ya migogoro iliopo miongoni mwa wahusika. Hata hivyo, tatizo kubwa tulilo nalo ni kimya chao wakati ninapowaomba kuzungumza. Hali hii inanifanya kutumia amri kwa mwanafunzi fulani lakini kwa bahati mbaya anaweza kumaliza kama dakika kumi bila kusema chochote. Kwa hivyo, mimi nilipata uamzi wa kutowauliza kwani naweza kushindwa kumaliza mambo ambayo natarajia kufundisha.

Maoni ya mwalimu wa hapo juu, yanatuonesha kwamba walimu hufundisha kwa lengo la kumaliza somo na siyo kukuza uwezo wa mwanafunzi. Aidha, walimu wanalazimisha wanafunzi kuzungumza wakati hawajajenga fursa na mifano inayowahimiza kuzungumza. Kwa mfano: mwalimu anawasomea wanafunzi hadithi na anawaomba kutoa maoni juu ya kitu ambacho hawajawasaidia kuelewa wala kuwapa fursa ya kushirikishana mawazo kupitia makundi ili wapate cha kusema. Hivyo basi, tuliangaaziwa kwamba walimu wangali na ujuzi mdogo wa kukuza umilisi wa kuzungumza na kusikiliza kupitia fasihi.

Wanafunzi nao walitoa maoni kuhusu namna fasihi ingepaswa kutumiwa kwa kuwafundishia na kuwakuzia stadi za kuzungumza na kusikiliza. Mwafunzi B2 anasema:

> Mwalimu atusomee hadithi nyingi darasani. Anapotusomea kwa mara ya kwanza nasi tunajisomea wenyewe. Akimaliza kutusomea atuweke katika makundi ili tujadiliane na tufanye mihtasari ya mambo tuliyosikiliza kutoka katika hadithi hiyo. Hapa, ni bora tujadiliane katika makundi lakini kila mwanafunzi aandike muhtasari wake binafsi. Baada ya kuwa na muhtasari wa hadithi kwa kila mtu, mwalimu atupe nafasi ya kuwasilisha yale tuliyoaandika. Baada ya mwanafunzi kuwasilisha kazi yake, ni bora apate

wakati wa kujadiliana na darasa zima kwa kujitahidi kujibu maswali yote anayoulizwa kuhusiana na wasilisho lake. Wakati huu mwanafunzi atakuwa anatenda lugha na kujizoesha kuzungumza mbele ya watu wengine bila uoga.

Kutokana na maoni ya mwanafunzi wa hapo juu, tunapata picha ya namna gani wanafunzi wanahitaji kufundishwa lugha hasa stadi za kusikiliza na kuzungumza. Kwa maoni yetu, hatuoni hasara ya kutekeleza mchakato ulioelezwa na mwanafunzi huyu. Hii ni kwa sababu hatuna shaka kwamba mchakato huu ukitekelezwa hatua kwa hatua unaweza kuzaa matunda katika ukuzaji wa mawasiliano miongoni mwa wanafunzi kwa kutumia lugha lengwa.

### 4.3.4 Namna ya Ukuzaji wa Uwezo wa Jumla Kupitia Fasihi

Kuna haja ya kubainisha namna fasihi inavyoweza kutumika katika ukuzaji wa uwezo wa jumla. Ukuzaji wa uwezo huo huelekeza moja kwa moja kwenye utekelezaji wa mtaala unaoegemea katika uwezo. Uwezo huo unaotarajiwa kukuzwa ni pamoja na tafakuri tunduizi, utafiti na utatuzi wa matatizo, ubunifu na ugunduzi, stadi za mawasiliano, ushirikiano, utawala binafsi na stadi za maisha na ujifunzaji usio na mpaka (REB, 2015). Kila uwezo ulijadiliwa kwa kubainisha namna ya kuukuza kupitia fasihi miongoni mwa wanafunzi husika.

#### 4.3.4.1 Jinsi ya Kuitumia Fasihi Kukuza Tafakuri Tunduizi.

Tafakuri tunduizi haipaswi kutenganishwa na somo linalofundishwa darasani. Inapaswa kutathminiwa kama mada nyingine za somo (Chang, 2009). Chang (Khj) anapendekeza njia tatu za kukuza tafakuri tunduizi miongoni mwa wanafunzi kama zifuatazo: Kwanza, muda zaidi unapaswa kutengwa kwa ajili ya wanafunzi ili kujibu maswali yaliyowekewa alama na mwalimu katika karatasi zao za kumbukumbu. Karatasi ya majibu inaweza kuundwa na kuambatishwa ili wanafunzi waweze kuchunguza kwa undani mawazo yao na kujiwekea changamoto wenyewe juu ya kazi husika. Pili, wanafunzi wanahitaji kuelezwa kuhusu umuhimu wa uwasilishaji katika makundi. Tatu, ikiwezekana, mfululizo wa kozi za tathmini unapaswa kuundwa ili kuendeleza tafakuri tunduizi katika mifumo mbalimbali ya maudhui ya kimaarifa.

Data za utafiti wetu zilionesha kwamba baadhi ya walimu wa Kiswahili wanaweza kuunda mikakati mwafaka katika ukuzaji wa tafakuri tunduizi kupitia fasihi. Hapa chini tuna matokeo kutoka ushuhudiaji ambapo mwalimu B1 alikuwa anafundisha uhakiki wa hadithi simulizi inayopatikana katika kitabu cha mwanafunzi wa kidato cha tano inayoitwa “Jongoo na Chura”

wanafunzi walijadili kuhusu sehemu ambayo Jongoo alikuwa akimweleza rafiki yake Chura namna alivyopata ngozi nyororo kwa kusema:

> “Rafiki yangu Chura, ngozi hii nyororo unayoiona ni kazi kubwa tena ngumu ambayo mke wangu amekuwa akifanya kwa muda wa miaka mingi. Kila asubuhi huweka kikaango motoni kisha hujaza mafuta....” Kabla hajaendelea na kumaliza, Chura alimkata kauli rafiki yake kwa kusema, “Basi! Basi! Nimeishaelewa. Huna haja ya kunielezea zaidi. Yote haya nitayatenda na utaona nitakavyonawiri.” Jongoo alijaribu kumshawishi amsikilize lakini Chura alisisitiza kwamba kwa utangulizi ule amekwisha elewa kila kitu. Marafiki wale waliagana.

Kutokana na sehemu hii ya juu, wanafunzi walipewa nafasi ya kujadiliana na kutafakari juu ya mazungumzo ya Jongoo na Chura. Wanafunzi wengi walisema:

> Inaonekana kuwa Jongoo alikuwa anataka kuongeza kitu muhimu sana kwa maneno yake. Ila, rafiki yake Chura alimkata kauli. Naona kwamba hali hii ya Chura kumkata kauli Jongoo huweza kumletea matatizo hatari kwani hakumtegea masikio ili amalize kwa ukamilifu kitu ambacho alitaka kumwambia.

Mwalimu aliwauliza wanafunzi “Je, mmewahi kuwaona watu kama Chura wanaowakata kauli watu wengine wakati wanapotaka kutoa ujumbe kwao au kwa watu wengine?” “Je, mnadhani kwamba kuna matokeo mabaya yanayoweza kutokea kutokana na jambo la kuwakata kauli watu wengine?”

Kutokana na maswali ya mwalimu, wanafunzi wengi walijibu kwa kusema:

> Ndiyo, mara nyingi tunawaona watu kama Chura. Hata katika darasa na jamii au familia zetu tunawaona sana. Kwa mfano; wakati wa mijadala na mikutano, baadhi ya watu hukatiliana kauli. Wenzao wanawabembeleza na kuwaomba kuwategea masikio kutokana na wazo wanaloamini kwamba ni muhimu kwao na kwa jamii kubwa lakini wanakataa kuwapa nafasi ya kusema. Na kuna wengine wanaokata kauli wenzao wakati wanapowapa maelezo fulani wanayowauliza kwa sababu hawayajui, lakini wakawakata kauli wakati baado hawajamaliza kusema. Watu hawa mara nyingi hufanya kinyume na mahitaji ya msemaji au mwelezaji kwa sababu

hawakumtegea masikio. Ingawa mara nyingi hawaonyeshi kwamba walipata hasara lakini, nina uhakika kwamba hujuta.

Hali hii inayodhihirika katika mjadala wa mwalimu na wanafunzi inatuonesha namna ambavyo wanafunzi wanaweza kutumia tafakuri tunduizi inayotokana na kazi za fasihi kwa kutoa suluhu za matatizo yanayowakumba katika maisha yao halisi.

Ubora wa fasihi katika ukuzaji wa tafakuri tunduizi kama msingi wa uwezo tofauti aghalabu hutokana na kwamba wakati wanafunzi wanaposhughulikia kazi za fasihi, wanahitaji kuonesha uwezo tofauti kama vile kutofautisha maoni na ukweli na uongo; kuelewa uhalisi au maana zilizodokezwa na sauti ya mtunzi au msimulizi; kupata maelezo yanayohusiana na maswala yanayojadiliwa; kujua usababishaji wa uhusiano au uhusiano kati ya visa na matukio; kugundua mshikamano dhaifu kutoka katika maelezo yaliyozingatiwa; kutoa hoja za kimaadili na hukumu zenye misingi ya haki; na kutumia kile ambacho wamejifunza kutoka katika mchakato huu kwa nyanja zingine au kwa ulimwengu halisi.

Wanafunzi walionesha kwamba kinachohitajika kama gharama kufanikisha mchakato wa ukuzaji wa tafakuri tunduizi kwa kutumia kazi za fasihi, ni mambo muhimu yafuatayo:

Kwanza, ni kutumia mijadala juu ya kazi ya fasihi iliyoteuliwa na kuandaliwa vizuri. Ni bora mwalimu achague kazi mwafaka kwa wanafunzi wake, afanye maandalizi ya somo vizuri kwa kutumia mijadala inayoongozwa ili kushughulisha wanafunzi kikamilifu. Pili, ni matumizi ya maswali yenye ujanja na mitego maalum. Ni bora mwalimu awaulize wanafunzi maswali ambayo yana ujanja na mitego ambayo yanaibua fikra zao juu ya kazi husika. Hali hii huwasaidia wanafunzi kutoa na kufafanua mawazo yao kwa kutumia tafakuri tunduizi. Tatu, ni uchaguzi wa matini za kusoma ambazo zinawapa wanafunzi miktadha ya kuaminika katika ukuzaji wa tafakuri tunduizi na utatuzi wa matatizo nazo zinachangia kwa kiasi kikubwa kuchangia katika ukuzaji wa tafakuri tunduizi miongoni mwa wanafunzi. Hali hii inajumuisha kuhusianisha mawazo ya kazi husika ya fasihi na maisha halisi ya mwanafunzi ili aweze kufikiri zaidi juu ya maisha yake.

#### 4.3.4.2 Namna ya Ukuzaji wa Utafiti na Utatuzi wa Matatizo Kupitia Fasihi

Wakati wa kutumia fasihi kwa kusudi la kuwasaidia wanafunzi kukabiliana na matatizo halisi, walimu wanapaswa kuzingatia madhumuni ya kazi ya kujifunza, kuamua nani atashiriki, na kupanga juu ya kuhusisha matatizo ya wahusika wa hadithi na uzoefu wa maisha wa wanafunzi (Jalongo, 1983).

Miller (1997) anapendekeza miongozo ifuatayo kwa walimu juu ya kutumia fasihi kuwasaidia wanafunzi kukuza uwezo wa utafiti na utatuzi wa matatizo: Mosi, ni kuwapa wanafunzi fursa na nafasi ya kuamua na kujadili tatizo kama wanavyolitambua na kuliona. Pili, kuwahamasisha na kuwatia moyo wanafunzi juu ya fikra zao kuhusu utatuzi wa tatizo husika. Tatu, ni kuwasaidia wanafunzi kuchunguza faida na hasara za masuluhisho mbalimbali juu ya tatizo fulani na kuwaongoza kuchagua moja linaloonekana kufaa zaidi. Nne, ni kuwaruhusu wakusanye nyenzo na rasilimali muhimu kisha, ikiwezekana waanze kutekeleza suluhisho wanazozichagua kwa tatizo husika. Tano, akiwa pamoja na wanafunzi, mwalimu atathmini na kujadili ikiwa suluhisho la tatizo lilifanikiwa. Kama limefanikiwa, mwalimu awasaidie wanafunzi kufikiria mabadiliko katika suluhu lililotekelezwa, au awahimize kutafuta suluhu mpya.

Aidha, data za utafiti zilizotokana na ushuhudiaji zilionesha kwamba walimu wa Kiswahili wanashindwa kuhusisha matatizo yanayoshughulikiwa darasani na miktadha ya nje ambapo wanafunzi huishi. Ushuhudiaji ulituonesha kwamba baadhi ya walimu wanajaribu kuuliza na kutumia maswali sahihi yanayokuza uwezo wa utatuzi wa matatizo miongoni mwa wanafunzi katika mchakato wa ufundishaji na ujifunzaji. Aidha, maswali na majibu yanayotolewa kwa maswali hayo huishia darasani yaani mwalimu hajengi mazingira ya kuwahamasisha wanafunzi kuyatekeleza katika maisha yao halisi.

Hata hivyo, fasihi inaweza kutumika kama chombo bora cha kuwasaidia wanafunzi kukabiliana na matatizo ya kihisia na kijamii. Kupitia majadiliano ya masuala yenye matatizo yaliyomo katika fasihi, walimu wanaweza kuwasaidia wanafunzi kukabiliana na masuala ya maisha halisi yanayowasilishwa katika kazi ya fasihi inayoshughulikiwa.

#### 4.3.4.3 Jinsi ya Utumizi wa Fasihi kama Nyenzo ya Ukuzaji wa Ubunifu na Ugunduzi

Ubunifu na ugunduzi vinazidi kuwa muhimu katika maendeleo ya jamii ya maarifa ya Karne ya 21. Ni ujuzi na uwezo wa kufanya miunganisho isiyotarajiwa na kutoa mawazo mapya na yanayofaa (Ferrari na wenzake, 2009). Kwa hivyo, ujifunzaji wa ubunifu ni ujifunzaji wowote unaohusisha uelewa na ufahamu mpya, ambao humruhusu mwanafunzi kwenda zaidi ya ujuzi wa kimawazo, na kuzingatia zaidi ujuzi wa kutafakari.

Data za utafiti zilituonesha kwamba wanafunzi wana ubunifu na ugunduzi mdogo sana katika Kiswahili.Wanafunzi walituelezea kwamba hali hii inatokana na ukosefu wa vifaa vinavyowaathiri kubuni kitu kipya juu ya mambo wanayojifunza darasani. Baadhi ya wanafunzi wanaeleza kwamba hawana muda wa kutafakari juu ya mambo wanayojifunza

darasani kutokana kazi nyingi za nyumbani kutoka walimu na wazazi. Hapa tuna dondoo kutoka usaili. Mwanafunzi D2 anasema:

> Kutokana na mifano ya kazi za fasihi tunazojifunza darasani, nasi tunaweza kutunga kazi zetu binafsi na kuzikusanya kwa mwalimu ili azisahihishe na kuzitolea maoni. Kwa bahati mbaya mara nyingi mwalimu anatukosoa makosa ya kisarufi tu lakini ni bora kutushauri na hata kuhusu mpangilio na uwiano wa mawazo, mada yenyewe na uchaguzi wake nakadhalika. Tuna changamoto kubwa ya ukosefu wa muda wa kufanya utafiti na kufikiri kwa ajili ya masomo mengi na kazi za nyumbani.

Dondoo hili linatuonesha kwamba mwalimu anatarajiwa kuwasaidia na kuwahamasisha wanafunzi wake katika mchakato wa ukuzaji wa ubunifu na ugunduzi. Ni bora mwalimu atenge muda wa kuchanganua mawazo ya wanafunzi ili aweze kuyatolea maoni yanayowahamasisha kukuza uwezo huu. Wanafunzi nao wanahitaji muda wao wa kufanya utafiti na kufikiri juu ya mambo wanayojifunza. Hii ni kwa sababu ubunifu na ugunduzi hauishii tu katika uhakiki wa fasihi na ujifunzaji wa lugha darasani, bali unapaswa kutendwa katika jamii na familia halisi za wanafunzi. Hivyo basi, ukuzaji wa uwezo huu huhitaji marekebisho yenye athari nzuri kwa mwanafunzi.

Aidha, data za utafiti zilitueleza kuwa tatizo hili hutokana na ukosefu wa fursa kutoka kwa walimu, muda na mazingira. Walimu hawajengi fursa za kukuza ubunifu za ugunduzi wala hawatumii mikakati inayofaa kukuza uwezo huu. Hapa tuna mawazo ya walimu juu ya swala la utumizi wa fasihi katika kukuza uwezo wa ubunifu na ugunduzi miongoni mwa wanafunzi. Mwalimu B1 anasema:

> Tunaweza kutumia mifano ya kifasihi na kuwaomba wanafunzi kujenga mawazo na kazi zao kwani kazi za kifasihi huwavutia zaidi. Hata hivyo, tatizo kubwa linatokana na wanafunzi tulio nao leo, walifeli katika mtihani wa serikali. Wao wanadhani kwamba mchepuo wa lugha ni rahisi ndipo wakajiunga hapa. Hawawezi kuwa na jambo jipya. Tatizo lingine linatokana na ukosefu wa muda na rasilimali zinazowahamasisha wanafunzi kukuza ujuzi huu. Shule nyingi hazina kamusi ya Kiswahili, hazina kompyuta na mtandao hata wanafunzi wetu hawana simu za kutumia labda katika utafiti yaani tunatumia akili zetu tu.

Dondoo la hapo juu linatuonesha kwamba walimu hawawaamini wanafunzi wao. Hili ni tatizo kubwa katika ufundishaji na ujifunzaji. Kutokana na Nadharia ya Utambuzi na Nadharia ya Maingiliano ya Tamaduni-jamii, kila mwanafunzi anaweza kubuni kitu kipya kutokana na mifano aliyopewa pamoja na athari za kijamii. Hivyo basi, mikakati ya kwanza katika mchakato wa ukuzaji wa ubunifu na ugunduzi ni mwalimu kumwamini mwanafunzi na kumpa muda na fursa ya kutafakari juu ya mambo ambayo anamfundisha. Kwa hivyo, dondoo hili linatuonesha kwamba walimu hawawapi muda wanafunzi ili nao wafanyie uchunguzi masomo yao.

Aidha, kutokana na data za ushuhudiaji, mtafiti aliona kwamba walimu wanapambana na swala la utumizi wa dakika za somo ili wamalize yale wanayotarajiwa kufundisha kutokana na mtaala. Hali hii inawafanya kuwanyima wanafunzi muda wa kufikiria wala kujadili juu ya maswali na mazoezi wanayoulizwa wakati wa somo. Hata makundi hayatumiki ipasavyo kwani hayapewi muda ufaao kwa kumaliza kazi wanazopewa wanamakundi. Ili kukuza uwezo wa ubunifu na ugunduzi miongoni mwa wanafunzi kwa kutumia fasihi, ni bora mwalimu awaamini wanafunzi na kuwatengea muda wa kufanyia kazi zaidi maswali ya kifasihi wanayopewa. Ni bora kuchagua kazi zinazoeleweka kwa wanafunzi na zenye wahusika wabunifu na wagunduzi. Mwalimu anapaswa kuwapa maoni wanafunzi juu ya kazi zao. Mwalimu anatarajiwa kutumia muda zaidi kwa kuunganisha maudhui na wanafunzi kuliko kumaliza somo.

#### 4.3.4.4 Kukuza Stadi za Mawasiliano Kupitia Fasihi

Maley (2001) anaeleza kwamba fasihi ni nyenzo tajiri ya kufundishia mawasiliano katika lugha ya pili kwa sababu kazi za kifasihi hasa hadithi na maudhui yake huwavutia na kuwanufaisha wanafunzi kuzungumza. Matokeo ya utafiti wetu yanatueleza kuwa walimu na wanafunzi wa Kiswahili hujaribu kutumia fasihi katika ukuzaji na uendelezaji wa umilisi wa mawasiliano. Hali hii inathibitishwa na data zilizokusanywa katika ushuhudiaji ambazo zinaonesha kwamba kazi za fasihi hutumiwa kwa kufungua na kuendeleza mijadala kati ya wanafunzi wenyewe kwa wenyewe, lakini pia kati ya wanafunzi na walimu.

Hata hivyo, katika usaili, wanafunzi walitoa maoni yao kuhusu namna wanavyopenda kukuziwa uwezo wa mawasiliano kupitia fasihi. Mwanafunzi A2 anasema:

> Wakati tunapoenda kujifunza kazi fulani ya fasihi, ni bora mwalimu atusaidie kuelewa vizuri anwani ya kazi husika na yaliyomo. Kisha, atuongoze na atupe muda wa kuhusisha anwani yake na yaliyomo.

> Tunapoelewa mambo haya, tunaweza kutoa maoni mengi na kuyawasilisha juu ya kazi hiyo. Kitu kingine ni kutupatia fursa ya kufanya mashindano kati yetu na shule nyingine juu ya kutunga kazi za kifasihi katika Kiswahili kama vile nyimbo, shairi na hata kuwasilisha maoni yetu juu ya kazi za wengine kama vile riwaya.

Dondoo hili linatueleza vizuri namna ambavyo wanafunzi wanadhani fasihi inaweza kutumiwa katika kukuza uwezo wao wa kimazungumzo. Ni kweli wanafunzi huhitaji kuelewa, kuhusisha na kuunganisha anwani (kichwa, jina) ya kazi ya fasihi na yaliyomo. Fursa hii huwajengea mazingira ya kutoa maoni mengi juu ya kazi husika. Baada ya jambo hili, ni bora mwalimu awapatie wanafunzi muda wa kuwasilisha na kushirikisha maoni yao kupitia lugha lengwa. Kama alivyoeleza mwanafunzi A2, mijadala na mashindano ya utunzi katika lugha lengwa ni muhimu sana katika mchakato wa ukuzaji wa stadi za kimawasiliano.

Aidha, walimu nao walitoa maoni yao kuhusu namna ya kukuza stadi za mawasiliano katika Kiswahili kupitia fasihi.

Haya ni mawazo ya mwalimu D1 anasema:

> Tunajaribu kutumia mbinu inayoegemea kwa mwanafunzi na makundi zaidi. Wakati wa ufundishaji na ujifunzaji tunajenga mijadala kati yetu na wanafunzi au kati ya wanafunzi wenyewe juu ya kazi inayoshughulikiwa. Tunawauliza maswali wanafunzi na kuwapa fursa za kuongea na kutetea maoni yao. Tunatunga maswali kutokana na kazi inayoshughulikiwa na kuwapatia wanafunzi kwa ajili ya kuyawasilisha.

Mawazo ya mwalimu D1 yanaonesha kwamba walimu wanaelewa baadhi ya njia na mikakati ya kukuza stadi za mazungumzo miongoni mwa wanafunzi. Hata hivyo, data za ushuhudiaji zilituonesha kwamba hawaitekelezi mikakati hiyo kama wanavyosema katika dondoo la hapo juu. Hii ni kwa sababu wengi hujadili na wanafunzi wachache sana wakati wa somo. Wakati mwingine baadhi ya walimu hawatumii njia ya unasibu kwa kuuliza au kuwaongelesha wanafunzi. Hali hii inasababisha kutumia wanafunzi wanaojiamini kuliko wengine. Hata hivyo, njia ya mijadala na midahalo kati ya makundi hufaa zaidi. Njia ya mijadala na midahalo huwafanya wanafunzi kugombania heshima yao ya ushindi. Hali hii humfanya kila mwanakikundi wa kundi kushirikisha wazo lake ili wapate ushindi. Mada za kifasihi huwavutia na kuwamotisha wanafunzi kuzua na kuendeleza mijadala kati yao. Baadhi ya mada za mijadala zinazowavutia wanafunzi ni kama vile kulinganisha watunzi au wasanii,

kujadili juu ya maana ya mtunzi, kupendekeza maendeleo ya sehemu au ya kazi nzima, kutoa maoni na suluhisho juu ya migogoro iliyopo kati ya wahusika nakadhalika.

#### 4.3.4.5 Ukuzaji wa Ushirikiano, Utawala Binafsi na Stadi za Maisha Kupitia Fasihi

Jyotsna na Dwarakanath (2018: 74) wanaeleza jinsi fasihi inavyoweza kutumiwa katika ukuzaji wa utawala binafsi na stadi za maisha kwa kutumia mfano wa kazi moja ya fasihi. Wanasema:

> If we take the "Hamlet" one of the famous works of Shakespeare who is a legendary in literature. He gives a message and direction to the young minds/students/readers through the character he created on the life skills.
>
> Tunapochukua "Hamlet" moja wapo ya kazi maarufu za Shakespeare ambaye ni bingwa katika fasihi, anatoa ujumbe na mwelekeo kwa akili/wanafunzi/na wasomaji wachanga kupitia mhusika aliyemtengeneza kuhusu stadi za maisha [Tafsiri Yetu].

Baada ya kutoa mfano wa kazi ya fasihi na kueleza namna unavyochangia katika mchakato wa ukuzaji wa stadi za maisha na utawala binafsi miongoni mwa wanafunzi, Jyotsna na Dwarakanath (whj) waliendelea kutoa sampuli ya mafundisho juu ya ujuzi wa utawala binafsi na stadi za maisha. Kwa mifano miwili kutoka aina mbili tofauti, katika mfano wa kwanza wataalamu hawa wanafafanua kwamba Shakespeare alitumia mhusika wake Hamlet ili kuonya vijana kuhusu stadi za maisha, kuwa waangalifu sana wanapozungumza na wengine. Wanasema:

> Give thy thoughts no tongue; and
> Give every man thy ear, but few thy voice
>
> Toa mawazo yako siyo ulimi, na umtegee kila mtu sikio lako, lakini sauti yakoisijitokeze sana. [Tafsiri Yetu]

Mfano wa hapo juu unaonya watu juu ya jinsi ya kushirikiana na watu kwa ufanisi. Onyo hili halimaanishi kusikiliza bila kusema wala kutozungumza wakati wa mawasiliano. Linasisitiza kusikiliza kwa makini na kwa uhakiki bila kumkata kauli mzungumzaji. Onyo hili ni muhimu sana maishani kwani linanaweza kutufanya sote kupata ujumbe kamili wakati wa mawasiliano.

Katika mfano wa pili, Jyotsna na Dwarakanath (whj) wanatumia shairi la Robert Frost iitwayo *the road not taken* na kueleza kwamba mwandishi alitoa ushauri kwa hadhira yake kuhusu jinsi ya kuishi kwa ufanisi katika ulimwengu wenye miiba ya kuchoma. Wanasema:

> "Do not believe anything anybody tells you, including anything I tell you unless it agrees with your own experience and your own common sense".

> "Usiamini chochote unachoambiwa na mtu yeyote, ikiwa ni pamoja na chochote ninachokuambia mimi, isipokuwa kile kinachokubaliana na uzoefu wako mwenyewe pamoja na fikra zako" [Tafsiri Yetu].

Maoni ya hapo juu nayo hayakatazi ushirikiano kati ya mtu na watu wengine. Kitu kinachosisitizwa ni umakini, uangalifu, utafakari na uamzi wa mtu mwenyewe juu ya ushirikiano kwa ufanisi wa maisha yake. Uwezo wa kusikiliza kwa umakini na uhakiki bila kukatana kauli, ni mojawapo ya stadi muhimu sana katika maisha ya mwanadamu hususan katika Karne ya Ishirini na Moja ambapo watu wanalazimishwa kupata kila habari kwa ukamilifu wake. Uwezo wa kuhakiki habari nao unahusu stadi ya utawala binafsi ambao nao unahitajika kwa kila mwanadamu. Hivyo basi, maonyo ya hapo juu, yanajumuisha stadi tatu yaani ushirikiano, utawala binafsi, na stadi za maisha.

#### 4.3.4.6 Fasihi katika Ukuzaji wa Ujifunzaji usio na Mpaka

Ujifunzaji usio na mpaka ni muhimu kwa siku zijazo kwani huwapa watu uwezo fulani wa kukabiliana na mabadiliko na kujenga maisha bora ya baadaye (UNESCO, 2020). Hivyo basi, ni muhimu kukuza uwezo huu miongoni mwa wanafunzi.

Data za ushuhudiaji zilituonesha kwamba baadhi ya walimu huingiza mawazo yanayohamasisha wanafunzi kupata mifano ya ujifunzaji usio na mpaka. Hata hivyo, mifano waliyotoa aghalabu ilikuja kiholela. Kwa hivyo, ni bora zaidi kutumia mifano kutoka kazi za kifasihi kama vielelezo vya ujifunzaji usio na mpaka kwa wanafunzi.

Ujifunzaji bila mpaka huweza kufundishwa kupitia methali, misemo, hadithi, riwaya na kazi nyinginezo za kifasihi. Hapa tuna dondoo kutoka mwalimu D1 akieleza namna ambavyo wanatumia fasihi kwa kufundisha ujifunzaji usio na mpaka. Anasema:

> Tunaweza kupata mifano ya methali kama vile "mali bila daftari hupotea bila habari" methali hii inaweza kunisaidia kufundisha wanafunzi jinsi elimu ya biashara haina mpaka, nikawaelezea mengi zaidi. Napenda

> kutumia riwaya ya *Adili na Nduguze* ambapo Adili alikubali kwenda kujifunza juu ya biashara za ugenini ingawa biashara yake haikukuwa na tatizo.

Kutokana na mifano iliyotolewa na mwalimu D1 kuna fursa nyingi za kufundisha uwezo wa ujifunzaji usio na mpaka kupitia fasihi. Kitu muhimu sana ni kujua kazi inayojumuisha mifano mwafaka kwa kukuza uwezo huu. Kama anavyoeleza mwalimu wa hapo juu, katika riwaya ya *Adili na Nduguze* iliyoandikwa na Shaban (1980) kuna mifano ya wahusika kama vile Adili, mfalme Rai na Ikibali ambao ni vielelezo vya ujifunzaji usio na mpaka. Kwa upande wa Adili, alionesha ujuzi wa kukubali kujifunza kutokana na kila hali. Kwa upande wake, mateso na dhiki yalikuwa yakimsaidia kujifunza kama furaha na starehe. Ikibali na mfalme Rai nao wanaweza kutumiwa kama mifano ya kuigwa maishani. Hivyo basi, ili kukuza uwezo wa ujifunzaji usio na mpaka miongoni mwa wanafunzi, ni bora mwalimu atumie mifano mizuri kwa wanafunzi ambayo inawakilisha mambo yajitokezayo maishani mwao. Ni bora pia kuwauliza wanafunzi somo au ujumbe walioupata kutokana na matendo, sifa na tabia za wahusika wanaopatikana katika kazi fulani ya fasihi.

### 4.3.5 Namna ya Kuitumia Fasihi Kufundisha Maswala Mtambuka

Ujumuishaji na ufundishaji wa masuala mtambuka katika kila somo ni muhimu kwa sababu husaidia wanafunzi kupanua uelewa wao kuhusu maswala muhimu katika jamii yao. Matokeo ya data zilizokusanywa na utafiti wetu, yalionyesha kuwa baadhi ya walimu wa Kiswahili hawaelewi maana ya maswala mtambuka wala hawajui kuzifundisha ipasavyo. Utafiti ulikusanya dondoo la mwalimu B1 akitoa maana ya maswala mtambuka.

> Maswala mtambuka ni kama aina ya maswali yanayoulizwa na wanafunzi katika somo.

Dondoo hili linaonesha kwamba kila swali linaloulizwa na mwanafunzi ndani ya mchakato wa somo huchukuliwa kama swala mtambuka. Kwa hiyo, kutokana na dondoo hili tuliona kwamba baadhi ya walimu wa Kiswahili hawajui maana ya swala mtambuka. Kwa bahati nzuri, tulipojadili baadhi ya mifano ya maswala mtambuka, wengi waliitoa kwa usahihi. Hii ni baadhi ya mifano waliyotoa: Mafunzo kuhusu usawa wa jinsia, mafunzo kuhusu desturi ya usanifishaji, utunzi wa mazingira, elimu kuhusu uzalishajimali nakadhalika.

Wakati wa kujadili namna anavyoelezea mwanafunzi kuhusu maswala mtambuka kupitia fasihi, walimu walitoa mawazo yao. Mwalimu C1 alisema:

> Kuna mashairi mengi yanayozungumzia swala la usafi. Tunaposhughulikia aina ya shairi kama hili, siwezi kukwepa mada ya usafi kwani ni swala la muhimu katika maisha ya kila binadamu.

Mawazo yamwalimuwa hapo juu yanaeleza vizuri namna maswala mtambuka yanavyoweza kujadiliwa kupitia fasihi. Kwa kueleza jinsi anavyoweza kuhamasisha swala la thamani na mwenendomiongoni mwa wanafunzi, mwalimu mwingine D1 aliegemea shairi la Benjamin Nashon linalopatikana katika kitabu cha mwanafunzi wa kidato cha tano. Shairi hilo ni lifuatalo:

> Farakano za hewani, zenye kuzusha mikasa,
> Wema ukiwa moyoni, kweli hutazitomasa,
> Utaziacha njiani, ziende zinakopasa,
> Ugomvi, usengenyi, adui za mtu mwema.
>
> Ukarimu maishani, upole, utii hasa,
> Mambo haya duniani, yazishinda hata pesa,
> Wema kitu cha thamani, toka jana hadi sasa,
> Mtu aliye na wema, anazo busara nyingi (uk.88)

Kutokana na shairi hili, mwalimu D1 alisema kwamba wanaweza kulisoma darasani halafu mwalimu akawauliza wanafunzi swali kama hili; “Kutokana na shairi hili ni nini kinashinda pesa?” Uwezekano wa kujibu swali hili ni kwamba wanafunzi wataorodhesha tabia nzuri kama zilivyotajwa na mshairi. Baada ya kuorodhesha tabia hizo, mwalimu anaweza kuendeleza mjadala kwa kuuliza swali la “kwa nini tabia hizo hushinda pesa?” Kutokana na swali hili wanafunzi wataendelea kutoa maoni yao wakijadili umuhimu wa maadili na mwenendo mwema.

Leo, serikali ya Rwanda inapambana na changamoto ya watoto wa mitaani. Hali hii mara nyingi hutokana na tatizo la kuzaa watoto ambao wazazi hawana uwezo wa kuwalea. Kutokana na tatizo hili, mtaala unaoegemea katika uwezo unazingatia suala mtambuka la elimu kuhusu ufahamu wa jinsi. Kuna kazi nyingi zinazojadili ugumba na utasa, UKIMWI na matokeo mengine mabaya ya umalaya na uasherati kama matatizo ya kijamii. Kazi hizo zinaweza kutumiwa kuwaelezea wanafunzi swala la jinsi na udhibiti wake.

### 4.3.6 Uteuzi na Uchaguzi wa Kazi za Fasihi katika Ufundishaji wa Lugha na Ukuzaji wa Uwezo wa Mwanafunzi

Ni jukumu la mwalimu kuteua kazi za fasihi zinazofaa kwa kuvutia na kuwa mfano mzuri wa kuhimiza uwezo wa jumla au stadi za Karne ya Ishirini na Moja. Atmaca na Günday (2016:129) wanakubali kwamba kazi za fasihi hazina mpaka kutokana na viwango tofauti vya wanafunzi. Wanasema:

> Literary texts are authentic works that can be used at every level in the classroom. For example, fairy tales and stories can be used in a foreign language class as a very effective course material for children. Likewise, the classical novels and poems known all over the world can be used also by teacher in the class as teaching material that will make the lesson more fun and enjoyable for adults.
>
> Maandishi ya kifasihi ni kazi halisi zinazoweza kutumika katika kila ngazi ya darasa. Kwa mfano, masimulizi ya kubuni na hadithi zinaweza kutumika katika darasa la lugha ya kigeni kama nyenzo nzuri sana za kozi kwa watoto. Kadhalika, riwaya na mashairi yanayojulikana kote ulimwengu yanaweza pia kutumiwa na mwalimu darasani kama nyenzo ya kufundishia ambayo itafanya somo kuwa la kuchekesha na kufurahisha kwa watu wazima [Tafsiri Yetu].

Mawazo ya Atmaca na Günday (Whj) yanatuthibitishia kwamba fasihi inaweza kutumika kwa kila kiwango cha mwanafunzi. Hapa, mwalimu anatarajiwa kwanza kuandaa kazi zinazoendana na viwango vya wanafunzi wake, kazi zinazozingatia utamaduni na maisha yao halisi na zinazovutia kifani na kimaudhui. Kisha, anatarajiwa kujenga muktadha wenye fursa ya wanafunzi kuzisoma na kuzielewa.

Kwa upande mwingine, data za utafiti uliofanyika zinaonyesha kwamba kuna upungufu katika uteuzi wa kazi za fasihi za ufundishaji na ujifunzaji miongoni mwa walimu. Hapa chini kuna mawazo ya mwalimu A1. Anasema:

> Fasihi inaweza kutumiwa kwa kufundisha lugha na kukuza uwezo wa jumla wa wanafunzi. Lakini hii inawezekana kwa wanafunzi wa kiwango cha juu. Tunajua kwamba lugha inayotumika katika kazi za fasihi si rahisi kuielewa hasa kwa wanafunzi kama tunao katika kidato cha nne.

Dondoo hili, linatuonesha kwamba tatizo lipo kwa upande wa walimu. Huenda tatizo hili linatokana na ujuzi wao mdogo katika nyanja mbalimbali kama vile lugha ya Kiswahili, utafiti au elimu (ufundishaji). Hii ni kwa sababu matokeo ya uchanganuzi wa matini yalionesha kwamba kazi za fasihi simulizi zilizopo katika vitabu vya wanafunzi wa kidato cha nne hadi cha sita, zote zinatumia lugha rahisi kuliko vifungu vya ufahamu vilivyomo. Hata kwa ujumla, kuna kazi nyingi hasa simulizi za Kiswahili ambazo ni rahisi kuzielewa kuliko fahamu zinazotumiwa na baadhi ya walimu wakati wa ufundishaji na ujifunzaji wa Kiswahili. Hivyo basi, mwalimu anatarajiwa kupata muda wa kutafiti, kukusanya, kusoma, kuhakiki, kuteua na kuchagua kazi za fasihi zinazofaa kukuza uwezo wa lugha na uwezo wa jumla miongoni mwa wanafunzi wake kulingana na viwango vyao vya lugha na tafakuri tunduizi.

## 4.4 Muhtasari wa Sura ya Nne

Sura hii imeshughulika na uwasilishaji wa matokeo ya utafiti. Matokeo ya utafiti yametokana na malengo ya utafiti huu. Utafiti huu umebainisha athari za fasihi katika ufundishaji wa lugha na utekelezaji wa mtaala unaoegemea katika uwezo. Katika sehemu ya ufundishaji wa lugha ya pili, sura hii imejadili jinsi fasihi inavyoweza kutumiwa kama nyenzo ya kufundishia vipengele vya lugha kama vile sarufi na msamiati pamoja na stadi za lugha kama vile kuandika, kusoma, kusikiliza na kuzungumza. Kwa upande wa utekelezaji wa mtaala unaoegemea katika uwezo, sura hii imejadili jinsi fasihi inavyoweza kutumiwa ili kukuza uwezo mbalimbali kama vile tafakuri tunduizi, utafiti na utatuzi wa matatizo, ubunifu na ugunduzi, stadi za mawasiliano, ushirikiano, utawala binafsi na stadi za maisha pamoja na ujifunzaji usio na mpaka miongoni mwa wanafunzi. Pia, sura hii imejadili jinsi fasihi inavyojumuisha na kuzingatia mifano ya maswala mtambuka yanayosisitizwa katika utekelezaji wa mtaala unaoegemea uwezo. Mwishoni, surahii imejadili swala la uteuzi na uchaguzi wa kazi za fasihi katika ufundishaji na ujifunzaji wa lugha na utekelezaji wa mtaala unaoegemea katika uwezo. Sura inayofuata inahusu muhtasari, hitimisho na mapendekezo ya tasinifu.

## SURA YA TANO

## HITIMISHO

### 5.1 Utangulizi

Utafiti uliozaa tasinifu hii ulihusu kuchunguza fasihi kama nyenzo ya kufundishia lugha ya pili na kutekeleza mtaala unaoegemea katika uwezo. Kutokana na malengo ya utafiti huu ambayo yanaweka umahsusi kwa Wilaya ya Rusizi hususan katika shule za sekondari, kidato cha tano katika mchepuo wa Kiswahili, mtafiti alichukua sampuli ya shule nne (4) na kuongozwa na Nadharia ya Utambuzi na Maingiliano ya Tamaduni-jamii. Katika sura hii tunaangazia muhtasari wa tasinifu, utoshelevu wa nadharia za uchambuzi wa data, mchango mpya wa utafiti huu, maoni kuhusu utafiti huu, mambo yanayotakiwa kuzingatiwa ili kuondokana na changamoto, mapendekezo, na hitimisho kuhusiana na utafiti ulioibua tasnifu hii. Mapendekezo yamegawanywa katika sehemu nne. Sehemu ya kwanza ni mapendekezo kwa walimu na wanafunzi. Pili, ni mapendekezo kwa watunzi wa fasihi kwa jumla. Tatu, ni mapendekezo kwa serikali na watunga mitaala. Mwisho, ni mapendekezo kwa tafiti zijazo.

### 5.2 Muhtasari waTasinifu

Tasinifu hii ililenga kuchunguza nafasi ya fasihi katika ufundishaji wa lugha ya pili na utekelezaji wa mtaala unaoegemea katika uwezo. Utafiti ulitumia kazi tofauti za fasihi andishi na simulizi, mawazo ya wataalamu na watafiti watangulizi pamoja na mawazo ya walimu na wanafunzi wa lugha ya pili na fasihi. Katika utafiti uliofanyikayalishughulikiwa mambo muhimu mawili ambayo ni pamoja na ufaafu wa fasihi katika ufundishaji wa lugha ya pili na utekelezaji wa mtaala unaoegemea katika uwezo pamoja na namna ya kutumia fasihi katika ufundishaji wa lugha ya pili na utekelezaji wa mtaala unaoegemea katika uwezo.

Ili kuthibitisha ufaafu wa fasihi katika ufundishaji wa lugha ya pili, utafiti ulijiegemeza kwenye mifano inayotolewa na fasihi katika ufundishaji wa sarufi, msamiati, stadi za kuandika na kusoma pamoja na stadi za kusikiliza na kuzungumza. Kwa upande wa ufaafu wa fasihi katika utekelezaji wa mtaala unaoegemea katika uwezo, tulijiegemeza kwenye mifano inayotolewa na fasihi katika ukuzaji wa uwezo wa jumla miongoni mwa wanafunzi pamoja na maelezo juu ya maswala mtambuka yanayotolewa na fasihi. Katika uchunguzi wa namna ya kutumia fasihi katika ufundishaji wa lugha ya pili, tulichunguza jinsi ya kutumia mifano inayotolewa na fasihi

kwa kufundishia sarufi, msamiati na stadi nne za lugha. Kwa upande wa namna ya kuitumia fasihi katika utekelezaji wa mtaala unaoegemea katika uwezo, tulichunguza namna ya kuegemea mifano ya fasihi kwa kukuza uwezo wa jumla miongoni mwa wanafunzi na kufafanua masuala mtambuka yakiwemo thamani na mwenendo mwema.

Tasinifu nzima imegawanyika katika sura tano. Sura ya kwanza inatoa utangulizi na mwelekeo wa utafiti huu kwa kujadili usuli wa tatizo la utafiti, tamko la tatizo la utafiti, malengo ya utafiti, maswali ya utafiti, manufaa ya utafiti, mawanda ya utafiti, vikwazo vya utafiti, na utatuzi wake.

Sura ya pili nayo imegawanyika katika sehemu kuu mbili ambazo nimapitio mbalimbali ya tafiti tangulizi yaliyopitiwa na viunzi vya nadharia zilizooongoza utafiti huu. Katika sehemu ya mapitio ya maandiko, utafiti umejikita kujadili na kutolea maoni mapitio kuhusu fasihi, mapitio kuhusu lugha, mapitio kuhusu ufundishaji wa lugha ya pili, mapitio kuhusu utumizi wa fasihi katika ufundishaji wa lugha ya pili, mapitio kuhusu mtaala unaoegemea katika uwezo na mapitio kuhusu nafasi ya fasihi katika ukuzaji wa uwezo wa mwanafunzi. Nayo, sehemu ya kiunzi cha nadharia inajadili Nadharia ya Utambuzi na Nadharia ya Maingiliano ya Tamaduni-jamii kama nadharia zilizoongoza utafiti wetu kutoka mwanzo hadi mwisho.

Sura ya tatu ni methodolojia ya utafiti. Vipengele vilivyofafanuliwa katika sura hii ni pamoja na usanifu wa utafiti, eneo la utafiti, wango na sampuli ya utafiti, ukusanyaji wa data, uchanganuzi na uwasilishaji wa data, masuala ya kuthibiti ubora wa utafiti, na pia itikeli ya utafiti.

Sura ya nne ni mjadala wa matokeo ya utafiti ambapo imejumuisha suala la uchanganuzi wa data. Sura hii imeongozwa na maswali mawili ya utafiti ambayo yamegawanya sura hii katika sehemu kuu mbili ambazo nazo zimegawanywa katika visehemu vinne. Sehemu ya kwanza ni ufaafu wa fasihi katika ufundishaji wa lugha ya pili na utekelezaji wa mtaala unaoegemea katika uwezo. Sehemu hii nayo imegawanyika katika visehemu viwili. Kisehemu cha kwanza ni ufaafu wa fasihi katika ufundishaji wa lugha ya pili. Kisehemu hiki kina vipengele kadhaa ambavyo ni pamoja na ufaafu wa fasihi katika ufundishaji wa sarufi, ufaafu wa fasihi katika ufundishaji wa msamiati, ufaafu wa fasihi katika ufundishaji wa stadi za kuandika, ufaafu wa fasihi katika ufundishaji wa stadi za kusoma, ufaafu wa fasihi katika ufundishaji wa stadi za kusikiliza, na ufaafu wa fasihi katika ufundishaji wa stadi za kuzungumza. Kisehemu cha pili ni ufaafu wa fasihi katika utekelezaji wa mtaala unaoegemea katika uwezo. Kisehemu hiki nacho, kimegawanywa katika vipengele kadhaa ambavyo ni pamoja na ufaafu wa fasihi katika ukuzaji wa tafakuri tunduizi, ufaafu wa fasihi katika ukuzaji wa uwezo wa utafiti na utatuzi wa matatizo,

ufaafu wa fasihi katika ukuzaji wa ubunifu na ugunduzi, ufaafu wa fasihi katika ukuzaji wa stadi za mawasiliano, ufaafu wa fasihi katika ukuzaji wa uwezo wa ushirikiano, utawala binafsi na stadi za maisha, ufaafu wa fasihi katika ukuzaji wa uwezo wa ujifunzaji usio na mpaka, na ufaafu wa fasihi katika ujumuishaji na ufafanuzi wa maswala mtambuka.

Sehemu ya pili katika sura ya nne ni namna ya kutumia fasihi katika ufundishaji wa lugha ya pili na utekelezaji wa mtaala unaoegemea katika uwezo. Sehemu hii imegawanyika katika visehemu viwili. Kisehemu cha kwanza ni namna ya kutumia fasihi katika ufundishaji wa lugha ya pili. Katika kisehemu hiki tasinifu ilijadili namna ya kutumia fasihi katika ukuzaji wa tafakuri tunduizi, namna ya kutumia fasihi katika ukuzaji wa uwezo wa utafiti na utatuzi wa matatizo, namna ya kutumia fasihi katika ukuzaji wa ubunifu na ugunduzi, namna ya kutumia fasihi katika ukuzaji wa stadi za mawasiliano, namna ya kutumia fasihi katika ukuzaji wa ushirikiano, utawala binafsi na stadi za maisha, namna ya kutumia fasihi katika ukuzaji wa ujifunzaji usio na mpaka, na namna ya kutumia fasihi katika ufafanuzi wa maswala mtambuka.

Sura ya tano ni hitimisho la tasinifu hii. Katika sura hii, tasinifu ilijadili vipengele kama vile muhtasari wa tasinifu yote, matokeo ya utafiti huu, na mapendekezo kadhaa yanayostahili kupewa kipaumbele katika tafiti zijazo hususan zinazohusiana kwa namna fulani na utafiti huu.

**5.3 Utoshelevu wa Nadharia za Uchambuzi wa Data**

Tasinifu hii ilitumia Nadharia ya Utambuzi naMaingiliano ya Tamaduni-jamii. Nadharia hizi zimechangia pakubwa katika ufanikishaji wa matokeo ya utafiti huu. Nadharia ya Utambuzi imetusaidia katika kuhakikisha kwamba kila kazi ya fasihi iliyoshughulikiwa inajumuisha na kusisitiza uwezo na mchango wa mwanafunzi mwenyewe katika mchakato wake wa ujifunzaji. Nadharia hii imetusaidia kwa pande zote mbili ambazo ni upande wa ufundishaji na ujifunzaji wa lugha pamoja na upande wa ukuzaji wa uwezo wa mwanafunzi kama msingi wa utekelezaji wa mtaala unaoegemea katika uwezo. Kutokana na nadharia hii, utafiti uliweza kuchambua kazi mbalimbali za fasihi ili kujiridhisha juu ya maudhui yaliyokuwa yanajadiliwa katika kazi hizo juu ya ufundishaji wa lugha ya pili au utekelezaji wa mtaala unaoegemea katika uwezo. Utafiti huu ulifanikiwa kupata uthibitisho wa kutosha kwamba fasihi inafaa katika kukuza ubinafsi wa mwanafunzi kama mchango wa msingi katika ujifunzaji wake wa lugha ya pili.

Kwa upande mwingine, Nadharia ya Maingiliano ya Tamaduni-jamii ilitusaidia kutalii kwa kina uhusiano na mchango wa jamii pamoja na mazingira katika ufanikishaji wa ufundishaji na ujifunzaji wa lugha ya pili pamoja na ukuzaji wa uwezo wa mwanafunzi. Kutokana na nadharia

hii, tasinifu iliweza kufafanua mchango wa fasihi katika ujengaji wa mazingira na fursa za kumuunganisha mwanafunzi na jamii au mazingira. Pamoja na hayo, mwanafunzi anaathiriwa katika upataji na utendaji wa lugha pamoja na ukuzaji wa uwezo wake.

**5.4 Mchango Mpya wa Utafiti Huu**

Mchango wa kwanza kutokana na utafiti huu ni kugundua wamba fasihi inafaa kwa kufundisha lugha ya pili katika muktadha wa mtaala unaoegemea katika uwezo hususan nchini Rwanda. Kutokana na mifano iliyotolewa katika fasihi ambayo ni vielelezo vya kufundisha na kujifunza msamiati, sarufi, stadi za kusoma na kuandika na stadi za kusikiliza na kuzungumza, fasihi ni nyenzo mwafaka ya kufundishia lugha ya pili hususan kwa muktadha wa Rwanda ambapo mtaala unaoegemea uwezo umepewa kipaumbele.

Jambo lingine ni kwamba fasihi ni nyenzo ya kutekeleza mtaala unaoegemea katika uwezo. Hii inatokana na hoja ya kwamba fasihi hutoa mifano ya kukuza uwezo wa jumla wowote ule unaotarajiwa kukuzwa na kuendelezwa miongoni mwa wanafunzi kama inavyotarajiwa na mtaala unaoegemea uwezo. Aidha, fasihi haisahau kutoa mifano ya ufundishaji wamasuala mtambuka yanayotarajiwa kufafanuliwa wakati wa ufundishaji na ujifunzaji kwa kuegemea maoni ya mtaala unaoegemea uwezo.

Utafiti huu pia uligundua kwamba muhtasari wa Kiswahili nchini Rwanda, ulijenga mazingira mazuri ya utumizi wa fasihi kama nyenzo ya kufundishia lugha ya pili (Kiswahili). Kutokana na wazo la kwamba muhtasari huu huwa na mada nyingi za fasihi wakati hulenga ufundishaji wa lugha, tuligundua kwamba ni bora mada hizo za fasihi zitumike kama nyenzo ya kufundishia sarufi, msamiati, stadi za kusoma na kuandika pamoja na stadi za kusikiliza na kuzungumza.

Matokeo mengine ya utafiti ni kwamba muhtasari wa Kiswahili nchini Rwanda pia hutoa fursa ya kutumia fasihi kama nyenzo ya utekelezaji wa mtaala unaoegemea uwezo. Kutokana na msisitizo wa muhtasari huu juu ya ukuzaji wa uwezo wa jumla pamoja na ufundishaji wa maswala mtambuka, fasihi inaweza kuwa nyenzo mwafaka katika ufanikishaji wa mahitaji ya mtaala huu. Kingine ni kwamba mtaala huu unasisitiza ufundishaji wa maadili na mwenendo mwema wakati fasihi hushughulikia jambo hili kama jukumu.

Jambo jingine ni kwamba utumizi wa fasihi kama nyenzo ya kufundishia lugha huweza kuboresha muhtasari wa Kiswahili. Muhtasari wa Kiswahili nchini Rwanda unatenganisha fasihi na ufundishaji wa lugha ya Kiswahili. Kutokana na muhtasari huu, vipengele na stadi za lugha ya

Kiswahili zinazoshughulikiwa baada ya mada za fasihi hulenga kuielewa fasihi na siyo kujifunza lugha. Utumizi wa fasihi kama nyenzo ya kufundishia lugha, huweza kuimarisha muhtasari huu.

Jambo jingine ni kwambautumizi wa fasihi kama nyenzo ya kufundishia lugha, huelekeza moja kwa moja kwenye utekelezaji wa mtaala unaoegemea katika uwezo. Muhtasari wa Kiswahili hauzingatii uwezo wa jumla kama mada ya kufundisha. Kutokana na hali hii, baadhi ya walimu hufundisha bila kutilia maanani ukuzaji wa uwezo wa jumla fulani miongoni mwa wanafunzi. Kila wakati fasihi hujumuisha na kukuza uwezo wa aina moja au nyingine miongoni mwa wanafunzi.

Aidha, utafiti umegundua kwamba utumizi wa fasihi kama nyenzo ya kufundishia lugha, utaondoa woga uliomo miongoni mwa wanafunzi juu ya fasihi. Muhtasari wa Kiswahili sehemu ya fasihi inatenganishwa na sehemu ya sarufi. Aghalabu, walimu wa Kiswahili hujikita kufundisha sarufi tu nakukwepa fasihi. Fasihi inapotumiwa kama nyenzo ya kufundishia sarufi na sehemu nyingine za lugha, wanafunzi watazoea fasihi na kuondoa hofuya kwamba fasihi ni ngumu.

### 5.5 Maoni kuhusu Utafiti Huu

Licha ya utafiti huu kuchunguza nafasi ya fasihi katika ufundishaji wa lugha ya pili pamoja na utekelezaji wa mtaala unaoegemea uwezo, Utafiti huu umetusaidia kuyaangazia mambo kadhaa ambayo yanahusiana na utafiti huu kwa namna moja au nyingine. Hivyo basi, tumepata msingi na fursa ya kuyatolea maoni mambo hayo.

Jambo la kwanza, ni kwamba ni muhimu sana kufanya utafiti zaidi hasa katika utumizi wa fasihi katika ufundishaji wa lugha ya pili. Katika siku hizi, utumizi wa fasihi katika ufundishaji wa lugha ya pili haupewi thamani. Hali hii huathiri utendaji ya lugha ya mwanafunzi kutokana ukosefu wa mifano halisi ya utendaji wa lugha inayopatikana katika kazi za kifasihi. Kupuuzwa hukukunatokana na fikra potofu kwamba fasihi inatumia lugha isiyo ya kawaida wala isiyo mfano wa lugha ya mazungumzo halisi. Hali hii inasababisha walimu na wanafunzi kuogopa sehemu ya fasihi wakati ni nyenzo bora ya kufundishia vipengele na stadi zote za lugha yoyote ile.

Pili, ni tatizo la hali ya usomaji vitabu kwa walimu na wanafunzi nchini Rwanda ambao unadhihirisha upungufu mkubwa sana. Tatizo hili likiendelea kuwa jinsi lilivyo leo, itakuwa kikwazo katika utumizi wa fasihi katika kufundishia lugha na kutekeleza mtaala unaoegemea

katika uwezo. Hali hii inaathiri uteuzi na uchaguzi wa kazi za fasihi za kutumia kulingana na viwango vya wanafunzi kama jambo muhimu sana. Uzito wa tatizo hili unatokana na ukweli kwamba mwalimu hawezi kuchagua kazi ya fasihi inayofaa kwa wanafunzi bila kuisoma na kuielewa.

Tatu, ni tatizo linalohusiana na uandishi wa kazi za kifasihi hususan kazi za fasihi ya Kiswahili. Huenda waandishi wa kazi za fasihi ya Kiswahili wapo nchini Tanzania na nchi nyingine zisizo Rwanda. Labda hii ndiyo sababu nchini Rwanda hatuoni vitabu vya kazi za Kiswahili. Nchini Rwanda, kuna upungufu mkubwa sana wa idadi ya waandishi katika lugha ya Kiswahili, na hata wale wanaojaribu kuandika katika Kiswahili hawashughulikii sehemu ya fasihi. Hali hii inasababisha uhaba wa kazi za fasihi nchini Rwanda. Hali hii husababisha upungufu katika uga wa lugha na elimu.

Jambo la pili muhimu linahusiana na utengenezaji wa mitaala ya kufundishia katika ngazi mbalimbali za kielimu. Imebainika kwamba mitaala inavyotengenezwa haitoi fursa ya kutumia fasihi kama nyenzo ya kufundishia lugha wala kutekeleza mtaala unaoegemea katika uwezo. Vitabu vinavyotolewa kama vile silabasi na vitabu vya wanafunzi havizingatii fasihi kama nyenzo ya kuwasaidia walimu kufundisha lugha wala kutekeleza mtaala. Hali hii inatokana na watunga mitaala ya kuitazama fasihi kuwa ni somo kwa upande wake na lugha kuwa ni somo linalojitegemea kwa upande mwingine.

### 5.6 Mambo Yanayotakiwa Kuzingatiwa ili Kuondokana na Changamoto

Mosi, ni kuwahamasisha waandishi Wanyarwanda kuandika kazi za fasihi zaidi katika lugha ya Kiswahili. Hali hii inaweza kuvutia taasisi za Kiswahili na wadau wengine kushiriki katika uendelezaji wa Kiswahili hususan katika shule za viwango mbalimbali nchini Rwanda.

Pili, kuboresha muhtasari wa Kiswahili kwa kuzingatia fasihi kama nyenzo ya kufundishia lugha na kutekeleza mtaala unaoegemea katika uwezo. Hali hii itamotisha utendaji wa lugha ya Kiswahili katika shughuli mbalimbali za wanafunzi kwani watakuwa na uzoefu wake.

Tatu, ni kuhakikisha kwamba kazi za fasihi zinazojumuishwa katika silabasi zinalenga kukuza uwezo wa mwanafunzi. Hapa ieleweke kwamba kila kazi ya fasihi haikuzi uwezo wa mwanafunzi. Hali hii inatokana na ufaafu wa kazi husika kwa kiwango cha mwanafunzi pamoja na yaliyomo. Hivyo basi, ni bora taasisi za elimu nchini Rwanda zishughulikie suala hili.

### 5.7 Mapendekezo

Kutokana na tasinifu hii, mtafiti anapendekeza kwa makundi mbalimbali yanayohusika na ufundishaji na ujifunzaji wa lugha ya pili pamoja na utekelezaji wa mtaala unaoegemea katika uwezo. Makundi husika ni walimu na wanafunzi, waandishi na watunzi wa fasihi, serikali na tafiti zijazo.

#### 5.7.1 Mapendekezo kwa Walimu na Wanafunzi

Mtafiti anapendekeza walimu na wanafunzi waongeze jitihada kutumia fasihi katika ufundishaji na ujifunzaji wa lugha. Hii ni kutokana na ukweli kwamba fasihi haisaidii tu kupata lugha lengwa bali pia husaidia kukuza uwezo wa mwanafunzi wa kuitumiakatika miktadha ya maisha halisi. Ukuzaji wa uwezo huo miongoni mwa wanafunzi ndilo kusudi la mtaala unaoegemea katika uwezo. Hivyo basi, walimu na wanafunzi wakiipa thamani fasihi katika ufundishaji na ujifunzaji wa lugha, itawafanikishia kufikia utekelezaji wa mtaala unaoegemea katika uwezo.

Kwa upande wa lugha, mtafiti anapendekeza stadi zote nne za lugha zitiliwe nguvu kwa upande wa walimu na kwa upande wa wanafunzi. Ikiwa mtaala wetu unasisitiza utendaji wa lugha, basi ujuzi wa kuzungumza na kusikiliza unapaswa kutiliwa nguvu zaidi katika madarasa ya lugha na nje. Ili umilisi wa kuzungumza na kusikiliza uendelezwe zaidi, tunapendekeza hatua na mikakati ifuatayo wakati wa ufundishaji na ujifunzaji. Mosi, mwalimu anapaswa kuwa mfano mzuri wa kuigwa katika kila stadi. Pili, kuandaa, kusoma na kutumia kazi za kifasihi tofauti wakati wa ufundishaji na ujifunzaji. Tatu, kuwapa kazi nyingi wanafunzi hasa za kuwasilisha na kuwapa muda wa kujiandaa. Nne, kila mwanafunzi apewe na ajue majukumu yake wakati wa ufundishaji na ujifunzaji. Tano, ufundishaji wa maingiliano ya kitamaduni usipuuzwe. Sita, lugha mama itumiwe tu pale inapohitajika kama vile katika upangaji wa kazi za jozi na makundi na urekebishaji wa kazi ambazo hazishugulikiwi ipasavyo. Sita, kutekeleza na kudumisha nidhamu darasani.

#### 5.7.2 Mapendekezo kwa Watunzi wa Fasihi kwa Jumla

Watunzi wa kazi zinazohusiana na fasihi ziwe simulizi au andishi, wanapaswaa kuendelea kutunga kazi nyingizaidi. Hii itasaidia watumizi wa fasihi hususan walimu na wanafunzi kupata kila aina ya kazi kulingana na malengo, viwango, mahitaji, wakati na mazingira ya ujifunzaji. Kazi za fasihi zinapotungwa kwa wingi, walimu wataweza kupata na kutumia kazi zenye lugha

inayoeleweka kwa kila aina ya kiwango cha wanafunzi. Hali hii itaondoa shaka waliyo nayo ya kwamba fasihi hutumia lugha ngumu.

### 5.7.3 Mapendekezo kwa Serikali na Wakuzaji Mitaala

Kutokana namaoni ya walimu na wanafunzi juu ya utafiti wa tasinifu hii, utafiti unapendekeza serikali na watunga mitaala kuzingatia mambo yafuatayo: Mosi, kushirikiana kwa kujumuisha kazi za fasihi katika mihtasari ya lugha na vitabu vya wanafunzi kama nyenzo ya kufundishia na kujifunzia lugha. Pili, kusaidia na kumotisha watunzi wa kazi za fasihi ili waweze kutunga kazi nyingi iwezekanavyo. Tatu, kusisitiza utumizi wa fasihi katika ufundishaji na ujifunzaji wa lugha ili ifaidike kutokana na pande mbili muhimu katika elimu. Pande hizo ni pamoja na ufundishaji na ujifunzaji wa lughana utekelezaji wa mtaala unaoegemea katika uwezo.

### 5.7.4 Mapendekezo kwa Tafiti Zijazo

Tafiti nyingi zaidi zinatakiwa kufanyika kwa kuweka wazi uhusiano kati ya fasihi na elimu. Hii ni kutokana na ukweli kwamba fasihi huzingatia vipengele kadhaa vya kielimu ambavyo huweza kujumuishwa katika maendeleo ya nyuga na masomo tofauti ya kielimu. Japokuwa tasinifu hii imeziba mwanya uliolengwa kuzibwa, lakini bado kuna sehemu ambazo zinapaswa kufanyiwa uchunguzi na utafiti wa kina, sehemu hizo ni kama zifuatazo:

i: Nafasi ya fasihi katika ufundishaji wa masomo ya Kisayansi kama vile Kilimo, Hisabati, Kemia, Baiolojia na masomo mengine kama vile Ujasiriamali, Historia na Jiografia.

ii: Nafasi ya fasihi katika ufundishaji na ujifunzaji wa siasa, utaifa na uzalendo.

iii: Nafasi ya fasihi katika ujengaji wa umoja, ushikamano na upendo.

Iv: Utumizi wa fasihi katika ujengaji na uendelezaji wa itikadi za kidini.

Eneo jingine la kufanyia utafiti zaidi ni utekelezaji wa mtaala unaoegemea katika uwezo. Aghalabu, walimu na wanafunzi huendeleza mchakato wa ufundishaji na ujifunzaji bila kuongozwa na mwelekeo wa kukuza uwezo fulani. Wakati mwingine, walimu hupuuza sehemu ya kuunganisha maudhui na wanafunzi wakati wa ufundishaji na ujifunzaji. Hali hii inasababisha upungufu mkubwa katika utekelezaji wa mtaala unaoegemea katika uwezo.

Jambo la mwisho ni kufanya tafiti zaidi kwa kuweka wazi mamlaka iliyomo katika fasihi ili kufanikisha utekelezaji wa mtaala unaoegemea uwezo. Lengo kuu la mtaala wa kisasa

unaoegemea katika uwezo, mwanafunzi anatarajiwa kuwa na uwezo wa kufanikisha shughuli zake za maisha halisi hususan uwezo wa kupewa na kutimiza majukumu ya ajira. Kutokana na dhima ya fasihi ya kushughulikia maisha halisi ya watu, ni bora tafiti ziweke wazi uwezo fasihi iliyo nao katika ufanikishaji wa malengo ya mtaala unaoegemea katika uwezo.

## 5.8 Hitimisho

Katika sura hii tumetoa muhtasari wa tasnifu yote kuanzia sura ya kwanza hadi ya tano. Pia tumejadili mchango mpya uliotokana na utafiti huu. Jambo jingine linalojitokeza katika sura hii ni maoni ya jumla juu ya utafiti huu pamoja na mapendekezo kwa sekta mbalimbali zikiwemo walimu na wanafunzi, waandishi na watunzi wa fasihi, serikali na pia kwa tafiti zijazo.

## MAREJELEO


Achillah, A. (2010). Matumizi ya Mbinu ya Kimuktadha Katika Ufundishaji wa Msamiati wa Kiswahili Katika Shule za Upili za Wilaya ya Kakamega (Tasinifu ya Shahada ya Umahiri) Chuo Kikuu cha Sayansi na Teknolojia cha Masinde Muliro. Yanapatikana kwenye https://africantheses.org/abstracts/2658-14390.

Adom na wenzake (2016). Constructivism Philosophical Paradigm: Implication for Research, Teaching and Learning. *Global Journal of Arts Humanities and Social Sciences*. 4 (10), 1-9.

Aljoundi. E. K. (2014). Language Acquisition Theories. Yanapatikana kwenye *https://www.researchgate.net/publication/299657306*.

Anderson, R. S (2019). Do Animals Communicate Using a Language? ORCiD https://orcid.org/0000-0003-4477-1635.

Assey, P na wenzake (2007). *Mazingira ni Kitovu Cha Maendeleo Katika Tanzania*; Mafunzo yaliyotokana na Mchakato wa Mkakati wa Kukuza Uchumi na Kupunguza Umaskini (MKUKUTA). Toleo la Maliasili Na. 6. Taasisi ya Kimataifa ya Mazingira na Maendeleo. IIED, London, Uingereza.

Ates, H na Alsal. K (2012). The importance of lifelong learning has been increasing. *Procedia - Social and Behavioral Sciences 46.*

Babaee, R na Yahya. W. B. R. W (2014). Significance of Literature in Foreign Language Teaching. International Education Studies. (7) 4. ISSN 1913-9020.

Bradford, A. (2006). Reading Literature and Learning a Second Language. *Language Learning*. 18 (3 & 4), 199-210.

Chang, S & Tung. C (2009). Developing Critical Thinking through Literature Reading. *Feng Chia Journal of Humanities and Social Sciences*. (19) 287-317.

Chu na wenzake (2020). The Competency Based Curriculum Implementation: Appraisal from The Perspective of Teachers Use of Resources. *International Journal of Trend in Scientific Research and Development.* 2 (4), 2278-2288.

Chuo Kikuu Huria cha Tanzania (2008). *OFP 008 KISWAHILI*. Chuo Kikuu Huria cha Tanzania. Dar es Salaam, TANZANIA. www.out.ac.tz.

Creswell, J. W na Creswell. J. D (2018). *Research Design*: Qualitative, Quantitative, And Mixed Methods Approaches (5TH edition). Los Angeles: SAGE Publications Ltd.

Daskalovska&Dimova (2012). Why Should Literature Be Used in The Language Classroom? *Procedia - Social and Behavioral Sciences. 46, 1182 – 1186.*

Economou, C. (2015). Reading Fiction in a Second-Language Classroom. *Education Inquiry*. 6 (1), 99-118.

Elkiliç, G na wenzake (2011). The Use of Literature in Teaching English Grammatical Structures as well as Some Linguistic Components. *International Education Studies*. 7 (4).

FHI 360. (2005). *Family Planning Needs in the Context of the HIV/AIDS Epidemic.* FHI 360, Johannesburg, South Africa.

Ford, K. (2014). Competency-Based Education: History, opportunities, and challenges. University of Maryland University College. DOI:10.13140/RG.2.1.4679.0885

Griffiths, P. (2002). What Is Innateness?*The Monist*. 85(1) DOI:10.2307/27903758.

Hapsari, A. (2016). Literary Competence for The Teaching of Literature in Second Language Educational Context. https://www.researchgate.net/publication/312574248.

Harerimana, F. (2017). *Tujivunie Lugha Yetu, Kitabu cha Mwanafunzi*: Kidato cha Tano, Mchepuo wa Lugha. MK Publishers Ltd, Kigali-Rwanda.

Henrietta, T na Antonela. T (2021). The Role of Literature as Vocabulary Teaching Instrument of a Foreign Language in Middle School. *Educatia 21 Journal*. (20), 09.

Henrietta. T & Antonela. T (2021). The Role of Literature as Vocabulary Teaching Instrument of a Foreign Language in Middle School. *Educatia 21 Journal*. (20), 09. http:// files.eric.ed.gov/fulltext/ED114384.pdf.

Idrissova na wenzake (2015). Improving listening and speaking skills in mixed level groups (on the material of New English File). *Procedia - Social and Behavioral Sciences*. An International Conference on Teaching and Learning English as an Additional Language, Antalya – Turkey.

Ismail1, A. I na Sharan. V, (2019). Teaching Writing Skill through English Literature: Palestine as an Example. *International Journal of Science and Research (IJSR)*. ISSN: 2319-7064.

Jyotsna, J & Dwarakanath. T, (2018) Teaching Life-Skills through Literature. International *Journal of Research and Scientific Innovation (IJRSI)*. 5(6).

Kabombwe & Mulenga, (2019). Implementation of The Competency-Based Curriculum by Teachers of History in Selected Secondary School in Lusaka District, Zambia. ResearchGate. 22:19-41. 10.17159/2223-0386/2019/n22a2.

Karanja, J. (2016). A *Guide to Research Proposal and Thesis Writing*. http://ssrn.com/abstract=2746361 or http://dx.doi.org/10.2139/ssrn.2746361.

Kitta, S. & Tilya.F. (2010). Assessment Status of Learner-Centred Learning in Tanzania in The Context of the Competence-Based Curriculum.*University of Dar es Salaam Journals.* https://journals.udsm.ac.tz/index.php/ped/article/view/1449.

Kothari, C. (2010). *Research Methodology*: Methods and techniques. New Delhi, Daryaganj: New age international. Ltd. Publishers.

Malan, S. P. T. (2000). The "New Paradigm" Of Outcomes- Based Education in Perspective. *Journal of Family Ecology and Consumer Science*, *28*, 22–28.

Matos, C. L & Afsarmanesh, H (2008). *Concept of Collaboration.* IGI Global, Hershey.

Maxwell, A. E. (1961). *Analyzing Qualitative Data*. New York: John Wiley & Sons, 1961.

Mazrui, A. (1981). *Kilio cha Haki*. Nairobi. Longhorn Publishers.

Mulyani, P. K. (2019). Innatist and Interactionist Learning Approaches of Elementary School Students' Language Acquisition. *Humaniora*. 31 (1), 14-20.

Mutembei, K. A. (2018). Fasihi ya Kitaifa na Fasihi ya Kiswahili ni Dhana ile ile? Chuo Kikuu cha Dar es Salaam. https://journals.udsm.ac.tz/index.php/mj/article/download/1582/1476.

Ndihokubwayo na wenzake (2021). Is Competence-Based Curriculum Well Monitored? Learning from Rwandan sector education officers. *Rwandan Journal of Education*. 5 (1).

Nodine, T. & Johnstone, S.M. (2015). Competency- Based Education: Leadership challenges. Change: *The Magazine of Higher Learning*, *47*(4), 61–66.

Nodine, T. R. (2015). How Did We Get Here? A brief history of competency- based higher education in the United StateS. ResearchGate. 1(1):5-11.

Nsengimana, V. (2021). Implementation of Competence-Based Curriculum in Rwanda: Opportunities and challenges. *Rwandan Journal of Education*. 5 (1).

Nzima, I. (2016). Tutors' Interpretations of Competence-Based Curriculum in Tanzania: Implications for practice in teacher education. *Journal of Education of the University of Dar es Salaam.*

Nzima, I. (2021). Implementation of Competence Based Curriculum in The Context of Colonial Education System in Tanzania. *International Journal of Research Studies in Education*. 10 (5), 33-43.

Opunde, S. (2015). Mwelekeo Mseto Katika Ufundishaji wa Lugha ya Kiswahili. Yanapatikana kwenye https://www.researchgate.net/publication/346496276.

OECD (2020). *Achieving the New Curriculum for Wales*, Implementing Education Policies. OECD Publishing, Paris.

Pantaleo, S. (2002). Children's Literature Across the Curriculum: An Ontario Survey.*Canadian Journal of Education / Revue canadienne de l' éducation* 27(2), 211-230.

Pardede, P. (2011). Using Short Stories to Teach Language Skills. Journal of English Teaching. (1),1, 14-27.

Parveen, H. & Showkat. N. (2017). Research Ethics. https://www.researchgate.net/publication/318912804

Ponera, A. (2019). *Misingi ya Utafiti wa Kitaamuli na Uandishi wa Tasinifu*. Dodoma, Central Tanganyika Press.

Rahman, F (2016). TheStrategyof Teaching Literature Through Language-Based Method: ACommunicativeApproach. The Annual Seminar on English Language Studies 2016.https://www.researchgate.net/publication/324331407

REB, (2015). *Competencebased curriculum*: Summary of curriculum framework pre-primary to upper secondary 2015. WordCore Communications Limited.

Richard, J. C & Rodgers, T (2001). Approaches and Methods in Language Teaching. New York: Cambridge University Press.http://dx.doi.org/10.1017/CBO9780511667305.021.

Rupeja, T. (2021). Implementation of Competence Based Curriculum in The Context of Colonial Education System in Tanzania. *International Journal of Research Studies in Education*. (5), 33-43.

Samúelsdóttir, (2015). The Innateness Hypothesis: Can Knowledge of Language Be Inborn? Unpublished manuscript. Háskóli Íslands.

Shkak, J. & Hassan. H (2020). Competency Based Curriculum: Challenges Around Supply Chain Management in the Oil Marketing Companies Operating in the Kurdistan Region of Iraq View Project. ResearchGate. https://www.researchgate.net/publication/345997202.

Sinnema, C. (2011). Monitoring and Evaluating Curriculum Implementation: Final Evaluation Report on the implementation of the New Zealand Curriculum 2008-2009. Ministry of Education, New Zealand. www.educationcounts.govt.nz/publications.

Spady, W.G. (1994). Outcome-Based Education: Critical Issues and Answers. *American Association of School Administrators*. North Moore Street: Arlington.

Starja, A. (2015). The Impact of Literature in Teaching a Foreign Language – A Case Study On the Use of Drama and Its Practical Implications. *European Scientific Journal*. .11 (14).

Tabaro, C. (2013). Code-Switching in Rwanda: A Case Study of Kigali City Secondary Schools. *A Multidisciplinary Journal of Southeast Asia*. (13), 14–26.

Taherdoost, H. (2016), Validity and Reliability of the Research Instrument; How to Test the Validation of a Questionnaire/Survey in a Research. *International Journal of Academic Research in Management (IJARM)* 5 (3) 28-36.

Terrell, S. R. (2016). *Writing a Proposal for your Dissertation*: Guidelines and Examples. New York: A Division of Guilford Publications, Inc.

UNICEF, (20219). *Global Framework on Transferable Skills*. New York, United Nations Plaza, UNICEF.

Urunana rw'Abarezi, (2018). *Implementing CBC*: Successes and Challenges. https://rwanda.vvob.be/publications.

Wambui, W. T (2015). *Communication Skills, Students Coursebook*. Deutschland, Saarbrūken: LAP Rambert Academic Publishing.

Wang and Yang, (2012). Problems and Strategies in Learning to Write a Thesis Proposal: A study of six M.A. students in a TEFL program. *Chinese Journal of Applied Linguistics.* 35 (3), 324–341.

Williams na wenzake, *(2019).* The Virtual Census: Representations of Gender, Race and Age in Video Games. *New Media & Society*. 11(5):815-834.

Wintersparv, S. (2020). Teaching Literature: From A Teacher's Viewpoint to A Researcher's. *Kulturella Perspektiv och författaren*. 3 (29), 57–64.

Yi, J. (2009). Defining writing ability for classroom writing assessment in high schools. *Journal of Pan-Pacific Association of Applied Linguistics,* 13(1), 53-69.

Zaker, A (2016). Literature and Creativity in an ELT Context. *ASIAN TEFL*. (1)2. www.asian-tefl.com.

# VIAMBATANISHO

## KIAMBATANISHO A

## A.1 MIONGOZO YA MBINU ZILIZOTUMIKA KUKUSANYA DATA ZA UTAFITI HUU

### A.1.I Mwongozo wa Mahojiano kwa Wanafunzi wa Kiswahili

1. Fasihi ni nini?

2. Uwezo ni nini?

3. Je, ni nini maana ya mtaala unaoegemea katika uwezo?

4. Je, unafikiri kwamba ni jinsi gani fasihi ya Kiswahili inaweza kufaa kwa kukufundisha lugha ya Kiswahili?

5. Ni namna gani fasihi inaweza kufaa kwa kukuzia uwezo wa maishani halisi?

6. Je, unafikiri mwalimu wako wa Kiswahili anaweza kutumia vipi fasihi ya Kiswahili ili kukusaidia kujifunza lugha ya Kiswahili?

7. Je, unafikiri mwalimu wako wa Kiswahili anaweza kutumia vipi fasihi ili kukusaidia kukuza uwezo wako wa maisha halisi?

### A.1.II Mwongozo wa Mahojiano kwa Walimu wa Kiswahili

Wakati wa kukusanya data kutoka kwa walimu wa fasihi ya Kiswahili, mtafiti aliuliza maswali yafuatayo kwa njia ya mahojiano:

1. Nini maana ya uwezo?

2. Je, mtaala unaoegemea katika uwezo ni nini?

3. Fasihi ni nini?

4. Je, ni namna gani fasihi inaweza kujumuisha mifano ya kufundishia lugha?

5. Jadili jinsi fasihi inaweza kutoa mifano ya kukuza uwezo wa jumla miongoni mwa wanafunzi.

6. Ni jinsi gani fasihi inaweza kujumuisha mifano ya maswala mtabuka ikiwemo thamani na mwenendo mwema?

7. Je, kwa namna gani unadhani fasihi ya Kiswahili inaweza kutumiwa kama nyenzo ya kufundishia na kujifunzia lugha ya Kiswahili?

8. Je, ni kwa namna gani unafikiri fasihi ya Kiswahili inaweza kukuza uwezo wa mwanafunzi katika ulimwengu halisi?

9. Je, ni vipi fasihi inaweza kuchangia katika utekelezaji wa mtaala unaozingatia katika uwezo?

7. Kama mwalimu wa lugha ya Kiswahili, eleza jinsi unavyoweza kufundisha lugha ya Kiswahili kupitia fasihi ya Kiswahili?

8. Kama mwalimu wa fasihi ya Kiswahili, eleza jinsi unavyoweza kufundisha fasihi ya Kiswahili kuelekea utekelezaji wa mtaala unaoegemea katika uwezo?

**A.1.III Mwongozo wa Ushuhudiaji kwa Walimu na Wanafunzi wa Kiswahili (Darasani)**

Mwongozo wa ushuhudiaji kwa walimu na wanafunzi wa wa Kiswahili na darasani ulikuwa

unachunguza mambo yafuatayo:

1. Kuchunguza ikiwa walimu wa Kiswahili hutumia fasihi wanapofundisha lugha.

2. Kuchunguza jinsi ambavyo walimu wa Kiswahili hujumuisha fasihi katika shughuli za ufundishaji na ujifunzaji wa lugha ya Kiswahili.

3. Kuchunguza kama na jinsi wanafunzi wanafurahia fasihi wakati wa ufundishaji na ujifunzaji darasani.

4. Kuchunguza ikiwa walimu wa Kiswahili wanatumia fasihi katika kukuza uwezo wa lugha na uwezo wa maisha halisi kwa wanafunzi.

**A.1.IV Mwongozo wa Uchambuzi wa Matini**

Katika mchakato wa ukusanyaji wa data, tulitumia uchambuzi wa matini ambapo mtafiti alichambua baadhi ya nyaraka za mwalimu, maandiko mbalimbali kuhusu mtaala unaoegemea katika uwezo, muhtasari wa Kiswahili na baadhi ya kazi za fasihi ili kutoa miongozo ya jinsi matumizi ya fasihi yanavyoweza kufaa katika ufundishaji na ujifunzaji wa lugha ya pili na kusaidia katika utekelezaji wa mtaala unaoegemea katika uwezo. Maandiko yaliyopitiwa ni yale

ya maktabani na kwenye vyanzo vya kielektroniki vinavyohusisha Taasisi zinazojulikana na kuaminika.

Mwongozo wa uchambuzi wa matini umefafanuliwa katika jedwali lifuatalo:

| **Vyanzo vya Maarifa** | **Vipengele Vinavyopitiwa** | **Lengo** |
|---|---|---|
| Vitabu, tasnifu, makala, tahakiki, majarida na vyanzo vya kieletroniki. | Vitabu vya fasihi kwa jumla, nakala vitabu vinavyohusiana na mtaala unaoegemea uwezo pamoja na utekelezaji wake, vitabu na tasinifu zinazohusiana na ufundishaji wa lugha ya pili. | Kupata mawazo/ taarifa mbalimbali kutoka kwa wataalamu mbalimbali kuhusiana na mada ya utafiti. |

**KIAMBATANISHO B**

**Barua ya Kibari cha Kufanyia Utafiti Kutoka Chuo**

UNIVERSITY *of* RWANDA

COLLEGE OF EDUCATION

RESEARCH AND INNOVATION UNIT

Rukara, 7th December 2021
Réf: 03/DRI-CE/083/EN/gi/2021

**The Mayor**
**Rusizi District**
**Western Province**
**Rwanda**

**Re: Research recommendation letter for Mr. Donard Bikorimana**

On behalf of the University of Rwanda-College of Education (UR-CE), I am pleased to introduce Mr. Donard Bikorimana, a post-graduate student at the School of Education of UR-CE. Mr. Bikorimana is writing his thesis on: **"Nafasi ya fasihi katika ufundishaji wa lugha ya pili na utekelezaji wa mtaala unaoegemea katika uwezo: *mfano wa ufundishaji wa Kishwahili wilayani Rusizi* (The Role of Literature in Teaching Second Language and Implementing Competency-Based Curriculum)"** to complete his Master of Education in Kiswahili Education.

He wishes to analyze the contribution of literature in teaching a second language and help in Competency-Based Curriculum implementation among Kiswahili teachers and learners in selected Rwandan secondary schools. In this regard, he needs permission to collect data from some selected secondary schools in the Rusizi district. The research participants are teachers of Kiswahili and their students at the advanced level (senior five of Literature-Kinyarwanda-Kiswahili (LKK)).

Mr. Bikorimana's research project passed successfully through an internal collegial ethical process. Thus, the University of Rwanda-College of Education: Directorate of research and Innovation confirms that his research adheres to ethical standards and principles. Therefore, we will appreciate it if you provide him with the necessary support he may require to undertake his research.

Please do not hesitate to contact us at wrceresearchin@gmail.com for further clarification if it is needed. We very much hope to get your usual cooperation in serving our nation.

Yours sincerely.

COLLEGE OF EDUCATION ★ UNIVERSITY of RWANDA ★ RESEARCH AND INNOVATION UNIT

**Digitally signed by**
**UR (Rukara, Directorate of Research & Innovation)**
**Date: 2021.12.07**
**Time: 14:05:09 +2'00**

**Assoc. Prof. Eugene Ndabaga**
Director of Research and Innovation
University of Rwanda-College of Education
E-mail: ndabagav@yahoo.ie
Mobile: +250788308862

**Cc:**

- Principal, UR-CE
- Postgraduate Program Coordinator, School of Education
- Dr. Wallace K. Mlaga (Supervisor)

EMAIL: dri.ce@ur.ac.rw P.O. Box: 55 Rwamagana WEBSITE: www.ur.ac.rw

## KIAMBATANISHO C

### Barua ya Kibari cha Kufanyia Utafiti Kutoka Wilaya ya RUSIZI

REPUBLIC OF RWANDA

Rusizi, 29/12/2021
N° ..5846./03.06

WESTERN PROVINCE
RUSIZI DISTRICT
TEL. 0788868429/ 0788660191
www.rusizi.gov.rw
rusizidistrict@rusizi.gov.rw
P.O BOX 253 RUSIZI

Mr Donald BIKORIMANA
MUGANZA Sector
RUSIZI DISTRICT
PHONE NUMBER: 0785552305
E-MAIL: bpatientdona@gmail.com

Dear Sir,

**Subject : Feed back to your data collection request**

Reference is made to your letter of 13/12/2021 applying for a permission for data collection in RUSIZI DISTRICT;

I am pleased to inform you that a permission for data collection you have requested for is granted to you in RUSIZI District. The data you are allowed to collect are only those related to your topic entitled ***"The Role of Literature in Teaching Second Language and Implementing Competence- Based Curriculum "***. Please note that all data collected should be only used for academic purpose, and the results of your study should be shared with the management of RUSIZI District. The focal point in this activity is the Director of Education Unit.

Sincerely,

**MUTESI Priscah**
Executive Secretary of RUSIZI District

**Cc :**

- The Mayor of RUSIZI District
- The Vice- Mayors (All)
- The Ag. Corporate Services Division Manager
- The Director of Human Resources and Administration
- The Director of Education Unit

**RUSIZI**

# VIAMBATANISHO D

## PICHA MBALIMBALI ZINAZOHUSIANA NA UTAFITI



Picha iliyochukuliwa wakati wa ushuhudiaji

Mtafiti akishuhudia ufundishaji na ujifunzaji

katika kidato cha tano, shule ya sekondari

ya Muganza wilani RUSIZI.



Picha iliyochukuliwa wakati wa ushuhudiaji

Mtafiti akishuhudia ufundishaji na ujifunzaji

katika kidato cha tano, shule ya sekondari

ya MUREHE wilani RUSIZI.



Picha ya ushuhudiaji darasani kwenye shule ya Sekondari ya Mashesha wilayani RUSIZI.



Picha ya mahojiano kati ya mtafiti na mwanafunzi katika ukusanyaji wa data kwenye shule ya sekondari ya Hanika wilayani RUSIZI.